# MUHTASARI WA

# MLANGO WA KUINGILIA KATIKA QUR'AN TAKATIFU

# UWASILISHAJI WA KIHISTORIA NA UCHAMBUZI LINGANISHI

*Kimefasiriwa na Sheikh Omari J. Mangilile*

*Kimepitiwa na Shaibu Swalehe Saidi*

*June 2021*

بسم الله الرحمن الرحيم

**DR. MOHAMMED ABDULLAH DURAAZ**

**MLANGO WA KUINGILIA KATIKA**

# QUR`AN TAKATIFU

**UWASILISHAJI WA KIHISTORIA NA UCHAMBUZI LINGANISHI**

**TAFSIRI NA UFUPISHO KWA KIARABU NA**

**MUHAMMAD ABDUL-ADHIIM ALI**

**TAFSIRI NA UFUPISHO KWA KISWAHILI NA**

**OMARI JUMA MANGILILE**

**NA KUPITIWA NA KUHAKIKIWA NA SHAIBU SWALEHE SAIDI**

**Haki miliki zimehifadhiwa**

**Chapa ya pili**

**1440 H – 2019 AD**

Namba ya ISBN – Darul Kutubil Misriyyati

2019 AD

## UTANGULIZI WA MUHTASARI

Licha ya kupita, takribani nusu karne tangu kufanyika kwa utafiti huu adhimu, kwa hakika matokeo yake bado hayafahamiki na hayajasambaa baina ya Waislamu. Licha ya umuhimu na ulazima wake, hasa hasa katika zama hizi ngumu na mazingira ya ulimwengu yaliyojazwa chuki dhidi ya Uislamu. Hilo limepelekea kuandaliwa kwa ufupisho wa utafiti huu adhimu ili kuwafikishia wasomaji wengi wa Kiarabu (Kiswahili) juhudi hizo za kielimu za mmoja wa wanazuoni wabobezi wa Kiislamu wa zama hizi. Kisha kuuwasilisha muhtasari huu kwa mpendwa msomaji ukiwa katika umbo dogo, muundo mwepesi, na uwasilishwaji rahisi. Ili ufahamike haraka, faida yake ienee kwa wote na kuchangia katika kuzuia changamoto zinazoukabili Uislamu. Pia, ili watu wote waone sura halisi ya Qur`an Takatifu. Qur`an ambayo haijateremshwa na Allah vingine ila iwe rehema kwa watu wote.

Allah amrehemu mpendwa wetu Dr. Mohammed Abdullah Duraaz. Ampe thawabu nyingi kwa kile alichokitoa katika kuutumikia Uislamu na Waislamu..

*Allah ndiye mlinzi mwenye kuwafikisha.*

*Alexandria: mnamo 10 Novemba 2017*

*Inayoafikiana na 6 ya Mfunguo Mosi 1439*

***MUHAMMAD ABDUL-ADHIIM ALI***

## Ufupisho wa dibaju ya mwandishi

Tunaweza kuisoma na kuitafiti Qur`an Takatifu kwa pembe nyingi, lakini pembe zote hizo zinaishia katika mambo makuu ya msingi mawili.. Nayo ni lugha na fikra. Qur`an Takatifu ni kitabu cha kifasihi na kiitikadi kwa wakati huo huo na kwa kiwango hicho hicho. Na kwa upande huu wa pili, nao ni kwamba Qur`ani ni hazina ya fikra zinazodhihiri kwa kupitia muundo na mtindo wake wa kifasihi wa kiwango cha juu mno. Muundo na mtindo huo tunauwasilisha hapa katika mapote matatu nayo ni: La kwanza: tabia ya wito wake, yaani mkusanyiko wa majibu yanayotolewa na Qur`an kutatua matatizo makuu mawili ya muda mrefu, nayo ni maarifa na tabia. Pote la pili ni: mtindo na muundo wa hoja toshelevu zitumikazo kuthibitisha ukweli wa wito wake. Na mwisho ni: hoja za kiakili zitumikazo kutolea ushahidi juu ya sifa ya kiuungu iliyotakatifu katika ujumbe wake.

Kwa hakika lengo la awali la utafiti huu lilikuwa kupata kanuni za kimaadili za kiqur`an zilizo mbali kabisa na kila kinachofungamana na mambo mengine yaliyosalia ya Qur`an Takatifu. Na hiyo ni kazi tuliyoiandalia kitabu kingine (kilichofasiriwa kwa Kiarabu kwa jina la: Dasturu Al-Akhlaaq Fiil Quraan – Desturi ya tabia njema katika Qur`an). Hata hivyo tumeonelea kuwa jambo la faida ni kuwasilisha fremu/ramani kuu ya jengo hili la kifikra lililo refu mno. Na kuweka wazi sehemu yenye jambo la kimaadili ndani ya fremu kuu. Na zaidi ni kuongeza utoaji wa mawazo makuu yaliyomo katika kila kifungu miongoni mwa vifungu vya kitabu cha Uislamu.

Na baada ya kuwasilisha nukta kadhaa za kihistoria kutokana na mapendekezo ya (Miso Maurice Patronier De Janndiak) Profesa wa Sorbonne.

Kwa hakika maudhui makuu ya utafiti wetu huu ni kuwasilisha ujumbe wa Qur`an Takatifu kwa ujumla wake kama inavyowasilishwa na Qur`an yenyewe. Na sio kama ilivyokuja kupitia hukumu au maelezo au ufafanuzi au utekelezaji ambao kiwango chake cha nia njema kinatofautiana kwa vipindi tofauti tofauti vya kihistoria. Kwa hiyo katika njia yetu ya kuhusiana na Quran, tutakabiliana imma na baadhi ya hukumu ngumu na kuzisahihisha au baadhi ya fahamu za haraka na kuzirekebisha. Na kwa yote haya, tutaiacha Qur`an isimamie namna ya kujitetea yenyewe kwa yenyewe na kutoa hoja baada ya hoja.. Tukimwachia msomaji nafasi ya kukadiria yeye mwenyewe kima cha hoja hizi kihistoria na kifalsafa.

Na jambo la kutajwa ni kwamba, kung`amua fikra ya Quran kutoka katika kava lake na kuitoa kwa namna hii, kutoka katika wigo wake wa kieneo na kuikurubisha na fikra za Ulaya zilizo mbali na lugha ya Kiarabu. Huko ndiko kufikia sehemu ya malengo ya ujumbe wa kweli wa Quran. Kwa kuwa Quran inamlenga kila mtu popote na vyovyote alivyo. Na hilo, ni pale Quran inapoelekeza wito wake kwa akili, ufahamu ulio salama na hisia njema kwa mwanadamu. Kwa hakika Quran ni wito wa dunia nzima unaolenga kusafisha ada mbaya, kuweka wazi itikadi na kuziweka karibu. Na kuondosha vizuizi vya kibaguzi na kiutaifa. Na kuweka kanuni ya haki na uadilifu mahali pa kanuni ya kutumia nguvu za ukandamizaji.

Parisi 21 Februari 1947

MOHAMMED ABDULLAH DURAAZ

# MLANGO WA KWANZA

# UKWELI WA KWANZA

# WA KIHISTORIA

## Utangulizi

Kabla ya kuanza utafiti wa kisomi juu ya kitabu cha Uislamu, tunakumbusha mazingira ambayo ndani yake Quran Takatifu imeteremshwa, na hatua zilizopitiwa na Quran hadi kufika mikononi mwetu.

Vyovyote vile kitakavyokuwa chanzo cha imani ya juu ya Quran, kwa hakika jambo lililothibiti Kihistoria ni kuwa, Quran inarejea kwa Muhammad bin Abdillah rehema na amani ziwe juu yake. Hiyo ni sawa sawa, ikiwa ameitunga kutoka ndani ya nafsi yake, au kutokana na ujuzi wake juu ya mazingira yake – kama wasemavyo makafiri – au ni kwamba yeye ameipokea hiyo Quran neno kwa neno kwa kusomewa na mjumbe wa mbinguni ambaye ni kiunganishi baina yake na Allah – kama Quran yenyewe inavyokazia dai hili. (Ameteremsha haya Mhuyisha Sharia mwaminifu, (Jibrili). As-shuaraa 26:193, (Sema: ‘’anayemfanyia ushinde Jibril (kwa kuwa ndiye aliyemletea utume nabii Muhammad asiwapelekee Mayahudi) (ni bure, hana kosa Jibril); hakika yeye ameiteremsha Quran moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (sio kufanya kwa kupendelea kwake); (Quran) inayosadikisha yale yaliyokuwa kabla yake, na ni uwongozi na khabari njema kwa wanaoamini). Al Baqarah 97.

Na kwa vile elimu zetu zenye mipaka maalumu haziwezi kupanda hadi kufikia chanzo hiki cha mbali na uwezo wa kibinadamu, kwa vyovyote vile, sisi tumeipokea kutoka kwa Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, sawa sawa kuwa yeye ndiye mtunzi wake au yeye ndiye wa pekee anayeifikisha kwa binadamu wote.

## Sura ya kwanza:
## Maisha ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kabla ya kupewa Utume.

Kwa kuangalia uhusiano mkubwa baina ya Mtume na ujumbe wake, tunaanza kwa kuwasilisha taswira fupi ya maisha ya Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, tangu utotoni mwake hadi wakati anakabidhiwa dhamana ya ujumbe wake kwa watu wote.

**Kwa hiyo, ni nani hasa huyu mhusika?**

Muhammad anatoka katika familia bora ya Makka, ya kabila la Qureyshi, tawi la Banii Haashimu linalosifika kuwa limeshinda katika upande wa unyenyekevu na uchamungu kuliko katika nguvu zake za kisiasa. Maelezo ya kihistoria yanalinasibisha na kizazi cha Ismaili mwana wa Ibrahimu kwa idadi kadhaa ya vizazi ambavyo sisi bado hatujapata uhakika wa idadi na majina yake isipokuwa vizazi ishirini na moja tu, navyo ni vile vya mpaka kufika kwa Adnaani. Mtume rehema na amani ziwe juu yake amezaliwa siku ya Jumatatu ya wiki ya pili ya mwezi wa Mfunguo Sita (mwezi wa tatu wa kalenda ya Kiislamu ya Hijiriya) ya mwaka wa Ndovu yaani ni tarehe ya vita vya Hijazi (Vilivyoshindwa) vilivyoendeshwa na ((Abraha)) gavana wa Yemeni chini ya utawala wa Byzantine kwa miguvu ya jeshi lake likishirikiana na kiasi kikubwa cha ndovu wa falme ya Habeshi (Ethiopia).

Kwa hakika Mtume Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alizaliwa akiwa yatima. Baba yake ambaye ni Abdullah alifariki kabla ya kuzaliwa Mtume kwa miezi saba. Akapelekwa kwa mnyonyeshaji mkazi wa jangwani aitwae Halima wa kabila la Banii Saadi mpaka alipofikia miaka minne. Na kama ilivyokuwa ada ya Waarabu waheshimiwa wa wakati huo ya kuwapeleka watoto wao wakalelewe na kukulia katika mazingira safi ya majangwani. Kisha mama yake akasimamia malezi yake akisaidiwa na dada wa kazi aitwae Ummu Aymani. Hata hivyo, Mtume hakufurahia kupata mapenzi ya mama yake kwa muda mrefu. Kwani mama yake naye alifariki hali yeye akiwa na umri wa miaka sita. Akachukuliwa na babu yake ambaye ni Abdul-Mutwalibi naye akampendelea kwa mapenzi na upole wake. Na akamtabiria mustakbali mwema. Punde tu, Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alipofikia miaka minane alimpoteza babu yake. Na ami yake (baba yake mdogo) ambaye ni Abdu Manafi aliyepachikwa jina la Abuu Twaalibi akasimamia

malezi yake. Akampa mapenzi ya moyoni kama ya baba na mama licha ya kuwa yeye mwenyewe hakuwa na hali nzuri ya kiuchumi huku akiwa na watoto wengi. Hata hivyo, Abuu Twaalibi aliona nafuu na hali nzuri kiasi ya maisha tangu ile siku kijana huyu alipoingia katika nyumba yake. Kwa ajili hiyo akawa anapendelea mno huyu Muhammad rehema na amani ziwe juu yake awe karibu naye daima. Na kwa hisia za kubadilishana, naye kijana huyu alikuwa hawezi kuvumilia kuwa mbali na ami yake. Kwa hiyo, tunamuona Muhammad rehema na amani ziwe juu yake (naye akiwa na umri wa miaka kumi na miwili) anaenda pamoja na ami yake katika safari ya kwenda Syiria mwaka 582 AD kwa ajili ya biashara.

Katika safari hii kinapatikana kisa mashuhuri cha kukutana kwa mara ya kwanza baina Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na duru za kidini kwa mtu mchamungu wa Kikristo ambaye ni Bahira huko Busra nchini Syria. Athari zinatusimulia kuwa, mchamungu huyu aliona baadhi ya alama za utume zilizoandikwa katika vitabu vitakatifu zikiendana na msafara huu. Hivyo basi, akauita huo msafara uende ukale kwake. Kisha akaanza kuchunguza nyuso za watu wa msafara huo na kuzilinganisha na zile alama zake zilizomo katika maandiko bila ya kupata chochote. Lakini mwishoni alipoongea na Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, ambaye ni kijana mdogo aliyekawia kufika katika sehemu hiyo, alimsogelea Abuu Twaalibi na kuongea naye kuwa ‘‘Kijana huyu atafanyakazi kubwa duniani, mrejeshe haraka nchini kwake, mlinde na uchukue tahadhari kumkinga dhidi ya Wayahudi ambao huenda wakamdhuru endapo watajua kwake yale ninayoyajua’’[1].

Na hatujui isipokuwa maelezo machache kuhusu historia ya maisha yake ya tangu kipindi hicho hadi anaoa. Na kwa ujumla ameutumia ujana wake katika hali inayokaribiana na umaskini. Na hili linaungwa mkono na Quran[2] na kufafanuliwa na Sunna. Baada ya kufiwa na baba yake na kuishi chini ya malezi ya babu yake, hakurithi kutoka kwa mama yake ila mjakazi mweusi, kundi la kondoo na ngamia watano. Kazi aliyokuwa akiifanya katika kipindi hicho kwa kiasi kikubwa ilikuwa ni kuchunga mbuzi. Na kuhusu kazi hiyo, Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasema hiyo ni kazi ya Manabii wa kabla yake akiwemo Musa, Daudi na wengineo.

[1] Sira ya Ibnu Hishaam, mjeledi wa kwanza uk. wa 115.
[2] (Na Akakukuta fakiri Akakutajirisha?) Dhuhaa 93:8.

Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa mbora mbele ya vijana wa rika lake kwa tabia zake nzuri na kwa upekee kabisa kwa haya zake kubwa. Pia alijiepusha na mambo ya kipuuzi puuzi na alijipamba na staha isiyo na mpaka. Alikuwa akimvutia kila aliyefanya muamala naye, na jambo hili likampatia kuaminika kwa kiasi kikubwa nyoyoni mwa watu, hali iliyopelekea ikubalike kwake yeye kuitwa jina la ‘‘Mwaminifu’’.

Na sifa kama hizi hua zinamuelezea mwenye nazo ana nafasi gani katika jamii. Hivyo tunamuona Mtume rehema na amani ziwe juu yake, ujanani mwake, akiitwa katika vikao vya wakuu wa makabila wanaoheshimika katika umoja wa ‘Al-Fudhuuli’[1].

Na kwa kiasi kile kile cha kuoa akiwa na miaka ishirini na mitano, ya kupata fursa ya kunyanyua kiwango chake cha kiuchumi, pia alipata fursa ya kufichua sifa zake nyingine zilizo nzuri nzuri. Kwani Bi. Khadija ambaye ni mjane, tajiri, msafi na mwema akiwa katika muongo wa nne wa umri wake alimpatia Mtume rehema na amani ziwe juu yake kazi ya biashara ya kwenda Sham. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akaitekeleza kwa uerevu na utakatifu mkubwa. Jambo lililomuhakikishia Bi. Khadija kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake anastahiki kuitwa jina la Mwaminifu. Na licha ya tofauti kubwa ya kipato baina yao, Bi. Khadija alimfungulia Mtume rehema na amani ziwe juu yake suala la kuoana naye. Naye Mtume rehema na amani ziwe juu yake akalikubali suala hilo, licha ya tofauti kubwa ya kiumri baina yao. Kisha baada ya hapo akaendelea naye kama mkewe wa pekee kwa kipindi chote cha robo karne na hakuna kulichowatenganisha isipokuwa kifo. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliendelea kuonesha uaminifu wake kwa Bi. Khadija jambo lililopelekea, hapo baadae, baadhi ya wake zake wamuonee wivu.

Ndoa yao ilikuwa ni miongoni mwa ndoa bora zaidi na yenye matunda bora zaidi. Alimzalia watoto wakiume wawili nao ni Kassimu na Abdullah, nao wote walikufa wakiwa wadogo[2]. Na mabinti wanne wote walisilimu nao ni: Zainabu, Rukiya, Ummukulthumi na Fatuma. Na huyu wa mwisho ndio alikuja kuwa mke wa Ali bin Abii Twaalibi (Khalifa wa nne katika makhalifa

---

[1] Neno fudhuulu maana yake ni: kupatanisha ili kupata mambo mazuri. Na umoja huu wa Maka ulikuwa unalengo la kuwapatia nguvu wanyonge na kuwatetea waliodhulumiwa dhidi ya madhalimu, kuweka amani baina ya makabila na kuwazuia wale wanaovuruga amani wasiivuruge.

[2] Mtume rehema na amani ziwe juu yake, baada ya hapo akiwa Madina aliruzukiwa mtoto wa kiume ambaye ni Ibrahimu kwa Maryamu mkibtwi (mmisri) na huyu Ibrahimu alikufa kabla ya kufa kwa baba yake kwa miezi michache (Tazama Mahamoud Pasha Alfalakiyyu, kitabu kilichotangulia ukurasa wa 7).

waongofu). Na hao wawili waliomtangulia Fatuma kwa kufuatana waliolewa na Othman bin Afaan (Khalifa wa tatu katika makhalifa waongofu).

Ama Zainabu, kwa hakika aliolewa kabla ya Uislamu na mtoto wa ami yake Abu Al-Aaswi ambaye naye alisilimu hapo baadaye. Na Zainabu alifariki kabla ya kufariki kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwa miaka miwili akiacha binti yake aitwaye (Umamah) aliyeolewa na Ali baada ya kufariki Bi Fatuma.

Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alikuwa ni baba mpole na mume mwaminifu alidhihirisha mapenzi yanayobubujika kwa watoto na wajuu wake. Kwani alikuwa anatembea kilometa kadhaa kwa miguu ili kuwaona, kuwakumbatia na kuwabusu wakiwa sehemu za kunyonyeshwa. Alikuwa anawaachia wampande na kumning`inia mgongoni wakati wa swala kama alivyokuwa akikatisha hotuba yake ili kuwapokea na kuwaweka wakae karibu naye katika mimbari. Na mjadala wake na watu wawili wa kabila la Banii Tamiimi kuhusu mapenzi ya baba[1] ni maarufu katika vitabu vya historia ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Na baada ya kujihakikishia utajiri, Mtume rehema na amani ziwe juu yake, aliendelea kuishi maisha ya kawaida na zuhudi (Kujiepusha na anasa) katika kula. Na hakupata faida yoyote na utajiri huo zaidi ya kuongeza wigo wa kuwafurahisha wale wanaomzunguka. Alimlipia Ami yake deni. Na ili kuonesha namna anavyothamini wema aliotendewa na Ami yake huyo pale alipomlea utotoni, alimchukua na kumlea Ali mtoto mdogo wa Ami yake ambaye kisha alimuozesha Fatuma binti yake mdogo kabisa.

Tukio kuu kabisa lililotokea wakati wa baina ya kuoa kwake na kupewa kwake Utume, akiwa na umri wa miaka thelathini na mitano ni tukio la ukarabati wa Kaaba. Kwa ajili ya umuhimu wa jengo hili, ambalo lilikuwa ni kama jumba kuu la ibada la kitaifa kwa eneo lote la Ghuba ya Arabuni. Kila kabila la Kiarabu lilikuwa linalitukuza jumba hili licha ya tofauti zao za kiitikadi. Kwa ajili hii tunawaona Waarabu wote wakipupia wapate nafasi ya kujifaharisha kwa kushiriki katika kuijenga upya Kaaba. Kwa faida ya

[1] Al-Bukhaariyu Kitabu Al-Adabu mlango wa 18 – kumekuja utajo wa mijadala miwili katika suala hili: Wa kwanza ni ule wa baina yake na Al-Aqrau bin Haabis Attamiimiyyu. Pale alipomuona Mtume rehema na amani ziwe juu yake akimbusu mjukuu wake ambaye ni Hassan, hapo Al-Aqrau akasema: Kwa hakika mimi nina watoto kumi na sijambusu hata mmoja katu. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akamwangalia kisha akasema: ''Asiyehurumia hatohurumiwa''. Mjadala wa pili ni pale Mbedui mmoja alipoenda kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akasema: ''Mnawachumu watoto na sisi hatuwachumu'' Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: Je, kuna ninachoweza kukimiliki kwako wakati Allah Mtukufu ameshaing`oa rehema kutoka katika moyo wako.

kugawana kazi baina ya makabila hayo yaliweza kufikia matakwa ya wote. Hata hivyo makabila haya yanayopingana yalijikuta yakikabiliwa na kazi isiyoweza kugawanyika baina yao. Kazi yenyewe ni kurudia kuliweka jiwe jeusi sehemu yake. Lakini hakuna hata mtu mmoja aliyeridhia kusamehe haki yake ya kulinyanyua hilo jiwe. Na hakukuwa na mtu hata mmoja wa kuweza kuzuia kusiibuke ugomvi baina ya makabila hayo. Pamoja na hayo, na kabla ya kuanza kuelekea upande wa kunyanyuliana silaha, kulifanyika kikao ambacho hatimaye kiliamua kwamba wapate mwamuzi wa tatizo hilo na mwamuzi wenyewe awe mtu wa kwanza kuingia katika eneo tukufu la Kaaba kwa kupitia mlango wa ukoo wa Bani Shaibah. Uweza wa Mungu ulitaka mtu huyo awe Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. Na hao watu walipomuona akiingia walipiga kelele wakisema ‘‘mwaminifu – mwaminifu’’ na kweli Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuharibu dhana yao ya kusubiria uamuzi wa uadilifu kutoka kwake. Naye – kwa akili za haraka haraka, mwamko na uadilifu wa kuzaliwa – alitandika shuka yake juu ya ardhi na kulichukua jiwe jeusi kwa mkono wake na kuliweka katikati ya shuka kisha akawataka wakuu wote wa makabila, kila mmoja wao ashike ncha ya ile shuka na kuinyanyua kwa pamoja hadi katika usawa unaotakiwa. Na walipolifikisha lile jiwe katika sehemu yake, Muhammad rehema na amani ziwe juu yake akalichukua na kuliweka sehemu yake. Kukatawala amani na kuridhia kwa wale wote waliohudhuria tukio hilo na kuenea amani baina ya makabila.

Na katika umri huu, Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alikuwa ameshakamilika kimwili, kiakili na kitabia. Na ukamilifu huu aliendelea nao mpaka anafikia mwisho wa uhai wake. Kimo chake kilikuwa kirefu kidogo kuliko wastani wa urefu wa kawaida. Alikuwa na umbo lenye nguvu, kifua kipana na mabega mapana. Kichwa kikubwa, paji la uso pana, uso uliojaa utulivu, mdomo mpana, meno meupee yalioachana kidogo, ndevu nyingi, nywele nyeusi zilizojikusanya na kujikunja zinazoning`inia hadi chini ya masikio yake. Alikuwa na macho meusi na katika mboni kuna vijinyusi vyekundu, na ngozi nyeupe inayoelekea katika rangi ya waridi. Mwendo wake ulikuwa ni wa taratibu wenye haiba kana kwamba anateremka kutoka mlimani. Nguo zake ni za kawaida safi na kupangika vizuri. Zuhudi (kujiepusha na anasa) yake haina mfano, lakini yeye hakua akikataa chakula kizuri kama itatokea fursa ya chakula hicho bila kupanga. Mvumilivu wa kuvumilia maumivu na tabu bila ya kukusudia kujipatisha tabu. Si mwingi wa kuongea ongea lakini hata hivyo huko kutoongea ongea sana hakumpunguzii utamu wa maneno yake wala hisia zake za ucheshi na wema. Na alipokuwa raisi wa pekee

wa dola hakudanganyika kwa heri na starehe za dunia. Kwa hakika alijiepusha yeye na familia yake na kila aina za matumizi ya fujo vyovyote yalivyo tena kwa kupenda kwao wenyewe. Siku moja wakeze walimpinga wazi wazi pale alipokataa kukubali matakwa yao ya kupata vitu na kupenda mapambo ya maisha ya kidunia.[1] Na kile kichache kilichosalia baada ya kufariki kwake hakikurithishwa kwa warithi wake na badala yake kiligawiwa kwa mafukara. Kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa juu zaidi kwa namna ya kipekee kwa sifa maalum nayo ni ubora wake kijamii. Kwani yeye alipewa vipaji vya upole na utaratibu alivyodumu navyo hata pale alipokuwa kileleni katika utawala wake. Hamkaripii anayeongea naye vyovyote vile atakavyokuwa na wala haharakishi kumaliza mazungumzo yake. Na hakuwa wa kwanza kuondoa mkono wake kutoka katika mkono wa mtu anayepeana naye mikono. Pamoja na msimamo wake na uadilifu wake katika kusimamia uadilifu baina ya watu alikuwa msamehevu katika mambo yanayohusu haki zake binafsi. Anasi bin Maaliki mmoja wa watumishi wake anasema: ‘‘Kipindi chote cha miaka kumi alichomtumikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake hajapatapo kumwadhibu hata mara moja wala hajawahi kumuuliza kwa nini umefanya hiki au kwa nini hujafanya hiki’’. Kilichomfanya afanikiwe kuishi kwa amani na watu mpaka muda huo si kingine zaidi ya kwamba yeye alijua namna ya kujipatia upendo wa kila watu atakaoishi nao. Kwani yeye hakukaa na kuanzisha uadui na upinzani na watu aliokuwa akipendana nao. Sasa anakaribia muongo wa nne wa umri wake, na amekuwa anaelekea katika tukio tukufu litakaloipatia tabia yake mwelekeo mpya na hili tukio kwa haki kabisa linazingatiwa kuwa ndilo mabadiliko ya kweli katika mtiririko wa historia yake.

Dalili za kwanza za kupewa kwake Utume, kama zilivyokuja katika simulizi ya Bi. Aisha Allah amuwie radhi ni kuwa kila alichokuwa anakiona ndotoni kilikuwa kinatokea vilevile kwa uwazi kabisa kama anga la mapambazuko ya asubuhi katika siku ya pili yake. Na baada ya hayo akaanza kupenda kujitenga na kukaa mpweke akiwa peke yake. Akachagua sehemu ya kujitenga kwake iwe ni mlima Hiraa au mlima Annuur uliopo kaskazini ya Makka. Na huko ni mbali na wanajamii wa Makka ambao ni wapagani na mafisadi, pia huko ni mbali na shughuli za kidunia. Alikuwa akipenda kujitenga

[1] (Ewe Mtume! Waambie wake zako: ”Ikiwa mnapenda maisha ya (hii) dunia na uzuri wake (mimi si nayo, na mimi siwezi kukulazimisheni kukaa na mimi katika hali ya ufakiri; basi mkipenda nikuacheni), njooni, nitakupeni kitoka nyumba, (baadhi ya matumizi) na kukuacheni muwachano mzuri.” Na kama mnataka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na nyumba ya akhera, basi Mwenyezi Mungu Amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa.) Al-Ahzab 28 – 29. Uk 19

na kubaki peke yake na nafsi yake[1] katika pango linalotazama Kaaba na anga pana lililotawanyika nyuma yake kwa upeo wa macho.

Katika usiku mmoja, katikati ya ukimya mkubwa, ilikuwa ni siku ya 17 ya mwezi wa Ramadhani, kama asemavyo Ibnu Saad (ni Februari ya mwaka 610 kwa kalenda ya AD) Muhammad rehema na amani ziwe juu yake aliingia katika mawasiliano ya mwanzo kabisa baina yake na ulimwengu wa nje ya maumbile. Akapitia uzoefu wake wa kwanza kwa ufunuo wa kweli kweli. Kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake ametunukulia yeye mwenyewe mtiririko wa tukio hilo kwa mtindo wa majibizano baina yake na Jibrilu, na baina ya mfuasi na mlezi. Jibrilu alisema: Soma. Kwa mshangao, Muhammad akasema: mimi siwezi kusoma. Jibrilu akarejea na kauli yake: (Soma) baada ya kumbinya Muhammad mbinyo mkubwa. Muhammad akasema: Nisome nini?! Kwa hakika lilijirudia jambo hilo hilo na kumbinya tena kwa ukali zaidi ya mbinyo wa kwanza. Kama vile makusudio yake yalikuwa ni kumtanabahisha Muhammad na kumuandaa vizuri kwa ajili ya kupokea maana mpya ambao inahitaji umakini na kuvumilia mazito yatakayomtokea. Lakini swahiba wetu aliyebanwa bado anauliza kwa wasiwasi: Nisomeje? Na hapo hapo ndipo huyo Malaika anamsomea: *(Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Ameumba mwanadamu kwa pande la damu. Soma, na Mola wako ni Karimu sana. Ambaye Amemfundisha (Binadamu ilimu zote hizo) kwa wasita (msaada) wa kalamu; (zilizoandika vitabu, watu wakapata ilimu). Amemfundisha mwanadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui).* Alaq 1 – 5.

Haya Maneno Matukufu yakathibiti katika kumbukumbu zake na akawa akiyarejea rejea kila Jibrilu anapotoweka. Wakati Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alipotoka pango ili kurejea nyumbani kwake alisikia sauti ikimwita. Akanyanyua kichwa chake kuelekea mbinguni na kuhamaki anamuona malaika yuleyule amefunika anga na anasema: (Ewe Muhammad, wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mimi ni Jibrilu). Hakuweza kugeuza macho yake au kusogea mbele au kurejea nyuma. Hakuwa akiona nukta yeyote mbinguni ila anamuona Jibrilu yupo mbele yake. Tukio hilo likaendelea kwa muda fulani kisha akawa haoni chochote.

---

[1] Simulizi za Al-Bukhaariyyu haziainishi muda wa huku kujitenga isipokuwa zenyewe zimeweka wazi kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alikuwa katika kujitenga kwake akikaa miusiku mingi hadi kinapoisha chakula chake. Na kila kinapoisha anarudi kwa mkewe na kuchukua chakula kingine. Ama ibnu Is-haka anataja kuwa muda wa kujitenga kwake kwa kukatakata ulikuwa mwezi mmoja.

Huenda kitete alichokipata Muhammad rehema na amani ziwe juu yake kutokana na uzoefu huu mpya wa kusikia na kuona umemletea shaka kwa muda fulani juu ya uhakika wa sauti ya malaika. Au alikuwa na baadhi ya hofu huenda amepatwa na hali ya mapepo ambayo haina ubaya sana kama ule ubaya wa wachawi na makuhani. Kwa hiyo akawa anaogopea asije akawa mmoja wa watu hao. Na huenda ikawa si mbali sana na uhalisia kusema kwamba maumivu ya mwili yaliyotokana na mahojiano haya yanafanana na maumivu ya kifo. Na huenda Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alikuwa na taswira kwamba yeye ameshakufa kwa ukali wa tukio hili. Na kwa kitete hiki cha kiakili na kimwili hapo hapo Muhammad alirejea nyumbani kwake huku akitetemeka kwa homa na kuhisi baridi. Akamuomba mkewe amfunike mashuka maziko ili imwondoke ile hofu. Na pale alipomaliza kumsimulia Bi. Khadija kile kilichomtokea na kumdhihirihishia hofu zake na kitete chake. Bi. Khadija akafanya kila awezalo kumuondolea hofu na kumpa moyo kwa maneno matamu na maliwazo mazuri: ((Hapana, nakuapia kwa Allah, kamwe Allah hatokudhalilisha. Kwa hakika wewe utaunga udugu, utawasidia watu, utawapatia wasio na kitu, utatuliza mioyo ya wadhaifu na kuwasaidia watu dhidi ya majanga ya dunia)).

Na kwa kuwa Bi. Khadija hakuweza kumpa maelezo ya kina yenye uthibitisho juu ya tabia ya tukio hili. Bi. Khadija akamwendea mtu aliyebobea katika masuala ya ufunuo ili kumtaka ushauri wake. Na Bi. Khadija akaazimia ampeleke Muhammad rehema na amani ziwe juu yake kwa mtoto wa ami yake – Waraka ibnu Naufali – ambaye ni mzee sana na kipofu aliyeingia Ukristo baada ya kutumia muda mwingi wa maisha yake kusoma vitabu vya Kiebrania na elimu za vitabu vya dini za mbinguni zilizotangulia. Naye akawaambia wao (Bi. Khadija na Muhammad rehema na amani ziwe juu yake): ‘‘Huu ni ujumbe ulioteremshwa na Mwenyezi Mungu kwa Musa rehema na amani ziwe juu yake. Ee laiti niwe kijana mbichi, laiti niwe hai, pale watu wako watakapokutoa. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: ‘‘Je, wao watanitoa?’’ Akasema: Ndio, katu hajakujapo mtu akiwa na mfano wa hicho ulichokuja nacho isipokuwa alifanyiwa uadui. Na kama nitaiwahi japo siku yako moja tu, nitakunusuru kukunusuru kukubwa sana kabisa’’.

Lakini uhai wa Waraka haukudumu muda mrefu ijapokuwa haya maneno ya kutumainisha yalileta mwanga wa matumaini kwa hii nafsi yenye kitete, kwa huyu mwanadamu mwenye hamu ya kupata elimu na kutafiti kwa uwazi na yakini. Yaani hii ni akili ya kisayansi. Tutakujaona kuwa haya matumaini

hayakuwa ya nguvu wala yenye kudumu kwa muda mrefu. Kwani ilikuwa ni jambo la kawaida kwa Muhammad kuvuta taswira ya kuthibitisha elimu hiyo iliyoahidiwa na sauti ya Haki katika siku zifuatazo. Na daima alikuwa anarudi kujipatia somo la pili katika eneo lilelile alilopokelea somo la kwanza. Akawa anakaa mkao na eneo lake la kwanza katika jabali na kuzungusha macho yake kila upande na siku zikawa zinafuatiwa na siku nyingine, wiki zinafuatiwa na wiki nyinge, miezi inafuatiwa na miezi mingine mpaka mwaka ukaisha na kuanza wa pili.

Kama anavyosema Shaabiyyu kisha ukaingia mwaka wa tatu huku Mtume rehema na amani ziwe juu yake akiwa anasubiri kuja kwa malaika. Na kila mara anapokaribia kufikia ukingo wa kukata tama anaona na kusikia ((Ewe Muhammad wewe ni Mtume wa Allah na mimi ni Jibrilu)). Maneno haya yalikuwa yanatia utulivu wa aina fulani katika moyo wake. Hata hivyo ufunuo halisi uliendelea kusubiriwa kwa muda mrefu huku yeye akigubikwa na huzuni na kuhisi dhiki kwa mara nyingine. Baadhi ya watu wakasema: hilo halikuwa vingine zaidi ya kupatwa na uwendawazimu. Na baadaye wengine wakaona kuwa kiuhalisia ni kweli jambo hilo lilihusiana na kupewa ufunuo mtukufu wa mbinguni. Isipokuwa kile alichokidhihirisha Muhammad miongoni mwa udhaifu wa kutokuvumilia hali iliyompelekea kuonekana kana kwamba hastahiki kupata huu wito wa Mwenyezi Mungu. Zikateremka aya mbili ([1]) ([2]) ili zimuondoshee hofu hizi, hata hivyo aya hizi hazikumpa ile elimu anayoingojea.

Muhammad rehema na amani ziwe juu yake akauanza mwaka wake wa arobaini na nne. Alikuwa anakesha muda mwingi wa usiku akisubiri kauli hii ((nzito inayosuburiwa)). Bali kwa hakika alishazoea tangu alipokutana na ufunuo wa kwanza kujitenga katika mlima Hira katika kipindi kama hicho yaani mwezi wa Ramadhani. Hatimaye alipomaliza kujitenga kwake na kutaka kushuka kwa kupitia upande ule unaoelekea Makka akasikia sauti ikimuita. Akageuka kulia, kushoto na nyuma lakini hajaona kitu. Akanyanyua macho yake mbinguni na kumuona Yule malaika aliyemuona katika pango la Hira. Lakini cha mshangao wa kumuona huyo malaika na ukubwa kupindukia wa kiumbe huyo wa mbinguni kulimpiga bumbuwazi mpaka miguu yake ikakosa

---

[1] ((Kwa neema ya Mola wako wewe si mwendawazimu. (Makafiri wakimwambia Mtume – kwa ajili ya kumtukana tu – kuwa yeye ni mwendawazimu)). Qalam 68:2. ((Hakukuacha Mola wako wala hakukasirika (nawe Ewe Nabii Muhammad). Dhuhaa 93:3.

[2] ((Ewe uliyejifunika maguo! Simama usiku (kucha kufanya ibada); ila muda mdogo (tu hivi). Nusu yake au ipunguze kidogo. Au izidishe – na soma Quran vilivyo. Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito)). Muzzammil 73:1-5.

nguvu ya kumbeba. Akatetemeka kwa hofu (na huenda ikawa alitetemeka kutokana na baridi la mwezi wa Januari). Kisha akarudi haraka haraka kwa Khadija ili kumuomba ampe uangalifu wake ule uliotangulia. Hata hivyo yule mgeni wake mkarimu akamuwahi huko nyumbani huku akimbebea hukumu ambayo inampasa yeye atekeleze misheni (kazi) yake ya pili: *((Ewe uliyejifunika maguo. Simama uonye (viumbe).))* Muddathir 74:1-2. Tangu wakati huo kazi na nafasi ya Muhammad haikufungika katika kupokea mafundisho ya Mola wake tu, bali alipaswa pia kuwafikishia watu. Kwa hiyo kazi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ikaongezeka na kuwa Nabii mfikishaji.

Tumeshaona kuwa katika kipindi cha amri mbili hizi, ufunuo ulikuwa ni wenye kukatika, upo polepole na mchache. Lakini punde tu baada ya kupewa jukumu la kufikisha ujumbe, ufunuo ukawa unamshukia Mtume rehema na amani ziwe juu yake – sisemi kuwa eti Quran iliteremka kwa namna ya mtiririko wa mfuatano na kwa vipindi vya karibu karibu – isipokuwa kwa namna fulani ya muunganiko bila kukata kama ulivyokatika hapo kabla.

Mwaka 612 AD ndio nukta ya kuanzia ya ujumbe wa Uislamu. Na zikaja tarehe za HIJRIYA[1] na kukigawa kipindi cha Ujumbe kwa sehemu mbili takriban zilizokaribu sawa: miongoni mwao ni miaka kumi ya Makka sehemu alipozaliwa na miaka kumi na mitatu ya Madina sehemu alipokufa tarehe 12 au 13 ya Mfungo sita mwaka 11 HIJRIYA sawa na tarehe (7 au 8 Juni 632 AD) baada ya kufikia umri wa miaka 63 kamili kwa miaka ya mwezi mwandamo yaani mingi kidogo kwa miaka 61 ya miaka ya miezi ya kuzingatia jua.

Hapana shaka kuwa katika mambo mazuri kabisa ni kumfuatilia Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika kazi zake za bidii na ujumbe wake wa uongofu katika muda wote wa miaka ishirini ulioleta mapinduzi miongoni mwa

---

[1] Hijra (Kuhama) maana yake ni kukatisha mahusiano na kujiweka mbali kwa hiari. Hata kama sababu zake si za hiari. Ni jambo linalojulikana kuwa Muhammad akiwa anafikisha ujumbe – alilazimika aihame nchi yake siku moja kabla ya siku ya njama zilizolenga kummaliza. Akaenda kujituliza Madina, ambako alifika mwanzoni mwa mwezi wa sita (Tarehe 2 au 8 au 12 kwa mujibu wa tofauti za wanahistoria). Mwanaanga wa Kimisri, jina lake limeshatangulia kutajwa, kwa kutumia data mbalimbali ameainisha tarehe ya kufika kwake Madina kuwa ni tarehe 8 ya Mfungo sita inayoafikiana na 20 Septemba 622 AD. Ila inapaswa tusiondoe akilini mwetu kuwa kalenda ya Kiislamu ya HIJIRIYA ilianza katika mwaka wa miezi miandamo. Mwaka ambao ndani yake ndio kulitokea tukio la kuhama (Hijra) na sio siku ile ile aliyohama Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Yaani yeye alianza jambo hilo kwa miezi miwili na siku kadhaa. Yaani siku ya kwanza ya Muharram sawa na 15 au 16 Julai ya mwaka 622 AD. Na ilivyokuwa mwaka mrefu wa miezi miandamo una siku 355 tu, na jumla ya miaka 33 ya miezi miandamo takribani ni sawa na miaka 32 ya miezi ya kuzingatia jua. Hivyo basi inawezekana kugeuza miaka ya Hijiriya kwenda miaka ya AD au kufanya kinyume chake kwa kutumia moja ya kanuni mbili za hesabu zifuatazo: AD = HIJRIYA + 622 – HIJRIYA/32. Ya pili: HIJRIYA = AD – 32 622 /32.

mapinduzi makubwa ya kiustaarabu yaliyowahi kujulikana na mwanadamu. Lakini kwa kuwa lengo kuu la kitabu hiki ni utafiti wa kichambuzi juu ya jengo la Quran yenyewe. Kwa kutazama kuwa tumeshayapitia na kuyadurusu maisha ya Muhammad rehema na amani ziwe juu yake mpaka tukafikia nukta ya kukutana baina ya Mtume na ujumbe wake. Kwa sasa tunaweza kukipitia kwa utafiti kitabu alihotuachia.

Katika sura ifuatayo tutapitia: namna ya kukiunda kitabu hiki Kitakatifu, kukifuma, kukilinda na kinavyosambaa katika vipindi vya kihistoria.

## Sura ya pili
## Namna lilivyokusanywa andiko la Uteremsho wa Hekima

Ikiwa maandiko asilia ya Quran Takatifu yaliyopo mikononi mwetu leo hii yanaafikiana kikamilifu na yale ambayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliwasomea waandishi wa ufunuo. Kwa hakika umbo lake la nje limetokezewa na mabadiliko makubwa. Kwani wakati huo hakukuwa na kitu kinachoitwa kitabu au mjeledi. Quran iliteremka vipande vipande vilivyoachanishwa na urefu wake unatofautiana baina ya sura moja kamili mpaka aya moja, na wakati mwingine sehemu ya aya. Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa anakisoma kila kipande kilichomshukia na kuwafundisha wanaoisikiliza ili nao wawafikishie wale wasioisikia mubashara kutoka kinywani mwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Watu wote walikuwa wanasubiria ufunuo kwa hamu kubwa na kutamani kuupokea punde tu unapoteremka.

Ingawa andiko lililoteremka halikufungika tu kuwa ni (kisomwa) yaani mkusanyiko wa aya zisomwazo na kuhifadhiwa vifuani, bali pia zilikuwa ni (kitabu) yaani kilichoandikwa kwa wino. Taswira mbili hizi zinasaidiana na kila moja inamsahihisha mwenziwe. Na kwa ajili hii Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa kila unapomjia ufunuo na kuwasomea wale waliokuwepo papo hapo anawasomea waandika ufunuo wauandike katika kitu chochote walichokuwa nacho mikononi mwao kwa mfano karatasi au ubao au kipande cha ngozi au juu ya mawe au vipande vya mifupa ya mabega… nk. Wanazuoni wa kutegemewa wanataja kuwa idadi ya waandika ufunuo ilifikia waandishi ishirini na tisa. Katika wao, waandishi mashuhuri ni makhalifa waongofu watano wa mwanzo. Lakini Muawiya na Zaidu bin Thaabiti walikuwa wanajihusisha zaidi na jukumu la uandishi wa Quran. Jukumu ambalo halikuwa katika hali ya urasmi ila huko Madina. Hata hivyo Waislamu wa Makka hawajajiweka nyuma na uandishi wa aya za Quran katika miswada yao binafsi kwa ajili ya matumizi yao. Kwa hakika imeonekana tangu wakati wa mwanzo kuwa vifungu vya aya havikubakia kuwa vimejitenga vyenyewe kwa wenyewe wala kufuatana kwa mujibu wa kuteremka ufunuo. Baadhi ya vifungu vilikuwa vinazidi vikiwa vimejitenga na vifungu vingine. Na kidogo kidogo vilikuwa vinaunda sura inayojitegemea baada ya kuunganishwa na aya nyingine zilizoteremka baada yake. Na kwa hakika baadhi ya aya zilikuwa zikiwekwa hapa na nyingine zikiingizwa pamoja na nyingine pale kwa mujibu wa maagizo

ya wazi wazi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Maagizo ambayo yeye naye alikuwa anayapata kutoka kwa Roho Mtakatifu (Jibrilu). Ili kutoa fursa kwa sura za Quran ziweze kuundwa na kukamilika kidogo kidogo ilikuwa inapaswa kungoja hadi ufunuo wote ukamilike na kisha kuitoa Quran ikiwa na umbo moja lililokamilika.

Hali hii haikuzuia waumini wasiwe na maarifa kwa njia ya mdomo ya kujua sehemu ya kila aya mpya katika kila sura kwa kuainisha kabisa, katika kila hatua miongoni mwa hatua za kuteremka ufunuo. Katika zama za uhai wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kulikuwa na mamia ya maswahaba wanaoitwa kwa jina la (mahafidhi wa Quaran) waliobobea katika kuisoma na kuihifadhi Quran kwa moyo. Na kuijua kila sura ikiwa katika umbo lake la muda au la mwisho. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akitaja kuwa katika mwezi wa Ramadhani wa kila mwaka alikuwa anaipitia Quran upitiaji wa jumla na kuzisoma aya zote zilizofunuliwa mbele ya Jibrilu. Na kuwa yeye, katika mwaka wa mwisho aliipitia Quran akiwa na Jibrilu mara mbili; jambo liliomfanya Mtume rehema na amani ziwe juu yake abashiri kukaribia kwa mwisho wake.

Na haukupita hata mwaka mmoja tangu kufariki kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake ila ikaonekana kuna haja na ulazima wa kukusanya nyaraka za Quran katika mkusanyiko ulioandikwa, mwepesi, ambapo aya za kila sura zitakuwa zinafuatana kama ilivyothibiti kwa mahafidhi wa Kiislamu. Omar bin Alkhatwabi alitoa wazo kwa khalifa wa kwanza mara baada ya vita vya Alyamaamati vilipelekea kuuwawa kwa mamia ya waislamu miongoni mwao wakiwa ((Mahafidhi wa Quran Sabini)).

Omar alikuwa akilenga, sio tu kuyalinda maandishi ya Quran na kuyaweka pahala salama na kuepukana na hatari, bali pia kulikiri umbo la mwisho la kitabu hiki kitakatifu na kulithibitisha kwa kupitia njia ya mahafidhi wake waliobakia hai. Na kutegemewa na maswahaba waliohifadhi. Na Abuu Bakar alimpatia jukumu hili Bw. Zaidu bin Thaabiti na kumwambia: ((Wewe ni mtu mwerevu na hatukutuhumu. Ulikuwa ukiandika ufunuo wakati wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Sasa simamia zoezi la kuikusanya Quran))[1] Zaidu mwenyewe alihudhuria usomaji wa mwisho wa kuisoma Quran uliofanywa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Kisha akajiwekea

[1] Baada ya Leblois kueleza simulizi hizi, alioongeza kwa kusema: ''Ni nani yule ambaye hakutamani, lau mmoja wa wanafunzi wa Yesu alioishi nao katika zama moja ndiye angefanya zoezi la kuandika mafundisho ya Yesu mara tu baada ya kuondoka kwa Yesu)). Tazama Al-Quran na Taurati ya Kiebrania – uk. 47, mjeledi wa tano.

kanuni ya kazi, nayo ni kuwa hatochukua mswada wowote ule ambao hauna ushahidi wa watu wawili wanaoshuhudia kuwa mswada huo umeandikwa kutokana na kusomewa na Mtume mwenyewe rehema na amani ziwe juu yake na si kutokana na kumbukumbu za kichwani. Na kuthibitishwa kuwa nao ni sehemu ya ufunuo ulio katika umbo lake la mwisho. Na baada ya kuikusanya Quran kwa kuzingatia tahadhari zote hizo. Zaidu aliikabidhi kwa Abuu Bakri ambaye naye aliihifadhi vizuri kwa muda wote wa ukhalifa wake. Na kabla ya kufa kwake aliukabidhi kwa Omar. Kisha naye Omari aliikabidhi kwa binti yake Bi. Hafsa mama wa waumini nyakati za mwisho za uhai wake. Huu msahafu rasmi wa kwanza una sifa za kipekee (msaahafu ambao tunaweza kuufananisha na faili linalokusanya kurasa zilizopangwa na bila ya kuwa na jalada) za kuwa wenyewe ni mkamilifu kabisa na unapatana kikamilifu na ufunuo ulioteremshwa.

Na msahafu huo unatofautiana na kopi nyingine za Quran zilizokamilika au zisizokamilika zilizokuwa kwa watu wengine. Kwa kuwa wenyewe uliondolewa na kuepushwa na kila kile ambacho hakikuwemo katika andiko asilia kulingana na wasilisho la mwisho. Pia ulikuwa hauna majina ya sura. Lakini licha ya kima kikubwa cha msahafu huo, na licha ya kile kinachoustahiki na kukipata miongoni mwa uangalizi uliotolewa katika kuukusanya, na kusalia kuwa umehifadhiwa kwa uangalizi mkubwa mno kwa Makhalifa wawili wa mwanzo. Licha ya hayo yote, hakika msahafu huo haukupata nafasi ya kusambazwa ila katika ukhalifa wa Othmani baada ya vita vya Armenia na Azebaijani

Wakati majeshi ya waislamu yaliyotoka Siria na Iraqi yalipokusanyika, yaliona baadhi ya kuhitilafiana katika visomo (Qiraati). Kwani wasiria walikuwa wanafuata usomaji wa ‘‘UBAYI’’ na wairaqi wanafuata usomaji wa ‘‘IBNU MASUUD’’. Wakaambiana wao kwa wao ‘’Usomaji wetu ni bora kuliko usomaji wenu’’. Hudhaifatu ibnu Al-Yamani kwa masikitiko akakimbilia kwa Othmani na kumtaka akomeshe mkanganyiko huu unaoweza kupelekea kutokea kama kile kilichowatokea Wayahudi na Wakristo cha kufarakana juu ya kitabu chao. Othmani akaunda tume ya waandishi wanne wa kiswahaba akiwemo na Zaid bin Thaabiti mwenyewe katika Maanswari – na Abdallah bin Zubeir, Said bin Al-Aaswi na Abdulrahmaani bin Al-Haarithi bin Haashim

katika Muhajirina. Kisha akawaamuru wakopi msahafu wa Hafswa kwa idadi ya kopi zinazolingana na idadi ya majimbo[1] makuu katika dola ya Kiislamu.

Na kwa kuisha kazi hii inayoafikiana kikamilifu na andiko asilia, msahafu wa Hafswa ukarejeshwa kwake. Na zile kopi nyingine zikawekewa magamba na kutawanywa katika hayo majimbo. Na hizo kopi zikazingatiwa kuwa ndio viigizo visivyo na mbadala na kubatilishwa kila kopi inayotofautiana na misahafu hiyo sawa sawa iwe kwa karibu au kwa mbali.

Baadhi ya Mashia walidhani kuwa eti Othmani amebadilisha andiko la Quran au ya kuwa yeye ameondoa baadhi ya maandiko yanayohusiana na Ali bin Abii Twaalibi. Lau hilo lingekuwa ni sahihi basi wale waliohifadhi Quran, tena walikuwa wengi sana wakati huo wa kusambazwa kwa misahafu ya Othamani, wangemrejea Othmani na kumuhoji juu na kuufananisha na kile wanachokiifadhi katika vifua vyao. Ila hakika mambo yalivyyo, hata Ibnu Masuudi mwenyewe ameukubali usahihi wa msahafu wa Othmani licha ya kwamba yeye hakuridhika na siasa ya Othmani kwa sababu zake nyingi. Na kwa kuangalia mapenzi makubwa ya waislamu ya mwanzo kwa dini yao – kwa uhalisia wao ndio walikuwa na hamasa zaidi na maandiko ya Mwenyezi Mungu kuliko makhalifa wao – haiwezekani kwetu sisi kueleza kuwa sababu ya wao ya kuukubali msahafu wa Othmani bila ubishi wala upinzani, inarejea katika utii wao usio na uoni (wa kibubusa) kwa upande wao. Kwa hakika ((Noldeke)) amekiri kuwa hali hiyo ni ushahidi wenye nguvu kuwa andiko la Quran ((lipo katika namna bora ya ukamilifu na kuafikiana kwa hali ya juu)).

Vyovyote itakavyokuwa, kwa hakika msahafu huu ndio wa pekee unaozunguka katika ulimwengu wa Kiislamu – likiwemo kundi la Mashia – tangu muda wa kipindi cha karne kumi na tatu. Hapa tunataja maoni ya kundi la Shia Imaamiya (kundi muhimu katika Mashia) kama ilivyokuja katika kitabu cha Abuu Jaafari Al-Ummu ((Hakika itikadi yetu juu ya jumla ya Quran ambayo Allah Mtukufu amemfunulia nabii wake Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, ni ile iliyomo kati ya majalada mawili ya Quran iliyopo kwa watu na si zaidi ya hiyo. Na idadi ya sura zinazotambulika na waislamu ni sura 114. Ama kwetu sisi, sura mbili nazo ni Adh-Dhuhaa na Alam-Nashrah zinaunda sura moja. Na kadhalika sura mbili za Al-Fyl na Quraysh. Vilevile sura mbili za Al-Anfal na At-Tawba. Ama yule anayeinasibisha kwetu itikadi ya

[1] Wapokezi wengi wanakubaliana kuwa, zilikuwa ni kopi tano zilizoandikwa kwa mkono (ukitoa ile kopi ya Othmani mwenyewe) zikapelekwa Makka, Madina, Basra, Kuufa na Damaskasi. Na Haatimu Al-Sajastaaniyu anataja kopi mbili zaidi za Yemeni na Baharein (Kitaabu Almaswaahifu cha ibnu Abuu Daudi uk 74).

kwamba katika Quran kuna mengi zaidi ya haya, huyo ni muongo)). (Hii ni tofauti ya umbo la nje tu na haipo isipokuwa kimtazamo tu; kwa sababu kopi zao hazitofautiani na kopi za Wasunni kwa chochote) [1]

Kutokana na hayo (Leblois) ametia mkazo kuwa: (Kwa hakika Quran ndio kitabu pekee kitakatifu kisicho na mabadiliko yanayotajika).

Na (William Muir) alikuwa ameshayatangaza hayo kabla yake pale aliposema: (Kwa hakika Msahafu huu alioukusanya Othmani umesambaa kwa njia ya kunukuliwa na wengi mkono kwa mkono mpaka ukatufikia bila ya kupotoshwa kwa njia yoyote ile. Kwa hakika umetunzwa kwa uangalifu mkubwa kiasi ambacho hakijatokewa na badiliko lolole linalotajika. Bali tunaweza kusema kuwa Quran haijawahi kutokezewa na kubadilishwa hata kidogo katika kopi zake zote zisizo na idadi, zinazozunguka katika miji mingi ya Kiislamu… haijawahi kuwepo isipokuwa Quran moja tu katika makundi yote ya Kiislamu yanayopingana. Na haya matumizi ya pamoja ya andiko hilo hilo linalokubaliwa na wote mpaka leo inazingatiwa kuwa ndio hoja kubwa na ushuhuda wa usahihi wa andiko lililotermshwa na tulilonalo. Na msahafu huo warejea kwa khalifa aliyepata majanga ambaye ni Othman aliyekufa kwa kuuawa).

Na hukumu hii ya kihistoria inayojipambanua kwa kuwa safi iliyoepukana na upendeleo haina mfano wake inahitaji kusahihishwa katika nukta mbili; kwa kuwa mambo yalivyo, andiko la Quran linarejeshwa kwa Othmani, wakati huyo Othmani hajafanya chochote zaidi ya kuusambaza mswada uliokusanywa zama za Abuu Bakri na ambao haukuwa vingine zaidi ya kuwa ni maandiko kamili kwa mujibu wa uwasilishaji wa mwisho wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake tena kwa kusomewa na Mtume mwenyewe rehema na amani ziwe juu yake. Pia hiyo hukumu inajumuisha ziada ya kuthibitisha kwamba kopi zinazonguka hazina tofauti yoyote ya usomaji. Hali sisi tunajua kinyume na maelezo hayo. Kwa hakika herufi zenye irabu ndefu siku zote huandikwa katika umbo la kila neno, wakati ambapo herufi zenye irabu fupi na za kati na kati huwa haziandikwi kabisa. Kama ilivyo kwa kundi

[1] Ama (sura ya An-Nuurayni) iliyopachikwa na ambayo imechapishwa na (Jaaridiin Dii Saaty) chini ya kichwa cha habari: (Sura isiyojulikana katika Quran). Kwa hakika mwanazuoni nguli – Miirzaa Skandar Kaadhim – kwamba sura hiyo inayodaiwa haina athari yake katika msahafu wa Kishia. Na haijatokea kutajwa katika vitabu maalum vya Kishia vya majadiliano yao ya kimapokeo. Bali hata jina la sura hiyo (An-Nuurayni) na ambalo linamwashiria Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na Ali, halikudhidhiri kwa mara ya kwanza kwa Mashia isipokuwa mnamo karne ya saba Hijiriya kwa mujibu wa yale yaliyokuja kwa At-Twuusiyu. Na hiyo sura haivuki na kuwa vingine zaidi ya mrundikano dhaifu wa vifungu na maneno yaliyoibwa kutoka katika Quran. Na haya yanapingana sana na uzuri wa mtindo na muundo wa Quran pamoja na mshikamano wake.

kubwa la herufi za Kiarabu hazitofautiani zenyewe kwa zenyewe kimaumbo isipokuwa kwa baadhi ya maumbo ya nukta, kwa mfano Al-Yaau, An-Nuun, Al-Baau na At-Taau.. na hizi nukta hazikuwa zikitumika katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, wala katika zama za makhalifa waongofu watatu wa baada yake. Na kwa kiasi kikubwa utamkaji ulikuwa haudhihiriki ila kwa mwongozo wa njia ya mdomo. Hata hivyo, hadithi zinatubainishia kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, hakufuata utamkaji wa namna moja wakati akiwafundisha waislamu Quran. Na haikuwa kwa nadra kwa neno (au mzizi wake) moja kupewa zaidi ya usomaji mmoja, na visomo vyote hivyo ni sahihi na vina maana yake, kwa mfano: (Maliki) huenda likasomwa (Maaliki) au (Malku) kadhalika neno (Fatabayyanuu) linaweza likasomwa (Fatathabbatuu) kwa mujibu wa visomo mbalimbali vilivyokuja katika hadithi. Kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Kwa hakika Quran hii imeshuka katika herufi saba, basi isomeni kwa kadiri itakavyokuwa wepesi katika herufi hizo). Na Al-Bukhariyyu anapokea kuwa Omar alimkaripia Hishamu bin Hakiim bin Hizaam kwa sababu ya kusoma kwake Suratul Furqaan, na At-Twabari anataja kuwa Ubayyu bin Kaabi alishtushwa na usomaji wa suratul An-Nahli. Na walipoenda kuhukumiana kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, alivikubali visomo vyote viwili. Kwa mtazamo wetu ni kwamba, kusambazwa Quran chini ya uangalizi wa Othmani kulikuwa na malengo mawili nayo ni:

La kwanza: kuzipa sifa ya kisheria namna mbalimbali za usomaji – zilizokuwa zimeingia katika wigo wa andiko lililoandikwa na zenye uasilia kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwa makubaliano ya waislamu wote – na kuzilinda namna hizo za usomaji. Na katika hilo kuna kuzuia kusitokee kugombana baina ya waislamu juu ya namna hizo za usomaji.

La pili: Kuondoa yale yasiyopatana moja kwa moja na andiko asilia la Quran. Ili kuwalinda waislamu wasitumbukie katika mpasuko hatari wa wao kwa wao. Na kulilinda andiko la Quran na upotoshaji wa aina yeyote ule unaotokana na kuingiza baadhi ya ibara zilizotofauti kwa aina fulani. Au ufafanuzi wowote uliongezwa na watu katika misahafu yao kwa nia njema.

Hiyo haina maana kuwa chapa ya Othmani – au msahafu asilia wa Othmani – unajumuisha visomo vyote ambavyo huenda Mtume rehema na amani ziwe juu yake amevifundisha kwa watu kwa jina la herufi saba. Kwa kuwa chapa hiyo hata kama kwa uhalisia imejumuisha visomo vilivyokubaliwa kuwa vilikuwepo katika andiko asilia kwa umbo lake la mwisho. Kwa hakika

chapa hiyo imeviacha visomo vyote vilivyokuja kwa njia ya mtu mmoja mmoja, ambavyo havikuwa na vidhitbiti vinavyohitajika. Kwa hakika msingi huu, tangu mwanzoni mwake ulikubaliwa baina ya maoni ya maelfu ya maswahaba waliokuwepo na kuuridhia kwa moyo mkunjufu. Tunaongeza kwamba, huku kuviondoa hivyo visomo katika andiko lililoandikwa hayakuwa malengo yake au matokeo yake kuvifuta hivyo visomo kwa njia ya simulizi za mdomo. Lakini kwa hakika mambo yalivyo ni kuwa uliacha mlango wazi kwa kila mtu anayehakikisha kuwa amemsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akisoma kwa kisomo fulani alichokianisha na asome kwa kisomo chake hicho maalum kwa uhuru kabisa, tena chini ya jukumu lake bila ya kuwalazimisha jamaa ya waislamu wafuate kile anachosisitiza kuwa amekisikia. Na hili ndilo lilotiliwa mkazo na Othmani mweyewe pale aliposema: ama Quran sikuzuieni isipokuwa mimi nakuhofieni na kufarakiana. Mnaweza kuisoma kwa herufi mnayoiona ni nyepesi kwenu. Wanazuoni wa dini katika kila zama wameendelea kutilia umuhimu katika kuvisoma hivi visomo ya mtu mmoja mmoja. Na hivyo visomo vinaendelea mpaka leo kuwa na vazi la utakatifu na vinatumika katika madrasa za Ahlu Sunna – sio kwamba hivyo visomo ni andiko la Quran – lakini kama hadithi zilizopokelewa na mtu mmoja. Na sababu iliyopelekea kuachwa kwa visomo hivyo katika andiko sahihi wakati wa kukusanya Quran ni kwamba vyenyewe havikuwa na kigezo muhimu cha kutosha cha kuthibitisha usahihi wake. Kigezo chenyewe ni uthibitisho wa kuwa andiko katika umbo lake lililoandikwa lina kigezo cha kupitiwa kikamilifu na kuthibitishwa vilivyo juu ya usahihi wake na Mtume mwenyewe rehema na amani ziwe juu yake au wale wanaomuwakilisha. Na zaidi ni kwamba, visomo hivyi visivyo rasmi havifungamani na sura zote za Quran, na hata havifungamani na hata sura moja kamili.

Kwa hivyo kile Maswahaba walichokitilia umuhimu katika kuthibitisha usahihi wa andiko la Quran ni kupatana herufi kwa herufi kwa kila kifungu katika kisomo husika na kile kilichoteremka na kuandikwa kwa agizo la Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Kisha baadaye kikasomwa mbele yake na kupewa uthibitisho wake wa mwisho kabla ya kufa kwake. Na uhalisia huu usio na upendeleo kabisa ni kitu kitakachobakia na kuendelea kwa miaka yote kuwa ni sifa kwao na sio dosari dhidi yao.

Na kama ikiwa kuteketezwa [1] kwa miswada ya mtu mmoja mmoja kunaonesha aina fulani ya moyo mgumu hasa katika wakati ambao hukajadhihiri upotoshaji wowote ule. Kwa hakika jambo hili linajulisha kuwa Othmani alikuwa anaona mbali na ni mtu makini katika kutambua uhakika wa mambo.

Fadhila za Waislamu wa leo hii za kufaidi na kufurahia hali ya kuwa na kitabu kimoja kilichotulizana zinarejea kwa kazi hii adhimu iliyofanywa na Othmani. Na kile kilichowekwa katika Msahafu wa Othmani miongoni mwa alama za nje, na kuwepo kwa baadhi ya herufi za nyongeza, au maneno yaliyoambatanashwa, au uandishi wa kale ambao unahusika na uandishi wa misahafu peke yake katika nakala zote za Quran za leo hii, sawa sawa zile zilizochapwa au zile za miswada. Vitu hivyo vinazingatiwa kuwa ni ushahidi wa upeo wa juu wa uaminifu uliopo katia unukuuji na usambaaji wa jengo la Quran toka kizazi hadi kizazi mpaka ukatufikia sisi ukiwa na ukamilifu huu usio na mfano. Na hakika andiko la Quran ni lenye kubakia kama lilivyo daima dumu likitoa changamoto kwa zama mbalimbali.

[1] Kiuhalisia, Othmani hakufanya mchakato huu kwa matashi yake bila ya kuwashauri watu. Kwa hakika Ali bin Abii Twaalibi, Allah amuwie radhi amekiri katika moja ya hotuba zake ya kuwa mchakato huu haukufanyika ila kwa makubaliano ya Maswahaba wote waliokuwepo. Na kwa hakika, lau kama Othmani asingefanya mchakato huu, basi yeye Ali angeufanya mwenyewe. (Ibnu Abii Daudi uk 12 – 22).

## Sura ya Tatu
## Namna msingi mkuu wa Quran ulivyofikishwa ulimwenguni

Kwa ujumla dunia yote inautambua msingi mkuu wa Quran ambao tunauita Uislamu. Na mara nyingi utambuzi huo unafupika katika kutambua sifa za nje nje tu. Na husemwa kuwa: Uislmau ni marekebisho ya kidini, kijamii na kitabia. Urekebishaji ambao, punde tu ulipodhihiri katika pwani ya bahari Nyekundu mnamo karne ya saba AD, ukawa unapiga hatua za ushindi kuelekea upande wa kaskazini, kusini, mashariki na magharibi. Mpaka ndani ya muda mchache kiuwiano ukaenea katika nusu ya dunia iliyokuwa ikitambulika wakati huo.

Tukio hili adhimu la kihistoria lisilo na mfano kwa zama zote zilizopita. Kwa hakika limechochea wanadamu wote kulitilia umuhimu. Kama lilivyochochea udadisi wa wanahistoria wa mambo ya kitabia na kidini. Wakajaribu kupata mfano wake katika yaliyopita bila kufanikiwa kuupata. Wakati mwingine walililinganisha na utekaji miji wa Aleksizanda Macedonian. Kwani ushindi wake nao ulikuwa wa haraka na kwa maeneo makubwa. Lakini utekaji huo haukuleta mabadiliko yoyote katika fikra za watu wala desturi zao. Kwa hiyo haukupita muda mrefu athari za utekaji huo wa Aleksizanda zikatoweka mwanzoni tu mwa ujio wa Uislamu. Na matendo ya Aleksizanda Mkuu hayakuvuka sekta ya ujenzi wa miundo mbinu kwa kuanzisha miji mikubwa katika maeneo ya Mashariki, miji iliyokuwa na uchumi mzuri kwa muda mrefu. Ama makundi ya raia na wakulima yaliendelea kudumisha tamaduni zao kwa upande wa lugha, tabia, mfumo wa kisiasa na kiuchumi. Na hata hiyo miji haikubadilishwa fikra na ada na kuwa za kigiriki isipokuwa kwa wachache miongoni mwa wafanyabiashara mabepari. Ama wakoloni wenyewe wa Kigiriki, baadaye nao walikuwa chini ya watekaji wengine. Na hiyo miji yao ilibomolewa kidogokidogo wakati wa utawala wa Warumi. Ama kwa upande wa kifikra, kwa hakika huyo Aleksizanda hakuchukua pamoja naye fikra za Kigiriki. Lakini yeye bila masharti wala kizuizi, alichukua fikra zilizokuwa zikitawala katika miji iliyoshindwa kwa wakati huo na kuingia katika itikadi zake. Na washirika wake hawakuwa wazuri zaidi yake, kwani nao hawakubadilisha chochote kabisa kabisa.

Na wakati wa utawala wa Wayunani na Warumi zilipatikana fikra za kifalsafa na kidini – nazo ni za madhehebu ya Kimashariki kabisa kabisa – hii ni fursa nzuri ya kusambaa huko ulaya kwa kupitia njia ya Wayunani (Wagiriki)

tena kwa jina la Uflatoni mpya au Ukristo. Kwa ajili hiyo ni haki kwetu tukisema kwamba, kwa hakika utekaji wa Kimashariki ndio ulioshinda.

Kisha ukaja Uislamu, na kila kitu kikabadilika baina ya mchana na usiku. Nao haujafungika tu na upande wa kisiasa na kiuchumi pekee. Kwa hakika ulipenya ndani ya nafsi za watu hao: kwa hiyo lugha, fikra, kanuni, matumaini, ada, taswira juu ya ulimwengu na fikra juu ya Allah. Yote hayo yametokezewa na mabadiliko makubwa ya msingi tena kwa haraka.

Mabadiliko hayo hayakuishia kwa zile nafsi zilizoamini tu, bali daima yalikuwa yana mwelekeo wa kuenea na kujipatia wafuasi wapya, kila pale ambapo Uislamu unapopata fursa ya kudhihiri kwa wepesi na utakatifu wake.

Lakini ukweli huu unapingana na rai iliyoenea mno na kusemwa sana huko Umagharibini, nayo ni kwamba eti Uislamu haukuenea ila kwa ncha ya upanga. Wakati ambapo, taathira inayotolewa na Uislamu katika nafsi za watu, wakati wa sasa, ni ushahidi mzuri wa kwamba Uislamu una nguvu ya dhati na upatano wa kipekee pamoja na maumbile ya wanadamu na uhakika wa mambo.

Kwa hakika kilichotokea katika miaka kumi ya kwanza ya wito wa Uislamu, ni kuwa nguvu zinazopinga Uislamu zilisimama kidete kumwaga chuki zake na kutumia mabavu yake yote ili kuukandamiza huo wito mchanga na kuwaadhibu wafuasi wake. Lakini wakati huo huo uwasilishaji mdogo tu wa misingi ya Uislamu ulikuwa kila siku ukiwavutia Waislamu wapya licha ya vikwazo vyote hivyo. Na miaka hii kumi inashuhudia upeo wa ushujuaa na uvumilivu vilivyokuwa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na Waislamu. Wote, walikuwa wanavumilia dharau na matusi ya watu wao dhidi yao. Zaidi ya hapo walivumilia kutengwa na kuwekewa vikwazo vilivyoambatana na matumizi mabaya mno ya kuadhibu na kutesa. Jambo lililowalazimisha mamia ya Waislamu wakiwepo miongoni mwao watukufu wa Kiqureyshi kutafuta sehemu salama ya kukimbilia iliyokaribu na mfalme wa Uhabeshi (Ethiopia).

Lakini mfano wa kuchukuliwa katika ukweli huu unaojulisha athari au kumbukumbu ya ajabu kwa wito huu wa amani umepigwa kwetu sisi na wakazi wa Yathribu (Madina). Kabla ya kuuona uso wa Mtume Mkarimu rehema na amani ziwe juu yake, na kabla ya kusikia sauti ya wito wake. Na kwa kusikia tu uteremsho wa Quran kupitia ndimi za mahujaji wao, Waarabu wa Madina waliupokea Uislamu na wakaipokea Quran kwa mapenzi makubwa hadi ikafikia kuwa hakuna ukoo hata mmoja uliobaki isipokuwa ulikuwa miongoni mwa

watu wake kuna idadi fulani ya waumini. Na zaidi ya hayo, hakika moto wa uadui na migogoro uliokuwa ukiendelea kuwaka miongoni mwao kwa takriban robo karne, ulizimika ghafla kwa mpulizo wa Mungu, na wakawa ndugu kwa neema za Allah. Na ibada za Kiislamu zilizokuwa hazitekelezwi kule Makka kwa sababu ya kukandamizwa – zikawa zinatekelezwa kwa jamaa (makundi) tena mbele ya macho na masikio ya watu wote huko Madina. Na katikati ya hali hii ya ukarimu, muhajiriina (wahamiaji) wote walipokelewa vizuri. Na hivyo ni baada ya kuacha nyumba na mali zao pamoja na kupewa maudhi kwa maudhi makali huko Makka.

Mpaka wakati huo, kwa uchache kila kitu kilikuwa kinapita kwa amani kwa upande wa Waislamu. Na hakukuwa na kitu kinachoonesha kwamba kuna uwezekano wa Waislamu kukimbilia katika matumizi ya nguvu. Na hivyo ni baada ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa na utulivu na kuamini kuwa wafuasi wake wamefika sehemu ya salama. Ikafikia upeo akaitakidi kwamba kinachotakiwa kwake ni kubakia Makka na kuendelea na wito wake. Lakini alipokea amri ya Allah ya kumtaka ahame katika kipindi ambacho njama na mikakati na njama za kumuua zilianza kufanyika. Baada ya kunusurika na hatari hii kwa njia za kimiujiza. Je, hakutakiwa kufikiria namna ya kuwalipizia kisasi maadui zake? Sivyo hivyo. Na kama tukifuatilia harakati zake baada kuhama tunazikuta kwamba zinamwelekeza katika matendo mazuri ya amani na ya kujenga: miongoni mwake ujenzi wa msikiti wake, na kuipangilia vizuri jamii kwa ndani na kiamani. Na kutekeleza faradhi ya funga na kuweka mfumo wa adhana. Na kila kitu kilikuwa kinaonesha kuwa Waislamu wameipa mgongo Makka kabisa kabisa. Mpaka katika suala la kibla cha swala. Hadi ilipofika nusu ya mwaka wa pili Hijiriya, pale walipoanza kuivamia misafara ya Maqurayshi ikiwa ni utangulizi wa kupambana nao..

**Haya mabadiliko ya ghafla yametokea wapi?**

Haiwezekani kueleza kuwa mabadiliko hayo yanatokana na nafsi ya Mtume mwenyewe rehema na amani ziwe juu yake. Mustashiriquuna (Wamagharibi wasomi wa mambo ya kimashariki) wamekubaliana kuwa michakato ya kivita si katika tabia zake. Bali kwa hakika kuwasamehe kwake washirikina mara nyingi kulimletea lawama kutoka katika Quran.

*((Haimpasii Nabii kuwa na mateka mpaka apigane (sana) na kushinda (barabara) katika nchi (ndipo achukue mateka). Mnataka vitu vya dunia, hali*

*Mwenyezi Mungu anataka (mpate thawabu za) Akhera! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, (na) Mwenye hikima.))* Al Anfal 67.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Ewe Mtume)! Waombee msamaha (hao wanafiki) au usiwaombee; (yote sawa sawa). Hata ukiwaombea msamaha mara sabiini, Mwenyezi Mungu hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wavunjao amri (Zake)).* At-Tawba 80.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Haimpasii Mtume na wale walioamini kuwatakia samahani washirikina ijapokuwa ni jamaa (zao); baada ya kuwabainikia kuwa wao ni watu wa moto wa Jahanamu.))* At-Tawba 113.

Pia hadithi zimetunukulia mengi miongoni mwa misamaha yake kwa makosa yaliyotendwa dhidi yake mwenyewe au dhidi ya ndugu zake[1].

Vilevile suala la vita haliwezekani kuegemezwa kwa jamii ya Waarabu, jamii ambayo inajipambanua kwa kuwa na roho ya kivita kama asili yao. Kwana wasomi hawaungi mkono uezekano kama huo. Kwa hakika wamethibitisha kuwa damu inaamsha fadhaa katika nafsi za Waarabu na hasahasa Waarabu wa majangwani. Ama wanapolazimishwa kupigana vita, kwa hakika wao wanavikabili badala ya kukubali kudhalilika na kuabika.

Kwa hiyo hapana budi kuna kitu fulani, kilitokea katika muda huo kilichopelekea kutokea kwa huu msimamo mpya. Kiuhalisia Quran inatuletea mbele yetu mandhari inayochangamsha sana. Kwani yenyewe inatunukulia katika masikio yetu sauti ya kuomba msaada ya ‘‘wanaume, wanawake na watoto’’ waliosilimu wakiwa Makka wala hawana cha kuwasaidia waweze kuhama au kujitetea dhidi ya dhulma wanayotendewa. Wanaadhibika kwa ajili ya imani yao, na wanaomba msaada wa Mwenyezi Mungu uwaokoe. Kwa hakika mbegu ya kale – somo na kiigizo – ilikuwa ni yenye kutoa matunda. Na yenyewe ipo mbali na madai mapya yoyote yale. Kila mara imani ilipopepea harakati za kiuadui na ukatili zilicharuka ili kuizima bila huruma.. Kwa hiyo hali itakuwaje..? Je, itakuwa ni haki kwa Muhajirina na Maanswari (Wahamiaji kutoka Makka na Wenyeji wa Madina) wakiwa katika amani yao, wasitilie umuhimu wala kujali chochote juu ya majaliwa ya ndugu zao wa huko Makka?

[1] Miongoni mwayo ni msamaha wake kwa mjumbe wa Makurayshi aliyeenda ili kumuua baada ya vita vya Badri. Na kwa yule Myahudi wa Kike aliyemwekea sumu. Na yule mwingine aliyemsukuma Zainabu binti ya Mtume na kumtoa mimba. Na msamaha wake kwa wale walioleta habari za uongo, na kwa watu wa Makka wakati wa ukombozi wa mji wa Makka. (Tazama ‘‘Muhammad na Al-Quran’’ cha Saint Hilaire uk 125 – 130).

Je, kimantiki inafaa wanyimwe ‘‘Ukweli’’ na ‘‘fadhila’’ kwa upande wa haki yao ya kupokea msaada, na wauachie ukandamizaji ukipeperusha silaha zake dhidi yao?

Licha ya hayo, kwa hakika msaada huo haukutolewa na Waislamu wa Madina kiwepesi wepesi, kwa uchache katika umbo lake la kivita. Inatosha tukirejea Quran ili tuone upeo wa kusita sita kwa upande wao.. Lakini ulazima wa kujitoa muhanga kwa kiasi kikubwa, muda wake ulikuwa umeshafika. Na Mwenyezi Mungu alitaka kutenganisha katika huo mgogoro uliokuwepo baina ya haki na batili. Kwa kiasi ambacho mateso yalikuwa yana mrengo wa mtu mmoja mmoja binafsi. Kwa upande wao Waislamu walijilazimisha kujizuia na kitendo rejeshi chochote cha kutumia nguvu kwa muda wao wote waliokaa Makka. Walivumilia majeraha yao kwa ushujaa mkubwa. Ama baada ya kugubikwa chuki za washirikina dhida ya Waislamu na mrengo wa kimbari na kugeuka kuwa ni vita vya kuangamiza. Hapo ndipo Waislamu – na hiyo ni baada ya miaka kumi ya uvumilivu madhubuti – waliporuhusiwa wasimame kwa pamoja[1] wajitetee kwa pamoja. Kutetea uwepo wao na kuwanusuru ndugu zao ambao hawana msaidizi. Na hapana shaka kwamba hukumu ya uadilifu inakubali kuwa hakuna lawama katika hali kama hii ya kujilinda tu kulikotukuka kwa hali ya juu. Hayo ndio mazingira yalipoanzia cheche za vita vya kisilaha vya kwanza vya Waislamu.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na (katika kuwaokoa) wale walio dhaifu – katika wanaume na wanawake na watoto – ambao husema: ‘‘Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe tuna mlinzi anayetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuu anayetoka kwako.’’ Wale walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini waliokufuru wanapigana katika njia ya shetani. Basi piganeni na marafiki wa shetani. Hakika hila za shetani ni dhaifu.))* An Nisaa 75 - 76.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Mmelazimishwa kupigana vita (kwa ajili ya dini). Nalo ni jambo zito kwenu …))* Al Baqarah 216.

---

[1] Amri ya jumla ya kupigana vita ilitoka katika mazingira yasiyo rafiki kwa Waislamu. Kiasi ambacho haiwezekani kwetu sisi kuafikiana na Dr. Sanclair aliyedai kuwa kanuni za Kiisalamu zilikuwa zinarekebishwa kulingana na ushindi wa Muhammad (uk 279). Kama alivyoipindua maana ya (Al Baqarah 2017) inayolaani uadui katika miezi mitukufu (uk 276) na akazingatia kuwa hizo ni njia za ukandamizaji wa kigaidi (Al Maidah 33). Ni muundo mpya wa vita unaozingatiwa kuwa ni hatua ya tatu katika mwendelezo huo (uk 277).

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu *((... Na wakasema: ‘‘Mola wetu! Kwa nini umetulazimisha kupigana? Lau ungetuakhirisha mpaka muda kidogo hivi (ingekuwa vizuri).’’ Sema: ‘‘Starehe ya dunia ni ndogo. Akhera ni bora zaidi kwa hao wenye kumcha Mungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi ulio katika uwazi wa kokwa ya tende.’’))* An Nisaa 77.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu *((Popote mlipo mauti yatakufikieni...))* An Nisaa 78.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((... na jingine makafiri. (Makafiri) wakawaona (Waislamu) zaidi kuliko wao mara mbili kwa kuona kwa macho...))* Aali Imran 13.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Na (kumbukeni) Mwenyezi Mungu alipokuahidini moja katika mataifa mawili ya kwamba ni lenu. Nanyi mkapenda mupate lile lisilo na nguvu; na Mwenyezi Mungu anapenda kuthubutisha haki kwa maneno yake na (anapenda) kuikata mizizi ya makafiri. Ili kuthubutisha haki na kuiondoa batili; hata wakichukia watu wabaya.))* Al Anfal 7 – 8.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni muweza wa kuwasaidia; Ambao wametolewa majumbani, (mjini) mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: ‘‘Mola wetu ni Mwenyezi Mungu.’’ Na kama Mwenyezi Mungu asingaliwakinga watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa na nyumba nyingine za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda.))* Al Hajj 39 – 40.

Lakini kuna swali linalojikita, na kimsingi ni kuhusu kama sheria za Quran zilirekebishwa baada ya muda, hivyo zikapanua wigo wa haki ya kujilinda hadi ikajumuisha kila aina ya uadui.

Inaonekana kuwa maarifa ya ulimwengu wa kimagharibi hayatoshi katika nukta hii. Kwani itikadi inayotawala kwao wao ni kuwa – ni haki kwa umma wa Kiislamu – bali hata kwa mujibu wa vitabu vyao vitakatifu – kutumia silaha, sawa sawa kwa lengo la kuwalazimisha watu wafuate dini yao au kuwaua wale wote wanaokataa kuingia dini yao. Na jambo hilo wanaliita ‘‘vita vitakatifu’’ na ibara hiyo wanaifanya iafikiane na neno ‘‘Jihadi’’ wakati ambapo neno hili

linakusudia ‘‘Kutoa juhudi’’. Kwa hiyo halina uhusiano wowote na upande wa kijeshi. Na kwa kuwa lenyewe limeteremka katika sura za Makka likiwa na maana ima kutoa juhudi katika kutoa mawaidha, kulingania na kujadiliana kwa wema. *((Basi usiwatii makafiri, na ushindane nao kwa (Qurani) hii mashindano makubwa.))* Al-Furqan 52. Ima kwa kutoa juhudi binafsi yenye taswira ya kitabia njema peke yake. *((Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu…))* Al-Ankabuut 69. Ama neno linaloeleza vita vya kweli kweli ni neno ‘‘Qitaali’’.

Na kwa kurejea katika maandiko ya Quran, inatuwekea wazi mada, lengo na mipaka inayokusudiwa na uwekwaji wa sheria ya Quran nyuma vita. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: *((Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni) Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.))* Al-Baqarah 190.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Lakini kama wakikoma, (basi); na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu. … Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa madhalimu.))* Al-Baqarah 192 – 193.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *(( … Na kama wakijitenga wasipigane nanyi na wakakuleteeni amani, basi Mwenyezi Mungu hakukufanyieni njia juu yao. – Mtawakuta wengine wanaotaka kupata salama kwenu na kupata salama kwa watu wao… Basi kama hawajitengi nanyi wala kukuleteeni amani wala kuzuia mikono yao, basi wakamateni na kuwaua popote mnapowapata (kama wanavyokufanyieni). Na hao ndio ambao tumekupeni juu yao hoja zilizo dhahiri (za kujuzu kupigana nao).))* An Nisaa 90 – 91.

Na katika sehemu nyingine tunakuta utofautishaji huo huo katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia ihsani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakukufukuzeni katika nchi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu. Mwenyezi Mungu anakukatazeni na wale ambao wanapigana nanyi katika dini, na kukufukuzeni katika nchi zenu, na wanasaidia katika kufukuzwa kwenu; (anakukatazeni) kuwafanya marafiki…))* Al-Mumtahinah 8 – 9. Na katika suratul At-Tawba tunaona uangalizi uliotolewa na Quran katika kuwatoa washirikina ambao hawajavunja mikataba yao, hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweka wazi na kusema: *((Isipokuwa wale*

*mlioandikiana nao miongoni mwa hao washirikina, kisha hawakukupunguzieni chochote wala hawakumsaidia yoyote juu yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda wao…))* At Tawba 4.

Ama sehemu ambazo Quran inawahimiza waumini kwa ajili ya vita zinadhihiri katika aya zaidi ya moja: *((Je, hamtapigana na watu waliovunja ahadi zao na wakafunga nia ya kumfukuza Mtume, nao ndio (pia) waliokuanzeni mara ya kwanza? Je, manawaogopa? Basi Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi mumuogope; ikiwa nyinyi mumeamini. ))* At Tawba 13. Kutokana na hilo, kwa hali halisi ilivyo, ndipo Mwenyezi Mungu akawaamrisha waumini katika kauli yake Mtukufu: *((… Na nyote piganeni na washirikina kama wao wote wanavyopigana nanyi; na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaomuogopa.))* At Tawba 36. Lakini vita hivi vinasimama mara tu wanapotekeleza mikataba, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: *((… Basi maadamu wanakunyokeeni kwa uzuri nanyi pia wanyokeeni kwa uzuri, hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaomuogopa.))* At Tawba 7.

Hutokuta katika sehemu yoyote ya Quran idhini ya kuanza vita. Na hakika si vinginevyo, maamrisho ya Quran yanategemeana na msimamo wa kiadui wa adui. Na zaidi ya hayo ni kwamba, hata kwa wale washirikina ambao hawahusiani na waislamu kwa mkataba wowote, waislamu wanatakiwa wawalinde. Tunaiona Quran ikimtaka Mtume rehema na amani ziwe juu yake awafikishe wao katika sehemu zao za amani, hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: *((Na kama mmoja wa washirikina akikuomba umlinde (ili asikie maneno ya Mwenyezi Mungu), kisha (akitoyakubali usimlazimishe wala usimdhuru, bali) mfikishe mahala pake pa amani (kama hataki kufuata Uislamu); na haya ni kwa ajili ya kuwa hao ni watu wasiojua.))* At Tawba 6. Kwa hiyo majukumu yote ya kivita yapo kwa mwenye kuanzisha vita. Na pale Quran inaposema: *((Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni) Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.))* Al-Baqarah 190. Kwa hakika anawakusudia kwa maneno hayo wale wanaopigana vita vya kweli kweli na kubeba silaha. Na hadithi za Mtume rehema na amani ziwe juu yake zimeweka wazi sharti hili kwa uangalifu mkubwa sana na kuondoa shaka zote: Wanawake, watoto, wakongwe, vipofu, wasiojiweza, wendawazimu, wakulima katika mashamba yao, na wenyekuabudu katika nyumba zao za ibada[1] hawataguswa

---

[1] Kama ingekuwa anakusudia vita ya kuipiga vita dini nyingine basi ingekuwa kuwapiga viongozi wa kidini ndio lengo la vita hivyo.

katika operesheni za kivita. Yaani na tendo lolote linalopelekea kuangamiza kwa namna ya jumla jamala kama mafuriko na moto… Na katika kutekeleza hukumu ya Quran ya kuwasamehe wale ambao wanaacha vita, Mtume rehema na amani ziwe juu yake ameusia na kusema kuwa ni haramu kumfuatilia adui aliyekimbia uwanja wa vita.

Kwa hiyo lengo la sheria hizi limewekwa wazi.. Zinduka, nalo ni ‘‘Kuondoa hatari’’. Uislamu unalaani moyo wa kuangamiza na moyo wa kudhibiti kila kitu, katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: *((Hiyo nyumba ya akhera tutawafanyia wale wasiotaka kujitukuza katika ardhi wala (kufanya) ufisadi, na mwisho (mwema) utawathubutukia wacha-Mungu.))* Al-Qasas 83. Na Quran haitaki kulazimisha kufuatwa kwa ‘‘itikadi ya dunia’’, *((Na kama angalitaka Mola wako (kuwalazimisha kwa nguvu kuamini) bila shaka wangaliamini wote waliomo katika ardhi (asibaki hata mmoja). (Lakini Mwenyezi Mungu hataki kuwalazimisha watu kwa nguvu) Basi je, wewe utawashurutisha watu kwa nguvu hata wawe Waislamu?))* Yunus 99. Kwa hiyo tofauti za kidini zitaendelea kuwepo baina ya watu, *((Na kama Mola wako angalipenda, angaliwafanya watu wote kuwa umati mmoja. (Angaliwafanya wote kufuata kitu kimoja. Lakini amewapa akili na nguvu ya kutumia akili zao hizo watakavyo, ikiwa kwa wema au kwa ubaya). Kwa hivyo wataendelea tu kuhitilafiana.))* Hud 118.

Na imani inatulizana kwa wachache miongo mwa watu, *((Na wengi katika watu hawatakuwa wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.))* Yusuf 103. Na Uislamu unasimama kidete dhidi ya yule anayepinga njia ya uhuru na kuwatumbukiza watu katika fitina na si kinyume chake.

*((Wanakuuliza (hukumu ya) kupigana vita katika miezi mitakatifu. Sema: ‘‘Kupigana vita katika (miezi) hiyo ni dhambi kubwa. Na kuzuilia watu na dini ya Mwenyezi Mungu, na kumkanusha (Mwenyezi Mungu), na (kuwazuilia watu) Msikiti huo mtakatifu, na kuwatoa humo watu waliomo, ni (dhambi) kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na kuwazuilia watu na dini yao ni mabaya zaidi kuliko kuuwa.’’ Wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika dini yenu, kama wakiweza. … ))* Al Baqarah 217.

Je, maana ya hiyo ni kwamba ‘‘kuwaongoza’’ watu au ‘‘kuwapotosha’’ si muhimu kwa Waislamu? Hii ndio tafsri ambayo wakati mwingine wanajaribu kuileta kwa usamehevu wa Waislamu kwa dini nyingine. Kwa hakika hii ni njia nyingine ya kupinga tabia ya halisia ya Quran.. Hakika wao wanainasibisha na

siasa kali na kutia chumvi mno katika kuwalazimisha watu waipende misingi yake. Imma kuonesha kuwa Uislamu umechoka na matamanio haya na haujali. Isipokuwa msimamo halisi wa Quran hauwakilishwi na upande wowote katika pande mbili hizi. Kwa hakika Quran inasisitiza ulazima wa kuwaita watu waende katika haki na mambo mazuri kwa hima kubwa. *((Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaoamrisha mema na wakakataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekewa.))* Aali Imran 104. *((Basi usiwatii makafiri, na ushindane nao kwa (Quran) hii mashindano makubwa.))* Al-Furqan 52. Na kwa muundo unaopambika kwa hekima, kutosheleza na upole. Na huyo wa upande mwingine aamini kile anachokisikia au asikiamini. Kisha baada ya hapo, ni juu yake asibane uhuru wa waumini katika kutekeleza ibada zao. Na kila mtu abebe majukumu yake kikamilifu.

*((Si juu yako kuwaongoa; lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. (Juu yako ni kuongoza tu). Na mali yoyote mtakayoyatoa ni (faida) kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Na mali yoyote mtakayotoa mtarudishiwa kamili (thawabu zake), wala hamtadhulumiwa.))* Al Baqarah 272.

*((Enyi mlioamini! Lililo lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni waliopotoka ikiwa mumeongoka. Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu; basi atakwambieni yale mliyokuwa mkiyatenda.))* Al Maidah 105.

Kwa hiyo msingi wa Quran ni msingi wa kuvumiliana/kusameheana. Na huenda jina hili likawa chini ya uhalisia wenyewe katika baadhi ya maeneo kwani tunaona:

**Mosi**: Kwa hakika wananchi wasiyoikubali itikadi ya Kiislamu lakini wanatii sheria zake za kiraia kwa amani. Kwa hakika wananchi hao wanakuwa wapo sawa na wananchi waislamu. ‘‘Wao wana haki kama ile iliyokwetu pia wana wajibu kama ule ulio kwetu’’.

**Pili**: Ama wale ambao hawaikubali itikadi ya Kiislamu wala sheria za Kiislamu. Kwa hakika Quran inawataka wao wawe na msimamo wa amani kuwaelekea Waislamu ili wafanyiane muamala ambao msingi wake ni uadilifu na wema. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: *((Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia ihsani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakufukuzeni katika nchi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu.))* Al-Mumtahinah 8.

Ama kafiri atakapoelekeza na kulenga mapigo yake kwa itikadi ili aizime nuru ya itikadi. Je, inaingia akilini dini isimame mikono nyuma, mbele ya yule anayeiangamiza muangamizo timilifu? Kwa hakika Waislamu wameshaishi na uzoefu wa aina mbili katika nyakati zake za mwanzo kabisa na kutanabahi ya kwamba hakuna kilicho sawa na kubadilishana fikra kwa uhuru na amani. Hadi pakasemwa: Kwa hakika idadi ya wale waliosilimu – wakati wa suluhu ya Hudaibiya – pale ambapo mipaka ya kambi mbili ilikuwa wazi. Ilifikia idadi inayozidi idadi yao kwa miaka yote iliyopita kwa pamoja. Na kwa hali yoyote ile, inamlazimu kila anayedai kwamba eti amegundua lengo lingine la mfumo wa vita katika sheria za Kiislamu basi na atutajie idadi ya makadirio ya wafuasi walioingia ndani ya Uislamu kwa sababu ya njia na michakato ya mateso.

Tunaweza tukachukulia kuwa kulitokea makosa katika nyakati za misukosuko, kama inavoweza kushukiwa katika baadhi ya kupotoka kwa vizazi vilivyofuata. Lakini, hebu na tusikie maungamo ya mmoja ya wakosoaji wakuu wa zama za sasa na ambaye yeye ni miongoni mwa wale ambao hawaungi mkono mfumo wa Kiislamu ‘‘Licha ya vikwazo rasmi vilivyokuwa vinazuia watu wasiingie katika Uislamu, lakini bado watu waliendelea kuingia katika dini hii makundi kwa makundi… Na kamwe hakujawahi tokea mbedui hata mmoja – naye akiwa katika kilele cha hamasa juu ya dini yake mpya – aliyefikiri kuizima itikadi ya dini nyingine kwa kumwaga damu.. Kamwe haijawahi tokea kwamba Khalifa ameendesha opereshi za ukandamizaji kwa Wakristo au wazandiki’’[1]

Na kwa vyovyote vile, hakika huzuni na maumivu ambayo tunaweza kuyanasibisha na vita vya Kiislamu yalikuwa ni kidogo mno. Na vita vyao vilikuwa vya haraka mno. Jambo ambalo linatuchukua sisi tuamini kuwa milango ya miji ilikuwa ipo wazi mbele ya majeshi ya ukombozi wa Kiislamu. Na haikuwa kingine juu yao ila kuisukuma tu ili kuifungua.. Hebu na tujikumbushe harakati za marekebisho ya Kiporestanti wa Ulaya, na ambazo hazikushughulikia kubadilisha ila misingi michache tu ya Kikristo – ziliigharimu Ulaya ndani ya kipindi cha karne moja na nusu maumivu na wahanga ambayo yanazidi juu ya hayo kwa wingi.

Kwa hakika kama jengo feki litadumu kwa kitambo fulana cha wakati kwa kutegemea nguvu ya kitu inachokitegemea. Lazima litaporomoka pale vile inavyovitegemea na kumsaidia kubaki na ambavyo ni vigeni kwake

[1] Gauthier ‘‘Tabia na Ada za Waislamu’’ Uk 207, 208 na 217.

vinapotoweka. Je, leo tunaona nini baada ya kupita karne kumi na nne na baada ya kukoma kwa kujitanua kwa Uislamu? Kwa hakika jengo la kijamii ambalo katika kipindi kirefu cha historia yake kimetokewa na visababishi vingi vya kuliangamiza vya ndani na vya nje, na zaidi ya hayo hilo ni jengo la dini na mwenendo mwema ambalo bado linaendelea kusimama kidete likiwa thabiti kabisa na gumu mno. Hadi likafikia kuelezwa kwa haki kabisa kuwa ‘‘Kwamba tangu kuanza kwa hijra (kuhama) haijawahi kutokea kuwa Mwislamu amebadili dini yake na kuingia dini nyingine’’. [1]

Na kwa hali yoyote ile tunaweza kukazia kuwa Waislamu wa leo hii ndio walio tayari kwa kiasi kidogo sana kukubali kuiacha dini yao kuliko wafuasi wa dini nyingine.

Je, hivi si katika jambo linalopingana na kanuni za kisaikolojia kuunasibisha mshikamano huu na aina fulani ya kujisalimisha kwa kurithi ambapo asili yake inarejea katika kulazimishwa kulikotokea kwa wazazi wa Waislamu wa mwanzo na kwamba hakika wao wanaendelea kudumisha kumbukumbu hiyo ikiwa imenakshiwa katika kina cha bongo zao?.. Hakuna mjadala ya kwamba ni jambo lililokatiwa shauri kwetu sisi na tunapaswa kukubali kwamba kuna sifa baadhi ya sifa za ndani katika Uislamu zilizouezesha Uislamu kusambaa na kuthibiti licha ya kuzaliwa kwake kwa muda mrefu uliopita.

[1] ‘‘Hotuba za Ufunguzi’’, kimeshatafsiriwa kwa lugha ya Kifaransa na mtunzi wake ni ‘‘Porter katika Utangulizi wa ‘‘Quran’’ mwandishi ‘‘De Ryer’’.

# MLANGO WA PILI

## QURAN KUPITIA MIONEKANO YAKE MITATU:

## KIDINI, KITABIA NA KIFASIHI

## Utangulizi

Ikiwa Quran daima imeathiri akili zisizo na mzaha zilizotofauti tofauti, basi hakuna budi kuwa Quran ina mvuto wa kipekee.

Na hivyo ni kwa kuafikiana kwake kikamilifu na njia za watu katika kufikiri na kuhisi.

Na kwa kuitikia kwake kile kinachotarajiwa na nafsi katika mambo ya itikadi na tabia.

Na kwa namna Quran inavyotoa utatuzi wa mafanikoa kwa matatizo makubwa yanayoleta vihoro.

Na kwa maana nyingine, hapana budi kwamba Quran inajumuisha yale yanayoshibisha haja za watu za kupata haki, heri na uzuri. Kwa vile inavyokusanya pamoja miongoni mwa sifa za matendo ya kidini, kitabia njema na kifasihi kwa wakati mmoja.

## Sura ya kwanza
## Haki au ni agenda ya kidini

Kwa hakika mambo muhimu yanayoonekana katika nguvu kumbakumba ijipambanuayo nayo wito wa Kiislamu inajificha – kwa rai yetu – katika njia ambayo imewasilisha kwa njia hiyo ukweli wa dini kwa lengo lililoweka ukomo wa tofauti zilizoibuka dhidi yake.

Baada ya dini nyingine kujibu maswali makuu mawili ya kiitikadi ambayo kwa maswali hayo zimetofautiana fikra za kifalsafa nayo ni: ‘‘Chanzo cha ulimwengu ni nini?.. Na mwisho wake ni upi?’’ Dini hizi zimeasisiwa kwa kujibu mfumo kamili wa itikadi na ibada zilizototofautiana kwa kutofautiana nyakati na jamii mbalimbali. Hata taswira ambayo imetufikia kuhusu dini hizo imeshaingiliwa na kupingana na kuhitilafiana katika muundo wake na hata katika misingi yake mikuu.

Kwa hakika Quran imezingatia sana juu ya fikra kwamba Mitume yote ya Mwenyezi Mungu inatiana nguvu yenyewe kwa yenyewe. Na wanashikamana katika kufikisha hakika moja. Na kwamba Manabii ni umma mmoja chini ya Mwenyezi Mungu Mmoja. Na kwa hakika umoja huu ulikuwa ukiwakusanya watu mbalimbali katika muda uliopita. Na kwa hakika si jinginelo, vizazi vilivyokuja kuungana nao, ndivyo vilivyosambaza kuhitilafiana na mfarakano.

Na Quran, huku ikiwasilisha wito wa Kiislamu kwa njia yake ya kimantiki. Uislamu kwa kuuzingatia eti wenyewe ni wito mpya wa Kimuhammadi ulio huru na unaoshindana na wito wa Kimussa na Kiyesu, na kugombana na miito hiyo miwili kwa hakika ya kidini. Hakika si vinginevyo, Quran inakiri kuwa Mwislamu ni yule ambaye kwa wakati mmoja anamwamini Mussa na Yesu na mitume yote ya Allah. Na kuwaheshimu wote bila kubagua baina yao. Pia anaamini vitabu vyao na misingi yao wao wote. Yaani Mwislamu anajisalimisha kwa Allah na kwa matakwa yake ambayo ameieleza mfululuzo kwa ndimi za Manabii na Mitume. Na kwa hili inawanyanyua watu kuwa juu ya mpasuko na kushindana. Na katika umoja huu watu wanapata kulingana kwa mizania ambako mtu hawezi kuukataa akitaka raha ya dhamiri yake. Kwa kuwa, muda ambapo itikadi yangu inakubaliana na itikadi inayotangazwa na hawa Mitume, kwa hapo sababu zinazohalalisha kuipinga itikadi hiyo zitakuwa zimeshaondoka…

Kwa hiyo, Quran inawaita watu warudi katika umoja wa kidini wa asili ambao unapokelewa, kukubaliwa na kujifaharishia na wale wenye nafsi tukufu. Na nyoyo zao zenye shauku zinafunguka kwa ajili ya itakadi hiyo. Na hapana shaka kuwa hii ni hatua ya kwanza na ya lazima, kisha baada ya hapo unakuja umuhimu wa mfumo na njia katika Uislamu.

Na tunaona kuwa nukta ya kuanzia na mbegu ambayo pembezeni mwake unazunguka mfumo wa utosheleshaji wa Quran umejikita katika fikra kuu hii: nayo ni kuwa Muumba anasifika na ukamilifu usio na mipaka, nguvu zisizo na mipaka na heri zisizo na mipaka, ameumba kila kitu kilichopo. Na akakiweka chini ya matakwa yake kikamilifu bila ya kuwa na mipaka. Na siri ya mafanikio ya fikra hii ni kuwa yenyewe inaendana kikamilifu na fikra ya dini moja ambayo Uislamu unalenga kuirejesha upya katika uhalisia wa maisha. Kwani kufarikiana hakuanzi ila kukiwa na dini nyingi. Na zaidi, ni kuwa utukufu wa fikra hii upo juu zaidi kuliko mazingatio yote finyu katika dini mbalimbali. Uislamu unawakumbusha watu ukweli wa milele walioujua au ambao ni mwepesi kwao wao kuujua.

Isipokuwa  upweke huu wa Mungu wa mwanzo au dini hizi za kinadharia – kama zinavyoitwa na Quran – zilikuwa zimezibwa, na kufunikwa chini ya kifusi cha itikadi na ibada zilizokuwa zinapelekea katika idadi isiyohesabika ya miungu kwa Waarabu .. Kama ilivyokuwa kwa watu wa kitabu, ambao na wao pia walifaulu katika kuwajumuisha pamoja baina ya Mungu Mpweke ambaye ni Muumba na idadi kadhaa ya miungu mingine inayoabudiwa. Jambo lililoufanya mtazamo wa Waarabu uwe wa kusema kuwa, kwa hakika miungu yote ni mungu mmoja. Hii ni kauli ya ajabu na ya uongo iliyofikia kiwango cha hao Waarabu wenyewe kudai kuwa hawajapatapo kuisikia kauli hiyo katika jamii zao, wala katika dini za mbinguni zilizotangulia. Kwa hakika Uislamu ukaja kuitoa fikra hii iliyogubikwa (na makandokando) na kuirejeshea jamii utakatifu na usafi wake unaoepukana na kila mazonge. Kwa hiyo Uislamu haukugundua wala kuvumbua dini mpya. Na hakika si vinginevyo Uislamu ulifupisha njia yake kwa kuondoa mazonge na sio kuongeza mapya. Na hivi hivi tunaona – kama tulivyogusia – ya kwamba nguvu ya fikra ya kidini inajikita katika tabia au maumbile yake asilia. Kwa hakika fikra hiyo inatusukuma kuiamini kwa nguvu ileile ya ilivyokita mizizi yake katika vina vya itikadi za wazee wetu wa mwanzo. Iliyojisimika hapo kale. Na kwa ajili hii tunaiona Quran – zaidi ya kutumika kwake katika kutolea ushahidi wa kimantiki – inaweka msingi wa wito wake katika upwekeshaji kama ilivyo katika historia ya Manabii katika

kila zama zilizopita. Kwa hiyo Quran inathibitisha kwa uwazi kuwa akili na maandiko vinashirikiana na Quran katika kuthibitisha itikadi ya upwekeshaji. Na kuukataa upagani na kumshirikisha Mwenyezi Mungu kwa namna zake zote zinazotofautiana.

Lakini inawezekanaje tufasiri, eti jambo nyeti kama hili linalotegemea mantiki na asili iliyokita mizizi, na daima linajisasisha kwa mafundisho chanya ya manabii – eti linaweza kutoweka kirahisi rahisi katika bongo za watu na badala yake ziingie fikra kinzani zake? Na sababu ni kwamba mwanadamu kwa maumbile yake anahisi kuwa anasukumwa kuipenda nguvu isiyo ya kawaida popote anapoipata. Na kutoka katika kupenda anaelekea katika ibada, kuna hatua zinazofuatana na hakuna katika hatua hizo isipokuwa tofauti za daraja. Kwani nguvu za kimaumbile kama vile jua, miti na chemchem ni maajabu yanayochukua akili za wenye kuyazingatia. Waona kwa matukio yaliyokinyume na maumbile ambayo yanatekelezwa na mikono ya mchawi au mtengeneza miujiza? Kwa kutumia mwongozo wa hisia za nje, utambuzi unaegemea kwa wepesi katika kuinasibisha asili ya tukio lolote katika chanzo chake kilicho pamoja nalo. Yaani kwa kitu ambacho kutokana na kitu hicho tukio limeanzia likiwa ni kama athari ya sababu ya kweli yenye nguvu ya kutenda na iliyohuru.

Na utambuzi hauwezi kunyanyuka kutoka katika taathira ya tukio kwenda katika chanzo chake, na kutoka katika kitu kinachogusika kwenda katika kitu dhahania, isipokuwa kwa juhudi za kifikra za kutaka, lakini ni mara chake kutolewa juhudi kama hizi. Wakati ambapo miongoni mwa malengo makuu ya Quran ni kuzitakasa na kuziunga mkono juhudi hizi kwa nguvu kubwa. Na hiyo Quran daima inatukumbusha kuwa ni muhali (jambo lisilowezekana) kutokea kiumbe chochote kutokana na kutokuwepo kitu au nguvu ya kuumba. Na ni muhali kitu kujiumba chenyewe. Au kuumba kila kiumbe bila mipaka huko mbinguni au ardhini. Wala hata kuumba mdudu yeyote hata kama kutakuwepo na nguvu na juhudi zote kwa ajili ya kuliendea lengo hili. Bali kama inzi atanyakuwa kitu kinachomilikiwa na mtu mwenye nguvu zaidi duniani. Basi mtu huyo hatoweza kukirudisha hicho kitu kutoka kwa inzi huyo. Kwa hiyo wote – isipokuwa Allah – hawamiliki hata chembe ndogo ya nyuklia huko mbinguni au ardhini. Si kwa kushiriki katika kumiliki wala kuwa wafuasi wa umiliki.

Hakuna yeyote isipokuwa Allah anayeweza kubadilisha mfumo wa kimaumbile wala kuubakisha kama ulivyo. Na kanuni za kimaumbile ambazo hata kwa kuziingilia kwetu hatuwezi kuzirekebisha kwa chochote. Kwa hakika

kuthibiti kwake kwa upande wa Muumba – ni hali ya kila kanuni ya kusababisha – imesimamia juu ya neno moja katika matakwa ya Allah Mtukufu.

Lau angalitaka angaliyafanya maji ya mvua kuwa ya chumvi yenye uchungu. Na mbingu angeidondosha juu ya ardhi. Na angaliondosha jamii ya wanadamu wote. Na ardhini angalileta viumbe wengine kuchukua nafasi ya mwanadamu. Nguvu zote ni za Allah. Kwani sababu za karibu na za mbali, na mambo yote yapo mkononi mwa huyu Muumba Mtukufu. Na kwake yeye tu ndio marejeo na mwisho wao.

Kwa kusikiliza hadithi hii tukufu huenda tukaegemea katika kuitakidi kuwa kuna uwezo mkuu ambao kwake yeye mwingiliano wowote wa kibinadamu hauna faida. Kwa hakika uwezo huu ni wenye kuepukana na chochote kikamilifu uliolazimishwa ulimwenguni.. Kwa kiasi ambacho mahusiano yoyote ya kisababu baina ya vitu yanapotea kikamilifu.

Itikadi hii – zaidi ya kukutaana na akili na kupingana na sayansi – inapingana na makundi mawili ya aya za Quran, la kwanza linalowataka watu, daima wafanye juhudi za kitabia njema. La pili linalofasiri matukio ya kimaumbile na kihistoria baadhi yake kwa mengine. Na jibu la sawasawa ni lile linaloanisha upeo na malengo ya kila hakika miongoni mwa mambo ya hakika yanayokubalika. Na hatutoi kumpa mwanadamu na ulimwengu uwezo wa dhati unaojitegemea ukamilifu wa kujitegemea. Wala hatumsifu mwanadamu kuwa ni mtu asiyeweza chochote kabisa kabisa. Na huu ndio msimamo wa kati na kati unaoingia akilini na ambao Quran inatuita tusimamie hapo. Kuna sintofahamu ya kukataa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kuwa yeye ndiye muumba miujiza. Kama vile, huenda kukawa na uwezekano wa kuing`arisha nukta hii na kusema ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakutoa miujiza au hoja za kutosha ili kuthibitisha utakatifu wa wito wake. Na ukweli ni kwamba mazingira yote ambayo si ya kawaida yanayoambatana na kudhihiri kwa Mitume na Manabii rehema na amani ziwe juu yao ili kufikisha jumbe zao na kuhakikisha mafanikio yao. Quran haioni kuwa mambo yote hayo ni matendo ya kibinadamu. Kwani ni kwa kudura ya Allah ndio inatokea miujiza hii au ile. Mikononi mwa hawa Manabii au katika ndimi zao.. Mwanzoni katika ujumbe wa Uislamu, kusoma baadhi ya aya za Quran, zilikuwa zinaweza kumbadili kafiri mpingaji kutoka katika hali ya umauti wa kimaono na kuwa hai kiroho.

Muhammad rehema na amani ziwe juu yake siye yeye aliyezifungua nyoyo zao. Wala sio yeye aliyewafanya Waislamu wawe ndugu wanaopendana kwa ajili ya Allah. Na wala sio yeye aliyehakikisha ushindi wa kiimani dhidi ya ukafiri na ushirikina.

Kwa hakika matendo haya yanatokea kwa idhini ya Allah na matakwa yake. Na hivyo hivyo miujiza uliyotokea mikononi mwa Mitume na Manabii na Muhammad rehema na amani ziwe juu yake akiwa miongoni mwao.. Hakuna fadhila kwa uerevu wa hali ya juu wa Mtume wala ukubwa wa elimu yake. Kwa hakika fadhila za mwanzo na za mwisho katika hayo zinatokana na kuingilia kwa ukarimu na wingi wa rehema kutoka Upande wa Allah Mtukufu. Ambaye ndiye chanzo cha kweli cha kila kiumbe na kila elimu na kila heri.

Na hivyo hivyo kwa fikra ya Allah mkamilifu asiye na mipaka na sifa zake zisizo na mipaka, ndipo Uislamu ukaweka msingi wa nusu ya kwanza ya uhakika wa dini kwa ujumla. Na msingi huu unafupishika kwa kueleza kuwa hakuna kitu katika vitu vyote vilivyopo kinachostahiki kuabudiwa na kunyenyekewa isipokuwa Allah Mmoja Mwenye kutenza nguvu.

Na kwa fikra hiyo hiyo, Quran ikaweka msingi wa nusu ya pili ya uhakika wa dini kwa ujumla: nayo ni kuamini maisha ya ahera (baada ya kifo). Kiasi ambacho tunatanguliza matendo yetu kwa ajili ya Allah na tunapata kutoka kwake malipo tunayostahiki. Na hapa tunapambanua baina ya nukta mbili: kuishi milele kwa roho na kufufuliwa kwa mwili. Na wito wa Kiislamu haukukabiliwa na upinzani wowote unaotajika kuhusiana na nukta ya kwanza. Isipokuwa imani potofu ya ‘‘Al-haamah’’ iliyokuwa imetawala kwa Waarabu inayoeleza kuwa roho ya mtu aliyeuawa inaendelea kuelea juu ya kaburi la mtu aliyeuawa huku ukisema ‘‘Ninywisheni’’. Na pindi anapolipiwa kisasi na kuuliwa kwa aliyemuua hapo ndipo hiyo roho inapojizuia na haidhihiri tena. Hadithi zimekanusha itikadi hii potofu ya zama za ujinga na kueleza hakuna ‘‘Al-haamah’’ na zikahukumu kuwa itikadi hiyo ni batili. Ama nukta ya pili, hiyo ndiyo ambayo washirikina walijikita kuipinga na kuibeza.

Kwa hakika Quran imeleta hoja zake za kupambanua zitokanazo na kitabu cha maumbile kilicho wazi… Quran ikazitaka akili zichunguze hatua anazopitia mwanadamu katika mzunguko wa maisha. Tangu alipokuwa pande la nyama linaloning`inia mpaka alipokuwa kiumbe mpya akiwa katika umbo la ukamilifu wakati wa kuzaliwa kwake. Je, ni vigumu kwa aliyeanza kuumba viumbe vyote kwa mara ya kwanza tena bila ya kuwa na mfano uliotangulia,

kuweza kuvirudisha kwa mara nyingine..? Na Quran inayaelekeza macho katika matukio ya kimsimu: ardhi ikiwa kame isiyo na mmea inabadilika na kuwa ustawi.. Na Quran imeweka misingi ya itikadi ya kufufuliwa sio tu kwa agizo la Mola ambalo Allah Mtukufu amejilazimisha yeye mwenyewe. *((…Ni ahadi iliyolazimika kwake (kuwafufua na kuwalipa)…))* An-nahl 38. Na hakika si vinginevyo, hilo ni mojawapo ya mambo ya lazima katika uadilifu wa Mungu na lina hekima tukufu. *((Atawafufua) ili kuwabainishia yale waliyokhitilafiana, na ili wajue waliokufuru ya kwamba wao walikuwa ni waongo.))* An-Nahl 39. *((… na ili kila nafsi ilipwe yale iliyoyachuma; …))* Al-Jathiyah 22. Na kama si hivyo basi maisha ya mwanadamu yangekuwa hayana lengo wala maana.

Na hivi hivi ndivyo ilivyowekwa misingi ya dini ya Umoja. Dini ambayo inahubiriwa na Quran. Na kama ikiwa fikra ya kidini imebaki katika msingi wake kama ilivyokuwa siku zote. Basi hakuna shaka ya kwamba dini hiyo imejihakikishia maendeleo ya kweli kwa njia ambayo imewasilishwa kwayo na Quran. Sio tu kwamba yenyewe imetiririsha ushahidi na hoja na zinazoweza kuzitosheleza akili ngumu mno, na vilevile kuzitikisa nyoyo ngumu mno. Na sio tu kwa kuwa Quran imetoa mitazamo yake mipana na ya kina juu ya ulimwengu wa mbinguni na wa ardhini. Ikatoa mawaidha na somo kutokana na kila tukio miongoni mwa matukio ya uumbaji ya ndani na ya dhahiri. Na hakika si vinginevyo mada yenyewe ya dini imedhihiri ikiwa ni yenye kuhusiana na mambo yanayomuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu na marejeo ya roho na zaidi ya hayo inahusika na maana ya uungu. Maana ambayo imekuwa ikijipambanua kwa utakatifu, usafi na utukufu wa aina maalumu, uungu uko mbali na kuwa na mwili wenye kila ubaya, nao una nguvu zipitazo zinazomchukuwa mwanadamu na kumfanya aelee katika ulimwengu wa kiroho – yote haya yamedhihiri kana kwamba imejichumia roho mpya ambayo haikuwa imezoeleka hapo kabla.

## Sura ya pili
## Heri au dondoo ya tabia njema katika Uislamu

Lakini nafsi ya mwanadamu licha ya upande wa haja yake ya kupata maarifa na itikadi. Inahitaji mno kanuni za kiutendaji zenye kuweza kuyaelekeza matendo ya mwanadamu, sawa sawa katika miamala yake na nafsi yake au katika uhusiano wake na watu wengine au na muumba wake. Kwa hakika Quran imeleta mfumo huu unaotosheleza na ni njia makini mno kwa kiasi kiwezekanacho. Na ikaweka mpango katika sekta hii mpango wa wazi. Ambao ataupitia mwanadamu kwa amani na utulivu. Na upande wa matendo katika Quran ulifikia umuhimu mkubwa hadi kufikia kutajwa kwa kukaririwa mara nyingi na kwa uwazi kama sharti ambalo halikwepeki (la lazima) ili kufunikiwa dunia na kupata furaha ya milele huko akhera. Na tutaweka wazi baadhi ya sehemu zilizopewa kipaumbele na wito wa Quran kwa watu kwa fadhila za mada zake na yaliyomo ndani yake yenye thamani kubwa. Na kwa fadhila za mtindo wake katika kuwasilisha hakika ya mambo.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu amepandikiza ndani ya kila mmoja wetu muono wa kitabia njema wa kimaumbile unaotufanya tukadirie na tupende wema kwa dhati ya wema, na kwa wenzetu – na hata kama tutashindwa kunyanyuka na kuufikia usawa huo. Kama muono huo unavyotufanya tujiepushe na tukio lolote na kujishusha.. Hakika sisi tunachukia katika nafsi zetu dosari zetu za ndani, na nafsi zetu tunazitafutia udhuru wa kuzitakasa na dosari hizo. Kwa sababu sisi hatukubali kusifika na aina yoyote ya udhalili.

Na kwa hisia hii ya kiujumla na inayoweza kupambanua baina ya uadilifu na dhulma na baina ya heri na shari, ndipo Quran inapopategemea kwa mara nyingi katika kuweka misingi ya mfumo wake wa kitabia njema. Vilevile inapategemea katika kutoa fasili ya fikra yake ya matendo. Kwani Mtume rehema na amani ziwe juu yake: *((... anawaamrisha mema na anawakataza yaliyo mabaya, na kuwahalalishia vizuri na kuwaharamishia vibaya, ... ))* Al – Aaraf 157. (kwa maana yake ya hakika na ya kimajazi). *((... Sema: Mwenyezi Mungu haamrishi mambo mabaya. ... ))* Al – Aaraf 28. Na inatosha tukitaja kuwa, kule kutegemea kwa Quran katika dhamira ya kitabia njema – katika ujumla wake – ili kupambanua baina ya heri na shari kumetajwa katika maeneo zaidi ya arobaini na matano.[1]

---

[1] Kwa mfano tazama kitabu chetu (Desturi ya tabia njema katika Quran) sura ya tatu – kifungu cha tatu.

Na kwa kuona kwamba hisia hii ya kimaumbile, sio siku zote inakuwa na nguvu na utendaji ule ule kwa kila mtu na kuweza kuwalazimisha wanyenyekee na kutii kanuni ya kimwenendo. Basi jambo hilo linapelekea kuwekwa mtaala kamili katika malezi unaotegemea uerevu na akili pembezeni mwa hisia za kitabia njema, ili endapo hisia hii ikitoweka basi ibaki fikra ya wajibu wa jumla. Na njia bora kabisa ya kuiamsha na kuifanya fikra hii itukuze hisia zetu ni kutaka msaada wa kuungwa mkono kutoka kwa watu waliobobea katika fikra hii miongoni mwa watu wenye busara na Manabii kwa kila zama. Na sio suala la nasibu tu kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake anahubiri yale yaliyotangulia kuhubiriwa na Mitume ya kabla yake. *((Mwenyezi Mungu anataka kukubainishieni na kukuongozeni katika mwendo wa wale waliokutangulieni, na (anapenda) kukukhafifishieni. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.))* An-nisaa 26. Na Quran baada ya kutaja idadi kadhaa ya Mitume amani iwe juu yao, inasema kumwambia Mtume Muhammad rehema na amani ziwe juu yake: *((Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoa. Basi fuata uwongozi wao. ...))* Al-An-am 90. Kiuhalisia, kwa hakika hatukuti msingi wa kitabia njema tunaonukuliwa na Quran ya kwamba wenyewe ni miongoni mwa mafundisho ya Mtume huyu au Mwenye busara yule. Isipokuwa msingi huo umeletwa na Quran katika sehemu nyingine ukiwa kama ni wajibu wa kuutekeleza kwa kundi la Waislamu.

Na katika yafuatayo tutaweka wazi kanuni za kitabia njema kama walivyokuja nazo Mussa na Yesu amani iwe juu yao. Kama zilivyotajwa katika Taurati na Injili. Na tutazikuta zimehifadhiwa kwa uangalizi mkubwa katika aya za Quran. Lakini – si kwa umbo la fungu moja – kama zilivyokuja katika amri kumi na Hotuba ya mlimani – kwa hakika zimekuja kama aya zilizo sehemu tofauti tofauti katika sura kadhaa za Makkah na za Madina. Na kwa mara nyingi zimekuja kwa umbo la aya zilizoteremka kwa tukio husika maalum.

**Zifuatazo ni Amri kumi:**

| Quran Takatifu | Taurati (Kutoka 20:3 – 17) |
|---|---|
| ((Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila Yeye tu…)) Bani Israil 23. | 1- Usiwe na miungu mingine ila mimi. |
| ((… Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu...)) Al-Hajj 30. | 2- Usijifanyie sanamu ya kuchonga,… |
| ((Wala msifanye kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ndiyo sababu ya kukuzuilieni na (kufanya mambo mazuri ya Uislamu)…)) Al-Baqarah 224. | 3- Usilitaje bure jina la Bwana,… |

| | |
|---|---|
| ((Mwenyezi Mungu hatakuteseni kwa viapo vyenu vya upuuzi…)) Al-Maidah 89. | |
| ((… na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi…)) Bani Israil 23. | 4- Waheshimu baba yako na mama yako… |
| ((… wala msijiue (wala msiue wenzenu)…)) An-Nisaa 29. | 5- Usiue. |
| ((Waambie Waislamu wanaume wainamishe macho yao (wasitazame yaliyokatazwa), na wazilinde tupu zao,… Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao…)) An-Nur 30-31. | 6- Usizini. |
| ((Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao;…)) Al-Maidah 38.<br>((… wala hawataiba,…)) Al-Mumtahinah 12. | 7- Usiibe. |
| ((… na jiepusheni na usemi wa uwongo.)) Al-Hajj 30. | 8- Usimshuhudie jirani yako uongo. |
| ((Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhaisha baadhi yenu (kwa vitu hivyo) kuliko wengine.)) An-Nisaa 32. | 9- Usiitamani nyumba ya jirani yako… wala chochote alicho nacho jirani yako. |

Hii ndio misingi ya kanuni za tabia njema anayoizungumzia Issa amani iwe juu yake: *(Kwa hiyo, yeyote atakayevunja mojawapo ya amri ndogo kuliko zote ya amri hizi, naye akawafundisha wengine kufanya hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika Ufalme wa Mbinguni, lakini yeyote azitendaye na kuzifundisha hizi amri ataitwa mkuu katika Ufalme wa Mbinguni).* Mathayo 5:19.

Lakini kuna jaribio la kuufunga wito wa Mussa kuwa katika wajibu wa amri hizi tu za msingi tena baada ya kuzidogesha. Kwa sababu kama tutaendelea na utafiti wetu katika maeneo tofauti tofauti miongoni mwayo ni: (Kutoka 22 – 23, Mambo ya Walawi 19 – 25, Kumbukumbu la Torati 6) tutakutana na sheria nyingine zinazohusiana na matendo ya moyoni na matendo ya viungo. na kwa hilo kumeandaliwa sheria za Injili:

| Quran Takatifu | Taurati |
|---|---|
| ((Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini, watapata adhabu iumizayo katika dunia na akhera;…)) An-Nur 19.<br>((…Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine…)) Al-Hujurat 12. | Usitoe habari za uongo. (Kutoka 23:1) |
| ((… Wala msisaidiane katika dhambi na uadui…)) Al-Maidah 2. | Usifuate genge la watu kutenda uovu… (Kutoka |

| | |
|---|---|
| | 23:2) |
| ((… Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu;… akiwa tajiri au masikini (wewe usitazame). Mwenyezi Mungu anawastahiki zaidi (kuliko wewe)…)) An-Nisaa 135 | Usiwe na upendeleo katika kesi ya maskini (Kutoka 23:3) |
| ((… Na saidianeni katika wema na taqwa…)) Al-Maidah 2. | Saidia wengine (Kutoka 23:5) |
| ((… Na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima na maskini na jirani walio karibu na jirani walio mbali, na rafiki walio ubavuni (mwenu) na msafiri alieharibikiwa, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kulia (kuume)…)) An-Nisaa 36. | Mgeni anayeishi pamoja nawe ni lazima umtendee kama mmoja wa wazawa wa nchi yako. (Walawi 19:34) |
| ((Na ambao katika mali zao iko sehemu maalumu. Kwa ajili ya aombaye na anayejizuilia kuomba (japo muhitaji). Al-Maarij 24 – 25. | Mfungulie mkono wako nduguyo mhitaji wako, maskini wako katika nchi yako. (Kumbukumbu 15:11) |
| ((… Na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima na maskini na jirani walio karibu na jirani walio mbali, na rafiki walio ubavuni (mwenu) na msafiri alieharibikiwa, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kulia (kuume)…)) An-Nisaa 36. | Usimdhulumu mgeni wala kumtesa.. (Kutoka 22:21) |
| ((… Na (pia yanakutajieni khabari hii) yale msomewayo katika Kitabu hiki juu ya wanawake mayatima ambao hamuwapi (mahari yao) waliyoandikiwa…)) An-Nisaa 127.<br>((Basi usimuonee yatima.)) Adh-dhuhaa 9. | Usimtese mjane yeyote aliyefiwa na mumewe wala mtoto yatima. (Kutoka 22:22) |
| ((… Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki…)) An-Nisaa 58. | Unapotoa hukumu uamue kwa haki; usimpendelee maskini wala kumwogopa mwenye cheo. (Walawi 19:15) |
| ((Wala usiwatetee wale wanaokhini nafsi zao. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi aliye khaini mwenye dhambi. Wanastahi watu lakini hawamstahi Mwenyezi Mungu; naye alikuwa yu pamoja nao…)) An-Nisaa 107 – 108. | Jitenge mbali na mashtaka ya uongo. (Kutoka 23:7) |
| ((… na wazuiyao ghadhabu na wasamehe watu (na wafanyiao ihsani);…)) Aali Imran 134. | Usifanye kisasi. (Walawi 19:18) |

| | |
|---|---|
| ((Maangamizo yatawathubutukia wapunjao (wenziwao). Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili. Lakini wanapowapimia kwa (kipimo cha) vibaba au mizani (au vinginevyo), wao hupunguza.)) Mutaffifyn 1 – 3. | Usikose kamwe kuamua kwa haki kuhusu vipimo vya urefu, uzito na ujazo. (Walawi 19:35) |
| ((… Wala usijaalie katika nyoyo zetu undani kuwafanyia Waislamu (wenzetu) …)) Al-Hashr 10. | Usifanye kisasi, wala kuwa na kinyongo juu ya wana wa watu wako; (Walawi 19:18) |
| ((… ‘‘Kuweni wenye kuabudu Mwenyezi Mungu…’’)) Aali Imran 79.<br>((… Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao…)) At-Tawba 108. | Ni lazima muwe watakatifu.. (Walawi 19:2) |
| ((… Wala hawapati, hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa (hao Muhajiri), na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo…)) Al-Hashr 9. | Umpende jirani yako kama unavyoipenda nafsi yako. (Walawi 19:18) |
| ((… Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana…)) Al-Baqarah 165. | Nawe mpende BWANA Mungu wako, kwa moyo wako wote. (Kumbukumbu 6:5) |

Na hivi hivi tunaikuta Quran inaonesha wajibu wake wa msingi nao ni kuhifadhi na kufikisha madhumuni ya vitabu vya mbinguni vilivyopita. *((Na tumekuteremshia Kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia (kama haya ndiyo yaliyoharibiwa au ndiyo yaliyosalimika)…))* Al-Maidah 48. Isipokuwa, hakika mambo yalivyo, ni kutekeleza njia yake ya uwasilishaji ya kuona kuwa ni bora kila somo liwasilishwe katika mnasaba wake. Hebu na tuyafuatilie mawaidha ya Injili na tuone namna kitabu cha Waislamu kinavyoyatia nguvu mawaidha hayo:

| Quran Takatifu | Injili |
|---|---|
| ((Wamependeshwa makafiri maisha ya duniani; na wanawafanyia maskhara Waislamu. Na wale wamchao Mungu watakuwa juu yao siku ya Kiyama…)) Al-Baqarah 212.<br>((… Na hayo ni matumizi ya maisha ya katika dunia; na kwa Mwenyezi Mungu ndiko kwenye | Heri walio maskini rohoni, maana ufalme wa mbinguni ni wao. (Mathayo 5:3) |

| | |
|---|---|
| marejeo mazuri.)) Aali Imran 14. | |
| ((Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya; hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri.)) Al-Baqarah 155. | Heri walio na huzuni, maana watafarijiwa. (Mathayo 5:4) |
| ((Na yaendeeni upesi upesi maghufira ya Mola wenu na Pepo (yake) ambayo iliyowekewa wamchao Mungu.)) Aali Imran 133. | Heri walio wapole, maana watarithi nchi. (Mathayo 5:5) |
| ((Je! Wanafikiri wale waliofanya maovu kuwa tutawafanya kama wale walioamini na kutenda mema – kwamba maisha yao na mauti yao yawe sawa? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu (ya kuwa wote watakuwa sawa.)) Al-Jathiyah 21.<br>((Kwa hakika wale waliokuwa wanafanya madhambi walikuwa wakiwacheka walioamini… Basi leo walioamini watawacheka waliokufuru.)) Al-Mutaffifyn 29 – 34. | Heri wenye njaa na kiu ya atakavyo Mungu, maana watashibishwa. (Mathayo 5:6) |
| ((Isipokuwa mwenye kuja kwa Mwenyezi Mungu na moyo safi; (huyu ndiye atakayepata ya kumfaa)). Ash-shuaraa 89.<br>((Na anayemuogopa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa kurehemu, na hali ya kuwa hamuoni, na akaja kwa moyo ulioelekea (kwa Mwenyezi Mungu)). Qaf 33. | Heri wenye moyo safi, maana watamwona Mungu. (Mathayo 5:8) |
| ((Hakuna kheri katika mengi wanayoshauriana kwa siri. Isipokuwa mashauri ya) wale wanaoamrisha kutoa sadaka au kufanya mema na kupatanisha baina ya watu…)) An-Nisaa 114. | Heri wenye kuleta amani, maana wataitwa watoto wa Mungu. (Mathayo 5:9) |
| ((Mnadhani kuwa mtaingia peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: ‘‘Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?’’ jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu.)) Al-Baqarah 214.<br>((Mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu, na mtasikia udhia mwingi kwa wale waliopewa Kitabu kabla yenu, na kwa wale walioshirikisha (Waarabu). Na kama mkisubiri na kujilinda na aliyoyakataza Mwenyezi Mungu (mtakuwa mmefanya jambo zuri); kwani mambo haya ni katika mambo makubwa ya kuazimia mtu | Heri wanaoteswa kwa sababu ya kufanya atakavyo Mungu, maana ufalme wa mbingu ni wao. (Mathayo 5:10) |

| | |
|---|---|
| kuyafanya)). Aali Imran 186. | |
| ((Kisha awe miongoni mwa walioamini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.)) Al-Balad 17. | Heri walio na huruma, maana watahurumiwa. (Mathayo 5:7) |

Kwa hakika Issa amani iwe juu yake amesema haki tupu pale alipokazia ya kwamba hakuja kuitengua na kuifuta Torati bali kuitimiliza na kuikamilisha.

Yaani ni kwamba yeye alikuwa anawapa wale wa baada yao jukumu la kusimamia usafi wa kitabia, jukumu ambalo lilianzishwa na Mitume ya kabla yake. Jukumu ambalo lilikuwa linatoa nafasi ya kusonga mbele na maendeleo.

| Quran Takatifu | Injili |
|---|---|
| ((… na wazuiyao ghadhabu…)) Aali Imran 134.<br>((… na wale ambao wanapokasirika husamehe.)) Ash-Shuura 37. | Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, msiue na mtu akiua itampasa hukumu. Bali mimi nawaambieni, kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu. (Mathayo 5:21 - 22) |
| ((Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, …)) Al-Hujurat 10.<br>((… Basi muogopeni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu,…)) Al-Anfal 1.<br>((Na wasomee khabari za watoto wawili wa Adamu kwa kweli. Walipotoa sadaka, ikakubaliwa ya mmoja wao, na ya mwingine haikukubaliwa…)) Al-Maidah 27. | Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako yuko ana neno juu yako. Iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako upatane kwanza na ndugu yako kisha urudi uitoe sadaka yako. (Mathayo 5:23 - 24) |
| ((Waambie Waislamu wanaume wainamishe macho yao (wasitazame yaliyokatazwa)… na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupo zao,…)) An-Nur 30 – 31. | Mmesikia kwamba imenenwa, Usizini; lakini mimi nawaambia, kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake. (Mathayo 5:27 - 28) |
| ((Wala msifanye kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ndiyo sababu ya kukuzuilieni ba (kufanya mambo mazuri ya Uislamu)…)) Al-Baqarah 224. | Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiape uongo, ila mtimize Bwana nyapo zako.; lakini mimi nawaambia, Usiape kabisa; hata kwa mbingu, kwa |

| | |
|---|---|
| | maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu. (Mathayo 5:33 - 34) |
| ((Oh! Nyinyi mnawapenda (maadui zenu hao), hali wao hawakupendeni!...)) Aali Imran 119. | Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi. (Mathayo 5:43 - 44) |
| ((… na wakayaondoa maovu kwa mema…)) Ar-Raad 22.<br>((… Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa mema)); Haa Mym Sajdah 34. | Lakini mimi nawaambia wapendeni maadui zenu (Mathayo 5:44) |
| ((… Yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. (Na) kwa walioamini ni mpole na Mwenye huruma.)) At-Tawba 128. | … na kuwaombea wale wanaowadhulumu nyinyi. (Mathayo 5:44) |
| ((… na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) salama.)) Al-Furqan 63.<br>((Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia ihsani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakukufukuzeni katika nchi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu.)) Al-Mumtahinah 8. | Kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je, mmefanya kitu kisicho cha kawaida?... (Mathayo 5:47) |
| ((Sio wema (tu huo peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (katika kusali. Yako na mema mengine). Bali wema (hasa) ni … na wanawapa mali – juu ya kuwa wanayapenda … )) Al-Baqarah 177.<br>((Nao hunyima misaada. (Basi sala zao hazina faida kubwa nao). Maun 7. | Akuombaye mpe, wala usimpe kisogo anayetaka kukukopa kitu. (Mathayo 5:42) |
| ((Ambao hufanya (amali zao ili watu wawaone tu) riyaa.)) Maun 6. | Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao … (Mathayo 6:1) |
| ((Mkidhihirisha wema au mkiuficha au mkiyasamehe maovu (ndiyo ndivyo)…)) An-Nisaa 149.<br>((… na wasamehe na waachilie mbali, wapuuze lililopita…)) An-Nur 22. | Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa Mbinguni atawasamehe nyinyi. (Mathayo 6:14) |
| ((Na mnakula urithi kwa ulaji wa pupa. Na | Msijiwekee hazina duniani, |

| | |
|---|---|
| mnapenda mali pendo la kupita kiasi.)) Al-Fajr 19 – 20. | nondo na kutu viharibupo, na wezi huvunja na kuiba. (Mathayo 6:19) |
| ((Mwenye kutaka jaza ya Akhera tutamzidishia katika jaza yake hiyo…)) Ash-Shuura 20. | Bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wezi hawavunji wala hawaibi. (Mathayo 6:20) |
| ((Mwezi Mungu anakupigieni mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanaogombana, na wa mtu (mwingine) aliyehusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao?...)) Az-Zumar 29. | Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamuwezi kumtumikia Mungu na mali. (Mathayo 6:24) |
| ((Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao; Mwezi Mungu huwaruzuku wao na nyinyi pia…)) Al-Ankabuut 60. | Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula na, mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwavalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao? (Mathayo 6:25 - 26) |
| ((Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao…)) Al-Hujurat 11. | Msihukumu msije mkahukumiwa nyinyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho ndicho mtakachopimiwa. Basi mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? (Mathayo 7:1 - 3) |
| ((Basi waidhishe ikiwa utafaa waadhi)) Al-Alaa 9. | Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, (Mathayo 7:6) |
| ((Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu, (waambie kuwa) Mimi niko karibu nao. Naitika maombi ya mwombaji anaponiomba…)) Al-Baqarah 186. ((Na | Ombeni nanyi mtapewa; (Mathayo 7:7) |

| | |
|---|---|
| Mola wenu anasema: ‘‘Niombeni nitakujibuni…)) Al-Muumin 60. | |
| ((… Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya hali nyinyi wenyewe msingevipokea isipokuwa kwa kutoviangalia…)) Al-Baqarah 267.<br>((Na waogope (mawasii kuadhulumu mayatima; na wakumbuke) kama na wao wangewacha nyuma yao watoto madhaifu wangekuwa na khofu juu yao…)) An-Nisaa 9. | Basi yote mtakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; (Mathayo 7:12) |
| ((Je! Ameukata huo mlima, (njia nzito ya kumfikisha Peponi.)) Al-Balad 11. | Ingieni kupitia mlango ulio mwembamba. (Mathayo 7:13) |
| ((Na katika watu kuna ambao kauli zao zinakufurahisha hapa duniani. (Lakini Akhera utabainika uovu wao). Nao humshuhudisha Mwezi Mungu kwa yaliyomo nyoyoni mwao, na hali wao wagomvi wakubwa kabisa. Na wanapoondoka, wanakwenda huku na huku katika ardhi kufanya uharibifu humo na kuangamiza mimea na roho. Na Mwezi Mungu hapendi uharibifu. Na wanapoambiwa, ‘‘Mcheni Mwezi Mungu,’’ mori wao huwapeleka zaidi kwenda kufanya madhambi hayo…)) Al-Baqarah 204 – 206. | Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. (Mathayo 7:15) |

Katika wasilisho lililopita, mada mbili kutoka katika Agano Jipya nazo ni talaka na kisasi mada hizo zinazoonekana kana kwamba zenyewe zinapingana na sheria ya Mussa.

Katika suala la talaka tunakuta uhuru ‘‘usio na mipaka’’ uliotolewa na Taurat kwa mume ambaye anaruhusiwa kumwacha mkewe hata kama ataona kuwa huyo mkewe ana jambo la ‘‘kumtia aibu’’ mume. Au hata kama huyo mume atakuwa na ‘‘hisia’’ za kumchukia mkewe. Wakati ambapo Injili yenyewe kana kwamba inapinga talaka isipokuwa katika hali ya usaliti (uzinzi). Ama katika upande wa kisasi, tunaona mkabala huu, Taurati inasisitiza kulipiza kisasi na kutaka damu ya muuaji nayo imwagwe na kulipiza kila baya kwa baya mfano wake. Issa amefundisha wajibu wa kutolipiza ubaya na kuusamehe.

Tukitazama neno kwa neno baina ya misingi hii, inabainaka kwetu ya kuwa, kana kwamba Ukristo umetengua sharia zilizopita. Lakini kama tutazama kwa kina zaidi, tutaona kuna pande mbili au daraja mbili zitokanazo na kanuni moja ya milele. Ya kwanza yake ni uadilifu na ya pili ni upendo. Kwani uadilifu unamlazimisha yule anayetaka kuitumia haki yake asivuke mipaka fulani ya kibinadamu. Ama yule anayetaka kusamehe haki yake kutokana na msukumo wa ukarimu na kutuliza nafsi, huyo hana shida.

Na kwa ajili hiyo tunaona njia zote mbili, ile ya Agano la Kale na ile ya Agano jipya zenyewe zinakamilishana au zinabadilishana. Au hakika mambo yalivyo, hakuna pa kukimbilia na kuhepa kukiri kuwa haitakikani kila njia katika njia mbili hizo itawale peke yake bila mwenzake, ila kwa jamii ndogo ya wanadamu, au ndani ya kipindi fulani katika historia. Kwa hiyo, kanuni sahihi ya tabia njema ndiyo inayoviunganisha vitabu viwili hivyo vitakatifu kwa pamoja. Kiasi ambacho kila kimojawapo kimejumuisha sehemu moja ya sehemu mbili hizo. Na kuacha sehemu iliyobaki ikiwa imejificha kwa kiasi fulani. Na kwa hakika Quran Tukufu imetawalia kuitangaza kanuni hii kwa ukamilifu na kuitilia umuhimu wa kila namna kuweka wazi pande zake hizi mbili na kudhihirisha thamani ya kila upande kwa dhati yake nayo inasema: *((Na mkilipiza, basi lipizeni sawa na vile mlivyoonewa. Na kama mkisubiri (msilipize) hakika huo ni ubora kwa hao wanaosubiri. Na subiri. Na kusubiri kwako kusiwe ila kwa ajili ya Mwenyezi Mungu* tu:...)) An-Nahl 126 – 127. Haya ndio yanayohusiana na kisasi na kusamehe.

Ama kuhusu talaka inatakikana tupitie kurasa za Quran Tukufu ili ibainike kwetu viunzi ambavyo ni lazima kuvivuka kabla ya kufikiria kuviangusha. *((… Na kaeni nao kwa wema; na kama mkiwaacha basi (msiwaache) kwani huwenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake.))* An-Nisaa 19. *((Na kama mkijua kuwa kuna ugomvi baina ya mke na mume basi pelekeni mwamuzi mmoja katika jamaa za mwanamume na mmoja katika jamaa za mwanamke. Kama wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa habari za siri na habari za dhahiri.))* An-Nisaa 35. *((… basi si vibaya kwao wakitengeneza baina yao sulhu (njema wakastahmiliana vivyo hivyo bila kuachana); maana sulhu ni kitu bora…))* An-Nisaa 128. Na juhudi zinazopaswa kufanywa ili kuleta mwafaka. *((Na wanawake walioachwa wangoje (wasiolewe) mpaka tahara tatu ziishe. Wala haiwajuzii kuficha (mimba) aliyoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini*

*Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya sulhu. Nao (wanawake) wanayo haki kwa sharia (kufanyiwa na waume zao) kama ile haki iliyo juu yao kuwafanyia waume zao. Na wanaume wana daraja Zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu (na) mwenye hikima. Talaka (unazoweza kumrejea mwanamke) ni (zile zilizotolewa) mara mbili (za kwanza). Kisha ni kumweka kwa wema au kumwacha kwa ihsani. (Wala usiweze kumrejea tena mpaka aolewe na mume mwengine maadam umetimiza mara tatu katika kumwacha ukimrejea). Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanamume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke. Hii ndio mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiiruke. Na wataoiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhalimu (wa nafsi zao)*. Al-Baqarah 228 – 229.

*((Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu Mwenyezi Mungu)! Mtakapotoa talaka kwa wanawake (mtakapowaacha) toeni talaka katika wakati wa eda zao. (Yaani waacheni wakati wa tahara zao ambazo katika tahara hizo hamkuwahi bado kuwaingilia. Huna ruhusa kumwacha saa utakayo tu). Na fanyeni hisabu ya (siku za) eda, (zisije zikaisha kabla hamjawarejea). Na mcheni Mwenyezi Mungu Mwenyezi Mungu, Mola wenu. Msiwatoe katika nyumba zao wala wasitoke wenyewe. (Mwanamke akiwachwa asitoke katika nyumba hiyo; akae papo hapo kwa kulishwa na kuvishwa mpaka eda iishe); ila wakifanya jambo la ufasiki ulio wazi, (hapo ndio wanaweza kutolewa). Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anayeiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu basi amejidhulumu nafsi yake. Hujui (sababu ya kuamrishwa haya): labda Mwenyezi Mungu atatokezesha jambo jingine baada ya haya (yaani jambo la kupatana). Basi wanapofikia muda wao, ima (warejeeni) muwaweke kwa wema, au farikianeni nao kwa wema; na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu. Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anavyoagizwa yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Na anayemwogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) humtengenezea njia ya kuokoka (katika kila balaa)).* At-Talaq 1 – 2. Na atakayerejea na kuacha maamuzi yake ya awali basi tendo hili la kurejea linamletea msamaha. *((Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao, (muda wao) ni kungojewa miezi minne. Na kama wakirejea (wakatangamana na wake zao) basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa*

*kurehemu.))* Al-Baqarah 226. Na kwa kuzingatia kwamba talaka ni ‘‘Ni halali inayochukiwa na Mwenyezi Mungu’’ kwa hiyo talaka si tendo la halali bila mipaka au linalotolewa bila kujali.

Na hivi hivi ndivyo Quran inavyoweka wazi, kuyaunganisha na kuyapatanisha matendo ya mitume. Na tunaitikadi kuwa katika huku kumpwekesha Mwenyezi Mungu, ambako katika wigo wake inakubali sheria moja yenye madaraja tofauti tofauti katika matendo ya heri – ni sababu muhimu yenye mchango mkubwa – na kwa sababu hiyo, wito wa Uislamu umeweza kuenea kwa watu wa kada nyingi. Na kwa kupitia sababu hiyo umeweza kukusanya fikra, mielekeo na tabia mbalimbali. Uislamu haukubali pamoja naye kuwa na misimamo mikali ya kujitenga bila kusamehe na uvumilivu. Wala kupuuzia bila mipaka. Na kwa kuweka kwetu wazi njia hii ya Uislamu ya kupatanaisha, tunakuwa kwa wakati huo huo tumeshadhihirisha maudhui za Quran katika wito wake na sharia zake.

Lakini Quran hasimami hapa tu, kwani yenyewe ina ujumbe mwingine nao ni kutimiliza na kukamilisha nyumba ya Mwenyezi Mungu iliyojengwa na Mitume na Manabii amani iwe juu yao katika zama zote zilizopita. Mtume rehema na Amani ziwe juu yake anasema: ‘‘Kwa hakika nimetumwa kuja kukamilisha tabia njema.’’ na ‘‘Na mfano wangu na mfano wa Mitume wengine ni sawa na mtu aliyejenga nyumba…’’ Na Quran inasema: *((Hakika hii Quran inaongoza katika njia iliyonyooka kabisa…))* Bani Israili 9.

Ni kipi kipya na cha kimaendeleo katika mafundisho ya tabia njema ya Kiqurani?..

**1- Katika sekta ya ubora wa mtu binafsi.**

Tunapata kanuni mpya na msingi mpya. Na hiyo kanuni mpya nayo ni kuiharamisha pombe na kumaliza vyanzo vyake, kwa kuzuia kutumia kinywaji chochote kinacholevya.

Na ama msingi mpya nao ni ‘‘nia’’ kwa kuizingatia kuwa hiyo nia ndio kiini cha matendo ya tabia njema. Musa alikuwa anawapa habari njena watu wake ya kupata ardhi ya ahadi, kuwashinda maadui, Baraka na raha katika kila jambo la duniani. Na Masihi akaja kufungua Agano Jipya na kuthibitisha kuwa neema na furaha zilizoahidiwa sio katika dunia hii bali zenyewe ni za ufalme wa mbinguni. Na hatimaye Quran Tukufu inakusanya njia ya kujenga ahadi mbili hizo na kuzipatanisha. Kwa kuzingatia kuwa, lengo si ufalme wa mbingu

tu wala si starehe za duniani tu. Bali lengo ni la juu zaidi ya hayo yote. Nalo ni kupata heri ya moja kwa moja, yaani kutafuta dhati ya Allah Mtukufu, ambaye ni lazima kumuweka moyoni wakati wa kutekeleza matendo ya kibinadamu ya kutii amri zake: *((… Na mali yoyote mtakayoitoa ni (faida) kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Na mali yoyote mtakayoitoa mtarudishiwa kamili (thawabu zake) wala hamtadhulumiwa.)) Al-Baqarah 272. ((Na hali ya kuwa hakuna yeyote aliyemfanyia ihsani ili awe anamlipa. Isipokuwa (anafanya haya) kwa kutaka radhi ya Mola wake Mtukufu.))* Al-Layl 19 – 20.

**2- Ubora katika mahusiano baina ya watu:**

Kwa sheria za Torati na sheria za Injili mti wa tabia njema ulisimama na kutoa matawi na majani yake. Ama kwa sheria za Quran ndipo mti huu unapotoa maua na kuleta matunda yake. Kwa hakika Quran imeleta sura mpya iliyo nzuri mno ambayo tunaweza tukaiita Ustaarabu wa kitabia njema: kwa hakika wenyewe ni uboreshaji wa kiufundi wa kweli katika adabu na vionjo vya kijamii na kuwa na heshima katika muonekano.[1]

**3- , 4 – Fadhila za jamii na Fadhila za Kijumla**

Katika kanuni za kitabia njema ndani ya dini ya wafuasi wa Mussa kuna kizuizi kirefu baina ya Waisraeli na wasiokuwa Waisraeli. Kwani kila heri inayoelekezwa kwa Muisraeli, endapo haitokuwa ya watu wake tu, basi inatakikana hiyo heri isivuke mipaka ya nchi yake wala isimjumuishe mgeni anayeishi nchini kwake. Kwa mfano kukopesha kwa riba (Kumbukumbu la Torati 22:20). Kumtaka mgeni atoe haki (Kumbukumbu la Torati 15:3). Kutomtia utumwani nduguyo (Walawi 25:39). Kutomsaliti (Walawi 25:43 – 45). Na kwa upande wa kushikamana kijamii na kuwa na hisia za majukumu ya kijamii. (Kumbukumbu la Torati 6:7, 13:5 na Walawi 20:22).

Ama kanuni za kitabia njema katika dini ya Kikristo ina fadhila kubwa kwa kuondoa kizuizi hiki. ((Je, mtapata tuzo gani kwa kuwapenda tu wale wanaowapenda nyinyi? Hakuna! …… Kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je, mmefanya kitu kisicho cha kawaida?...)) Matayo 5:46 – 47. Hata hivyo huo ubora wa tabia njema za Kikristo kama zinavyowasilishwa na Injili mara nyingi

[1] Maamkizi (An-Nisaa 86), kuingia katika nyumba (An-Nur 27 – 28), kuomba ruhusa (An-Nur 58 – 59), kula kwa jamaa wa karibu (An-Nur 61 – 62), kupunguza sauti (Al-Hujurat: 2 – 5), Kunong`ona (Al-Mujadila 8 – 11), dhana (Al-Hujurat 12), kuinamisha macho (An-Nur 31), kupunguza nguo (An-Nur 60), namna ya kuongea: (Al-Ahzab 32 – 33), kuingia nyumba za Mtume: (Al-Ahzab 53), kujiheshimu: (Al-Ahzab 59).

zinahusiana zaidi na mahusiano baina ya watu binafsi kuliko zinavyojulisha roho ya umoja kuwa ndio sifa ya msingi. Lakini upendo wa Kikristo kwa kupanuka kwake nje ya mipaka ya majimbo, na hamu yake ya kuwafikia wanadamu wote, kwa kweli umefanya vizuri kwa kule kubatilisha tabia za kibaguzi na kuzibadili na kuwa za kiudugu wa dunia nzima.

Lakini Quran, yenyewe ndio iliyoelekeza wazi wazi huko kuunganisha baina ya fadhila za kijumla na fadhila za kijamii. Kwani Quran inathibitisha kuwa nje ya undugu kwa ajili ya Allah kuna undugu kwa ajili ya Adam. *((Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu, (msipuuze jambo la kupatanisha) ili mrehemewe. Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): Jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni Mwislamu. (Na kufanya haya ni uasi) Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao)).* Al-Hujurat 10 – 11. Na imehimiza mapenzi na wema vitawale licha ya tofauti za hisia za kidini. *((Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia ihsani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakukufukuzeni katika nchi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu.))* Al-Mumtahinah 8.

Na kufanya uadilifu hata pamoja na maadui. *((… Wala kule kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika msikiti uliotukuzwa (wa Makka) kusiwapelekeeni kuwafanyia jeuri (ili kuwalipa jeuri yao; msifanye). Na saidianeni katika wema na taqwa, wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.))* Al-Maidah 2. Na kuharamisha riba kwa wote. Na kwamba mcha Mungu anakuwa hivyo hivyo sawa akiwa ndani au nje ya jamii yake. *((Na katika waliopewa Kitabu kuna ambao ukiwapa amana ya mrundi wa mali watakurudishia. Na katika wao kuna ambao ukiweka kwao amana ya dinari moja (tu hivi) hawakurudishii, isipokuwa uendelee kuwasimamia (kuwadai). Haya ni kwa sababu walisema: ''Hapana njia juu yetu (ya wasiokuwa dini moja na sisi).'' Na wanasema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu, hali wanajua (kuwa sivyo hivyo). Sivyo hivyo (wanavyosema. Lakini) anayetekeleza ahadi yake na akajilinda (na dhambi, atakuwa kipenzi cha Mwenyezi Mungu,) na Mwenyezi Mungu huwapenda wajilindao (na madhambi)).* Aalii Imran 75 – 76.

Na kutilia umuhimu suala la kuwakomboa mateka wa Kiislamu: *((Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na (katika kuwaokoa) wale walio dhaifu – katika wanaume na wanawake na watoto – ambao husema: ''Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe tuna mlinzi anayetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka kwako.''))* An-Nisaa 75.

Na kuwakomboa watumwa kwa namna ya kiujumla: *((Sadaka hupewa (watu hawa): - Mafakiri na Maskini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu) na katika kuwapa uungwana watumwa na katika kuwasaidia wenye deni na katika (kutengeneza) mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na katika (kupewa) wasafiri (waliharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.))* At-Tawba 60.

*((Sio wema (tu huo peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (katika kusali. Yako na mema mengine). Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na wanawapa mali – juu ya kuwa wanayapenda – jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (waliharibikiwa) na waombao na katika (kuwakomboa) watumwa na wakawa wanasimimamisha swala na kutoa zaka, na watekelezao ahadi zao wanapoahidiwa, na wavumiliao katika shida na dhara na (katika) wakati wa vita; hao ndio waliosadikisha (Uislamu wao), na hao ndio wamchao Mungu.))* Al-Baqarah 177. *((Kuukata mlima huo) ni kumpa mtumwa uungwana))*. Al-Balad 13.

Na hivi hivi ndivyo fikra ya ubora wa kiujumla iliyotajwa na Injili, ilivyoboreshwa na kuunganika zaidi na zaidi kila inapopanuka na kujumuisha sekta mbalimbali za kimaisha. Lakini, je maana ya hiyo ni kuwa jamii ya Kiislamu inajiachia sana katika viunganisho vyake vya ndani kwa ndani hadi inapotelea katika wigo mpana wa jamii kuu ya kibinadamu? Jibu ni kinyume chake, kwani katika Uislamu kuna misingi miwili inayothibitisha nafasi ya Uislamu kama kundi linalojipambanua na lenye kushikamana.

**Mosi**: unawaita waumini wawe kundi moja wasigawanyike – bila ya farka wala mpasuko – wazunguke kando ya msingi wao na kando ya kiongozi wao. *((Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu. (Zamani) mlikuwa maadui; naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo, kwa neema yake,*

*mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto wa (Jahannam), naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kuongoka.))* Aali Imran 103.

*((Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hiyo ndio kheri, nayo ina matokeo bora kabisa.))* An-Nisaa 59.

*((Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala msizozane (msigombane), msije mkaharibikiwa na kupotea nguvu zenu, na vumilieni (msitahamiliane). Bila shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaovumilia.))* Al-Anfal 46.

**Pili**: ni kwa Waislamu wote kudumisha tabia ya kutoyaachia maovu yatawale katika jamii yao: *((Na iogopeni adhabu ya (Mwenyezi Mungu ya hapa duniani) ambayo haitawasibu peke yao wale waliodhulumu nafsi zao miongoni mwenu (bali itawasibu hata walionyamaza wasiwakataze, bali na wengine pia); na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.))* Al-Anfal 25. Na ulazima wa kuhusiana juu ya haki na matendo mema. *((Isipokuwa wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana (kufuata) haki na wakausiana (kushikamana) na subira (kustahamiliana)).* Asr 3. *((Kisha awe miongoni mwa walioamini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.))* Al-Balad 17. Na kusaidiana katika mema na kumcha Mungu. *((... Na saidianeni katika wema na taqwa, wala msisaidiane katika dhambi na uadui...))* Al-Maidah 2.

Na mshikamano ndio kipimo cha jamii ya Waislamu wa mwanzo na ambao wameitwa umma bora uliotolewa kwa ajili ya watu. *((Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) – mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu…))* Aali Imran 110.

Pamoja na hayo, imedhihiri kwa baadhi ya Mustashirikina (wasomi wa kimagharibi waliusoma Uislamu) kuupa Uislamu taswira ya kuwa wenyewe ni dini yenye hisia ya mtu mmoja mmoja bila kipingamizi). Na kwamba Uislamu hata siku moja haujapatapo kutambua mafungamano ya kushikamana. Hadi umefikia upeo kuwa hao Mustashirikina wanaona kuwa yale matendo ya Waislamu ya pamoja kama vile swala za jamaa, kisimamo cha Arafa, swala ya

Idi, yote hayo ni matendo ya mtu mmoja mmoja yanayotekelezwa wakati mmoja bila ya kuwa na tabia ya kuwa yenyewe ni mahafali au makutano yenye mwelekeo maalumu au yaliyopangwa. Na kauli hii haina ukweli wowote, kwa ushahidi wa hicho tulichokitangulia kukiweka wazi... Ama katika swala tunawaona Waislamu wakiwa wamejipanga mistari, wote hao wanaomba kwa ajili ya jamii yote pale wanaposema: *((Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada. Tuongoze njia iliyonyooka..))* Al-Fatiha 5 – 6. Pia wanawaombea waja wote wema wa Mwenyezi Mungu. Swala na Zaka ni wajibu na ni mapacha wanaosimama kama hoja zenye nguvu kubwa zinazothibitisha roho ya mshikamano katika Uislamu.

**5- Fadhila katika miamala ya Kimataifa na baina ya dini mbalimbali**

Hii ni sura mpya ya kila aina ya upya katika tabia njema za Kiislamu. Kwani Uyahudi na Ukristo wakati wa kuanzishwa kwao hazikupewa nafasi ya kuwa na mahusiano na mataifa adui. Wakati ambapo Mtume rehema na Amani ziwe juu yake alikuwa na uhusiano wa daima na mataifa na dini mbalimbali. Wakati mwingine wakiwa na uhusiano wa amani na wakati mwingine wakiwa na uhusiano wa kiuadui. Katika kipindi cha miaka kumi. Kwa sifa yake ya kuwa mwanasiasa na kiongozi, na kwa upande wake wa kuwa kiongozi wa kiroho na tabia njema. Na miongoni mwa misingi ya miamala hiyo ni kuwa vita havitaruhusiwa kisheria ila kwa ajili ya kuondoa uadui. *((Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni) Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.))* Al-Baqarah 190. Na vita lazima vikome punde tu vinapoisha: *((Na kama (hao maadui) wakielekea katika amani, nawe pia ielekee na mtegemee Mwenyezi Mungu…))* Al-Anfal 61.

Pia kuna msingi wa kuheshimu mikataba waliyowekeana na maadui. *((Na timizeni ahadi mnazozitoa kwa jina la Mwenyezi Mungu mnapoahaidi; wala msivunje hizo ahadi baada ya kuzithubutisha, hali mumekwisha mfanya Mwenyezi Mungu kuwa shahidi wenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua (yote) mnayoyafanya. Wala msiwe kama yule mwanamke aliyeukata uzi wake vipande vipande baada ya (kuusokota) kuwa mgumu. Mnavifanya viapo vyenu njia ya kudanganyana baina yenu. Kwa ajili ya kundi moja la watu kuwa na nguvu zaidi kuliko kundi la watu wengine (ndio mnawaacha hao wasio na nguvu mliopeana ahadi nao! Msifanye hivyo…))*. An-Nahl 91 – 92.

Na lau kama adui ataanza kuvunja makubaliano yake, haifai kumshambulia papo hapo. Kwa hakika, kwanza kabisa anapaswa kumtangazia kwa njia za wazi wazi kwamba mkataba wake na sisi umevunjika. *((Na kama mkiogopa khiana kwa watu (mliofanya nao ahadi) basi watupie (ahadi yao) kwa usawa; hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wafanyao khiana.))* Al-Anfal 58. Haya, ukiachilia mbali na misingi iliyowekwa na hadithi za Mtume rehema na Amani ziwe juu yake.

## Sura ya tatu
## Uzuri na upande wa fasihi

Katika kina cha nafsi ya mwanadamu – kama tulivyosema – kunapatikana maono ya ndani kwa ndani yanayotofautisha baina ya haki na batili, heri na shari, vyovyote zitakavyotofautiana sura zake, lakini kwa sharti la kwamba huyo mwanadamu aone kwa uwazi na kwa ubongo safi. Kwani akili iliyokomaa na nafsi iliyojiandaa, haihitaji zaidi ya hayo ili kujiunga na wito mpya muda wa kuwa linapatikana katika wito huo sharti lenye pande mbili, nalo ni mafunzo ya kweli na wito wa kuyaendea mambo mazuri. Na hivyo hivyo ndivyo Hercules Mfalme[1] wa Warumi, licha ya kutokujua kwake lugha ya Kiarabu, alivyoweza kuamua kuwa ujumbe wa Muhammadi ni wa kweli. Na hivyo ni kwa kutegemea baadhi ya masharti ya kitabia njema alizokuwa akiziitakidi kuwa zenyewe ni za lazima na zinatosha kuthibitisha kuwa ujumbe huu ni wa Mungu.

Lakini mambo hayapo hivyo kwa watu wengi wa kawaida. Kwani kile kinachowavutia wao katika vile wanavyopewa ni ule uzuri wa umbo la nje nje na sio ubora wa maudhui yaliyomo. Kwa hiyo kitu kipya chochote kile kinachovaa vazi linaloonesha uduni na lisilovutia, linawafanya wao wakikatae kitu hicho na kukikimbia. Kwa sababu wao wanapupa ya kutoa maamuzi juu ya vitu kwa mujibu wa kutazama muonekano wake wa nje nje tu kabla ya kuchunguza maudhui na kiini. Na kwa hapa ndipo tunapotambua kima na thamani ya msaada wa kweli unaoweza kutolewa na fasihi kwenda kwa sayansi na hekima pale viwili hivyo vinapotetea haki na ubora.

Na wito wa Kiislamu kwa upande wa kifasihi unajidai kwa kuwa na ukamilifu usio na makandokando ya aina yoyote ile. Kwa muonekano wake na undani wake unashibisha haja ya mwenye kukifahamu Kiarabu. Na Quran – ndio inayobeba ujumbe huu – ilikuwa na itaendelea kuwa mfano na kiigizo kinachoshinda katika fasihi ya Kiarabu. Na kama tutatazama mtazamo usio na upendeleo katika sifa zake za kifasihi tunaweza kusema kuwa yenyewe ndio inazingatiwa kuwa kiigizo chema kwa kile kinachoweza kuitwa fasihi kwa namna ya kiujumla. Katika zama za dhahabu za lugha ya Kiarabu. Punde tu uteremsho huu wa hekima ulipoteremka haukupita muda mrefu ukazishinda hamasa zote za mashairi na nathari. Na ‘‘*mualaqaatu’’* ambayo ni mashairi bora na maarufu kabisa ambayo yaliyotundikwa vifuani mwa Waarabu na katika

---

[1] Tazama Al-Bukhaariyu, Kitabu Al-Jihadi, mlango wa 101, pia tazama katika B. Saint Hilaire katika kitabu chake ‘‘Muhammad na Quran’’ uk. 150 – 156.

milango ya Kaaba yaliteremshwa kutoka katika milango ya Kaaba na mioyoni. Na masikio yote yakaelekea upande wa muujiza huu mpya katika lugha ya Kiarabu.

Lugha ya Quran ni maada (material) ya sauti inayokuweka mbali na ulaini wa lugha ya mjini na ugumu wa lugha ya watu wa majangwani. Na yenyewe inajumuisha – katika mshikamano madhubuti – baina ya udhaifu wa lugha ya upande wa kwanza na ukomavu wa lugha ya upande wa pili. Na kuhakikisha kupatikana kwa uhondo unaokusudiwa. Yote hayo kwa fadhila za kupatanisha mziki mwororo wenye ubunifu baina ya viwili hivyo. Hakika yake ni mpangilio wa silabi na maneno katika mfumo ambao unashikamana sana kuliko lugha ya nathari. Na wenye kupungua kidogo katika mshikamano kuliko mashairi. Ndani ya aya moja unapata aina tofauti tofauti ili kuvutia uchangamfu wa msikilizaji. Na kuna vina vya mfanano mwishoni mwa aya zake. Yote hayo ili kusiwe na dosari katika kengere na mirindimo ya jumla ya kila sehemu ya kusimamia sura zake. Ama maneno yake yameteuliwa kutoka katika maneno mashuhuri. Pasi na kuporomoka hadi kufikia kiwango duni. Pia yamechaguliwa kutoka katika maneno matukufu ambayo hayasifiki kuwa ni maneno ya ajabu ajabu, isipokuwa kwa nadra sana. Na Quran inasifika kwa kuwa na ufupisho wa ajabu katika sentensi zake na umakini wa hali ya juu katika maana. Na uwazi wenye kumchukua mtu. Pamoja na kuwa na maana ya kina sana, kukubali hali zote, inasihi sana, kutoa nuru kila pande kama pande za kipande cha almasi inayomeremeta. Kwa hakika maneno yake ni kweli iliyothibitika kuwa watu wote licha ya tofauti zao za kielimu na kifikra wote wanakutana katika kuifahamu Quran. Kana kwamba kila ibara ndani ya Quran imeelezwa kwa maelezo yanayolingana na akili ya kila mmoja wao… Na yote haya yapo katika mada ambazo hazijaguswa na fasihi ya Jahiliya (zama za kabla ya Mtume Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake) kwa kiasi ambacho ni haki yetu kuthibitisha, kwa upande wa lugha peke yake, kuwa; kudhihiri kwa Quran kulikuwa ni kuumbwa kwa lugha mpya, mtindo mpya na muundo mpya.

Ama yale yanayoonekana kuwa ni zaidi ya uwezo wa mwanadamu, kwa mtindo na muundo wa Quran, kwa kweli hayo ni kwa vile hayakubali kanuni za kisaikolojia. Kanuni ambazo kwa muktadha wake tunaona kuwa akili na hisia havifanyikazi isipokuwa kwa kubadilishana tu, tena kwa uwiano wa kukinzana. Wakati ambapo katika Quran hatuoni ila kusaidiana kwa daima baina ya viwili hivyo katika kila mada. Tunaona maneno yakitembea kwa nguvu, na wakati huo huo yanajumuisha baina ya mafunzo, kutosheleza na kuathiri. Na kuvigawia

moyo na akili mafungu yao yanayostahiki. Juu ya hayo, sentensi zake daima zinaendelea kutunza haiba yake ya kishindo, na utukufu wake wa nguvu usio na ile hali ya kupanda na kushuka wala kutetereka.

Na Mwarabu asilia ambaye katika damu yake kunapita wingi wa kuijua lugha yake, alikuwa anafahamu kwa uwerevu wake na maumbile yake. Na alikuwa anahisi kuwa Quran imekuja kutoka mbinguni, inapenya nyoyoni na kuyastaajabisha macho. Hata makafiri wa zama za Mtume rehema na Amani ziwe juu yake, walitambua taathira hii ya Quran. Ndipo wakatofautiana katika kuitafutia fasili na namna ya kuitia dosari. Hadi wakafikia daraja la kuiita kuwa yenyewe ni uchawi. Kwani tunaona katika Quran Takatifu hali fulani hivi, ya lahaja mojo hivi, ya kipekee haitokani katika moyo wa mwanadamu bali isipokuwa yenyewe ni ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ama hadithi za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kwa hakika zenyewe ni maarufu kwa lugha yake ya kisanaa yenye madaha ya hali ya juu. Lakini licha ya hivyo inatofautiana na matini ya Quran kwa tofauti kubwa mno.

Inatakikana katika sura hii tuzingatie na kuwekeza baadhi ya juhudi zetu juu ya nukta ambayo Mustashrikina wote wameghafilika nayo (wameisahau). Na zaidi ya hao pia kuna baadhi ya Waislamu waliyoisahau. Nayo ni ile njia ya Quran Tukufu ya kushughulikia zaidi ya mada moja katika sura moja.

Baadhi ya Mustashrikina kwa mtazamo wao wa juu juu wameliona hilo na kudai kuwa katika Quran hakuna kushikamana wala muunganiko asili baina ya mada zinazoshughulikiwa na sura moja. Na zaidi ya hayo hawajaiona Quran vingine isipokuwa yenyewe ni mtawanyiko wa fikra mbalimbali zilizoshughulikiwa kwa njia isiyo na nidhamu nzuri na bila ya kiunganishi chohote cha kimantiki baina ya fikra hizo. Wakati ambapo baadhi ya wengine wameonelea kuwa sababu ya huku kutawanyika kunakodaiwa ni ile haja ya kupunguza uchovu unaotokana na udhaifu wa muundo na mtindo. Pia ni kutokana na huzuni inayotokana na kurudiwa rudiwa kwa toni jambo ambalo linakataana na ukamilifu wa ubora katika muundo na mtindo wa Kiarabu.

Pia kuna kundi la tatu lililoona kuwa umoja wa kifasihi kwa kila sura ni aina fulani ya kufidia upungufu wa msingi katika umoja wa maana. Wakati ambapo kundi lingine linalojumuisha Mustashrikina wengi nalo limeona – likiwa linajaribu kumtakasa Mtume rehema na Amani ziwe juu yaje – kuwa kwa hakika dosari hii sababu yake ni Maswahaba walioikusanya Quran na

wakafanya hili kosa la kuikoroga pale walipokusanya vifungu vyake na kuipanga kwa umbo la kuwa na sura.

Na haki ni kuwa, kwa hakika maelezo yao yote hayafai kuyachukua. Kwa kuwa hadithi safi na mapokezi sahihi yanakubaliana kuwa sura zilikuwa na umbo, utaratibu na mpangilio huu huu ambao tunaousoma leo hii tangu enzi za uhai wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

Na pale tunapotaka kupima na kukadiria uzuri wa bango lililochorwa haitakikani kuyafunga macho yetu katika sehemu finyu tu ya bango hilo. Bali yatupasa turejea nyuma kidogo ili sehemu za kuona zipanuke na kwa hiyo tutatazama mtazamo kamilifu. Kwa mfano wa mtazamo huu ndio inatakikakana kuisoma/kuitafiti kila sura ili tupime pande zake za hakika. Kwa hakika wakati uliopita tulipokuwa tunasoma chuo cha Al-Azhar tulifanya zoezi la kuifanyiakazi kanuni hii katika utafiti wa sura moja ya Madina (nayo ni suratul Baqarah) na sura mbili za Makka (nazo ni Yunus na Hud) na kwa hakika kazi hii ilikuwa ni kazi katika silabasi ya programu ya masomo.

Na kwa uhalisia ni kuwa sisi tulipata zaidi ya kile tulichokuwa tunakitafuta katika utafiti wetu. Kwa hakika ulituwekea wazi kile kilichoamsha mshutuko wetu nacho ni kuwa sura hizi zina mipango ya hakika ya wazi na iliyoainishwa. Mipango hiyo inaundwa na dibaju, kiini (mada/maudhui) na hitimisho.

Na kama tutazichukua katika mazingatio yetu tarehe zisizodhibitika na mtawanyiko uliokuwa mkubwa mno wa namna aya zilivyoteremka. Na tukaona kuwa kuteremka kwa ufunuo kwa ujumla wake kulikuwa kunafungamana na mazingira na matukio maalumu. Kwa hakika, hayo yanatufanya tujiulize kuhusu wakati ambao ndani ya wakati huo ulitimia mchakato wa kuipanga kila sura kwa umbo la kuwa kitu kimoja kinachojitegemea. Na kujiuliza huku kumetuweka mbele ya nukta ya kutahayarisha.

Ni sawa sawa kama tutachukulia kuwa mpangilio huu ulikuwa kabla ya kukamilika kwa kuteremka Quran au baada ya kukamilika kwake. Kwa hakika jambo lililokuwa likitarajiwa ni ima kuipanga Quran kwa kufuata mpangilio wa tarehe za kuteremka aya au kwa kufuata mpangilio mwepesi wa kimantiki kwa mujibu wa muingiliano wa mada. Isipokuwa kwa hakika jambo linaloonekana ni kuwa sura za Quran na mada zake zipo aina mbalimbali na haziingii katika mpangilio wowote katika mipangilio miwili iliyotangulia.

Jambo ambalo lilitufanya sisi kuweka uzito katika uwepo wa muundo au mpango maalumu uliochangamani sana. Unaoweza kuwa uliwekwa wakati uliopita kabla ya kuteremka kwa Quran. Lakini haraka haraka tukaelekea kuiacha hii nadharia tete kwa sababu ya upeo wa kutowezekana kwake kabisa kabisa. Nadharia hio tete inajumuisha kuweka taswira ya kuwa kuliwekwa mfumo uliotangulia ulio kama huu. Na kwa mfumo huo ndio zinapangwa vizuri aya za Quran baina ya vifungu vyake vipya ambavyo vitahitaji kuvitupia au kuvidhihirisha katika mzunguko wa miaka ishirini na mitatu. Tena kwa namna ya kuafikiana na kunasibiana mambo chungu nzima, matukio mengi na mazingira mbalimbali yanayopelekea kuidhihirisha habari hiyo. Hayo ni mambo ambayo hayawezekani kuyatarajia au kuyatabiri kutokea kwake au hata wakati wa kutokea kwake. Isipokuwa sunna za Mtume rehema na Amani ziwe juu yake zinatuthibitishia kuwa zenyewe zinaiunga mkono nadharia hii tete na ya ajabu. Kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake, punde tu unapoteremka ufunuo kwake yeye – alikuwa anaamrisha kwa kila kipande, kiwe kidogo au kikubwa, katika ufunuo huo – kiwekwe katika sura yake ambayo nayo ilikuwa bado haijakamilika. Na katika sehemu iliyoanishwa ndani ya sura hiyo. Na kwa sehemu ya nambari kwa mujibu wa aya zake. Na katika mpangilio ambao siku zote haukuwa mpangilio wa kitarehe. Na kwa kuiweka au kuziweka aya katika sehemu hii au ile, basi ndio inabakia hapo hapo milele. Bila ya kutokezewa na mabadiliko, au masahihisho, au marekebisho au kuwekewa viunganishi vya aina yoyote ile.

Kutokana na hili tunasema, hakika mambo yalivyo, kwa hakika hapana budi kulikuwa na muundo wa kila sura. Na zaidi ya uwepo wa muundo na mpango wa Quran katika ujumla wake. Kwa muktadha wake, kila ufunuo mpya ulikuwa unawekwa sehemu yake sahihi baina ya aya za surah hii au ile miongoni mwa sura zilizokuwa wazi.

Kana kwamba aya za Quran zilikuwa ni kipande kimoja kinachojitegemea kilichowekewa nambari katika mjengo uliosimama katika sehemu fulani. Na ikawa inatakikana kurudia kulijenga tena katika sehemu nyingine kwa umbo lilelile lililotangulia. Na kama si hivyo, inawezekanaje kuelezea mpangilio wake huo wa papo kwa papo unaoenda kwa njia maalumu kwa wakati mmoja, tena katika mambo yanayofungamana mara nyingi na sura za Quran, kama hizo kurasa tupu na hizo kurasa zilizotimia zisingekuwa zinazowakilisha umoja uliokamilika kwa muono wa mtunzi? Pia kuna mpango kazi mwingine wenye tabia ya kimuundo na kimtindo. Na kwa muktadha wake

tunaona kuwa vifungu ambavyo vitakuwa jirani vimeandaliwa mapema kwa njia maalumu. Kiasi ambacho vyenyewe kwa venyewe vinaoana na kupatana bila mikwamo wala kugongana.

Hapana shaka ya kuwa njia hii ya Quran haina mfano wake kabisa kabisa. Na kitabu chochote kile miongoni mwa vitabu vya fasihi au cha sekta yeyote ile hakiwezi kuwa – kimetimia kukitunga kwa mfano huu wa kipekee au kuwa kimetungwa katika mazingira kama haya ya kustaajabisha.

Kwa maana nyingine, kama mitikisiko katika mfumo wa kimantiki au dosari za matumizi ya lugha na umbuji (madaha) ndio matokeo ya lazima ya mfano wa mradi huu. Basi hata kama binadamu atajaribu kulitekeleza, kwa sababu ya vile vilivyomo miongoni mwa mkanganyiko wa kutahayarisha na yenye ugumu mno. Je, haitakikani tupate matokeo ya kuwa, kukamilika kwa mpango kazi huu na kuthibitika kwake na namna inayotakikana, lazima kutakuwa ni kutokana na kuingilia kwa nguvu kuu yenye uwezo huo uliopita kiasi wa kusimika kuafikiana huko kwa kimuujiza? Na kama si hivyo, ni nani huyu kiumbe ambaye anaweza kuyaelekeza matukio yaende kikamilifu kwa kuafikiana na huo mpango uliochorwa? Au inawezekanaje tuweze kutoa jengo la fasihi ya hali ya juu katika mkusanyiko wa mambo yanayotokea kwa nasibu tu, na jengo lenyewe ni Quran?

Ikiwa sura za Quran ni matokeo ya mazingira haya, basi kwa mtazamo wetu, umoja wake wa kimantiki na wa kilugha ni muujiza wa miujiza. Na kwa hakika hilo la uwepo wa umoja wa jozi (wenye pande mbili) limeelezwa waziwazi na watu wengi miongoni mwa watu waliobobea katika mada hii. Wakiwemo miongoni mwao Abuu Bakri Naisaboriyyu, Fakhru Diini Al-Raadhiy, Abuu Bakri ibni Al-Arabiy, Burhanddiini Al-Baqaaiyy, na Abuu Is-haqa As-shaatwibiy. Na ili kurejea mada hii kwa baadhi ya vifungu vilivyochaguliwa katika Quran tunaashiria kipitiwe kitabu chetu ‘‘Annabau Al-adhiimu’’.

Ila kwa hakika kupendezwa kwetu kutafikia kilele chake kama tutatambua kuwa hivi vifungu vya aya za Quran vilivyotawanyika. Katika kuteremka kwake vilifuata mpango mwingine unaotofautiana kabisa kabisa na ule mpango ambao tuliuzungumzia katika vifungu vilivyopita. Na hakuna kinachotupasa ila kuviwasilisha kuanzia mwanzo wake mpaka mwisho wake – hatua za kidogo kidogo za huu mpango wa pili ndani ya kipindi cha miaka ishirini na mitatu: tangu kupewa Utume hadi kupewa na Ujumbe, (kuanzia

*((Soma))* katika surat Al-Alaq 1. mpaka *((Simama na uonye viumbe))* katika surat Al-Muddathir 2).

Na kutoka katika wito wa siri mpaka wito wa dhahiri. *((Basi (wewe) yatangaze uliyoamrishwa (wala usijali upinzani wao) na ujitenge mbali na (vitendo vya) hao washirikina.))* Al-Hijri 94. Na kuanzia wito wa Mtume kuwaita ndugu zake *((Na waonye jamaa zako walio karibu nawe))* Ash-Shuaraa 214. Mpaka kuulingania mji wote wa Makka. *((Na Mola wako haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika mji wao mkuu, awasomee aya zetu…))* Al-Qasas 59. Kisha miji ya jirani. *((… Na ili uwaonye (watu wa) Mama wa miji (Makka) na watu waliopembezoni mwake…))* Al-An-am 92. Kisha watu wote. *((Nasi hatukutuma, (hatukukuleta) ila uwe rehema kwa walimwengu (wote))).* Al-Anbiyaa 107. Na kuanzia kusimika kanuni za misingi za Uislamu (katika sura za Makka) mpaka kufikia utekelezaji kivitendo (katika sura za Madina). Na kutoka katika kubughudhi unywaji wa pombe *((Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: ''Katika hivyo mna madhara makuu na (baadhi ya) manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake''…))* mpaka kuiharamisha kwa wazi wazi. *((Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na Kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu; na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu.))* Al-Maidah 90.

Na kutoka katika wito wa kuwa na subira na kuvumilia maudhi. *((Hawaoni wale walioambiwa: ''Izuieni mikono yenu (na kupigana na makafiri mpaka ije amri ya kupigana)? Na sasa simamisheni swala, na toeni zaka (tu)…''))* An Nisaa 77. Mpaka kufikia mapambano ya silaha. *((Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka…))* Al-Baqarah 190.

**Na kwa hapa inatosha tusajili historia mbili zenye upande mkubwa wa umuhimu:**

**Ya kwanza**: historia ya kuanza kwa wito: siku ya pango la Hira na Mtume kupokea ufunuo kwa mara ya kwanza. *((Ambaye amemfundisha (Binadamu ilimu zote hizi) kwa wasita (msaada) wa kalamu; (zilizoandika vitabu, watu wakapata ilimu). Amemfundisha mwanadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui.))* Al-Alaq 4 – 5. Na kuwa yeye atapewa kazi ngumu. *((Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito.))* Muzzammil 5.

**Na historia ya pili**: nayo ni Hija ya kuaga pale Mtume rehema na Amani ziwe juu yake alipotangaza kuwa ujumbe wake umeshatimia, na kazi yake ardhini imeshaisha. *((... Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu ...))* Al-Maidah 3. Na baada ya hapo Mtume rehema na Amani ziwe juu yake hakukaa muda mrefu akakutana na Mola wake.

Kwa hiyo, kwa hakika muendelezo huu ulikuwa unaafikiana na mpango/maandalio ya kimalezi ya kisheria yaliyowekwa katika wakati uliopita. Katika ujumla wake na kwa maelezo yake ya upana. Kwa kumjua mteremshaji wa ufunuo Mtukufu Aliyetukuka. Kama aya hizi zenyewe ndizo ambazo zilikuwa zinafuata wakati wa kuteremka kwake, kwa ule mpango wa kimalezi ulio bora zaidi. Kwa kule kuteremka kwake tu zimebadilika katika utaratibu wake wa kihistoria na kusambaa na kujikusanya kwa umbo lingine lililokuwa ni fremu yenye mipaka maalumu na yenye urefu tofauti tofauti. Kwa kiasi ambacho, mwishoni mwa mgawanyo huu uliokusudiwa, kinadhihiri kitabu kinachosomwa na kinachoundwa na vifungu vilivyokamilika. Kila kifungu katika hivyo kina mfumo wake wa kifasihi na kimantiki. Utamu wake hauna upungufu kuliko ule mpango mkuu wa kimalezi. Na huu ndio mpango wenye pande mbili na ambao haiwezekani ukatokana na moyo wa mwanadamu..

# MLANGO WA TATU

# CHANZO CHA KWELI CHA QURAN

## Utangulizi

Utafiti juu ya chanzo cha kila kitabu unahitaji kwanza utafiti juu ya yale yaliyomo katika kitabu hicho. Ama kwa upande wa Quran, kwa hakika utafiti juu ya chanzo chake unalazimisha kuenda kinyume na kanuni hiyo. Kwa sababu fikra ya kuwa chanzo chake ni Mwenyezi Mungu sio tu ni sehemu ya wito wake bali pia ni sehemu ya msingi katika wito huo. Kwa sababu Quran tangu mwanzo wake mpaka mwisho wake inamuongelea Mtume rehema na Amani ziwe juu yake au inamsimulia yeye, na milele haimuachi aelezee fikra zake binafsi..

Lakini kwa nini tusiyanasibishe maneno ya Quran na fikra zilizomo kwa yule mtu aliyekuja nayo?

Na vipi inawezekana tumfanye mtu huyu awe ni nyenzo tu ya kupokelea. Anayewasilisha kitabu chake kikiwa tayari na kikamilifu kama alivyokipokea kutoka katika chanzo cha nje na kisicho cha kibinadamu?

Katika jambo ambalo halina shaka ndani yake ni kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, naye akiwa anasisitiza hili, hakuwa wa mwanzo kuanzisha kadhia (kesi) ya ufunuo. Bali hakika yeye alikuwa ni mnyenyekevu zaidi kuliko Mussa ambaye amepokea Taurat – kama inavyosema Quran – katika mkutano mubashara baina yake na baina ya Allah Mtukufu Aliyetukuka pale aliposikia maneno ya Allah mwenyewe. Ama kwa mnasaba wa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, kwa hakika Quran ni kauli ya mjumbe wa mbinguni. Mjumbe wa katikati baina yake na baina ya Allah. Na ama kwa yale yasiyokuwa ya tofauti hizi, kwa hakika wawili hao wanaafikiana katika kuyanasibisha kwa Mwenyezi Mungu yale waliyoyapokea.

Na ama wale ambao kimsingi hawapingi ufunuo, basi ni haki yao wasiutekeleze msingi huo katika matukio maalumu ila baada ya kumaliza fursa zote za kawaida za kulielezea tukio hili. Na pindi wanapoungama huko mwishoni kuwa ufunuo huo chanzo chake cha mubashara ni Mwenyezi Mungu. Huku kuungama kunakuwa ndio hatima ya utafiti. Na ndio uamuzi wa kisayansi baada ya kumaliza njia zote za kuikosoa zinazowezekana.

Hebu katika utafiti wetu huu tujiepushe na ile hoja inayotegemea muujiza wa lugha katika Quran. Japo nayo ni hoja ambayo inathibitisha kuwa chanzo cha Quran ni Mwenyezi Mungu. Na tujiulize kama kuna uwezekano wa kuyafasili mawazo yaliyomo ndani ya Qurani kuwa yanatokana na sababu nyingine isiyokuwa ufunuo.

Kiuhalisia kuna chunguzi na tafiti nyingi zilizopitia njia hii katika nyakati zilizopita. Jambo ambalo linaufanya utafiti mpya katika uga huu kuwa ni marudio tu ya maneno yale yale yaliyotangulia. Hata kama yatatofautiana kiumbo na kinjia.

Katika mlango huu tutafuata mpangilio wa nyakati. Hivyo utafiti wetu tutaugawa katika sura mbili, hatua ya Makka na hatua ya Madina mutawaliya.

## Sura ya Kwanza
## Utafiti juu ya chanzo cha Quran katika sura za Makka

Duru za wapagani – Mahunafaa[1] – Maswabai – mambo ya Wakristo na Wayahudi – safari za Mtume rehema na amani ziwe juu yake na vitu alivyovishuhudia – vitu alivyovipitia – fasihi na ngano za kijamii – tafakuri zake za fikra binafsi.

Nadharia tete zilizonyepesi zinajaribu kupata dondoo zote za lazima za kuwezesha kujengwa kwa wito wa Quran katika mazingira finyu ya Hijazi[2] – kama sio eneo la Makkah tu. Na kutokana na mtazamo huu ‘‘Ernest Renan’’ ametuwasilishia katika Makala yake ya kuhusu ‘‘Muhammad na Chanzo cha Uislamu’’ mfano wa kipekee wa maisha ya Waarabu kabla ya Uislamu mnamo karne ya sita AD. Na badala ya kueleza kuwa watu hawa ni washirikina (wapagani) wanaojulikana na dunia nzima, yeye ametuwekea watu wengine kabisa ambao hawajawahi kujua zaidi ya Mungu mmoja. (uk 1070 – 1071). Na akatuchorea jamii iliyo katika kilele cha hamasa ya kidini. Dini zote zimekutana kwa watu hao pamoja na ustaarabu wa aina zote. Na kuongezea kuwa suala la dini ndilo lililokuwa jambo lao linalowashughulisha mno. (uk 1089). Na kwa mlinganyo huu, ujumbe wa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake hauvuki isipokuwa utakuwa ni mwendelezo wa harakati za kidini zilizotawala katika zama zake bila ya yeye kutanguliza jipya lolote lile. (1089). Kwa hakika huyu ‘‘Renan’’ amedhihirisha vionjo vya kifasihi vya hali ya juu vya watu hawa. Na mtazamo wao wa uhalisia na akaghafirika na sifa nyingine zisizompendeza.

Lakini picha halisi ya maisha ya Waarabu katika zama hizo tunaipata ndani ya Quran yenyewe. Na picha hiyo inatofautiana sana na maelezo yao kama tulivyoona hapo mwanzo. Kwa hakika maisha yao yalikuwa ni maisha ya ‘‘kupotea kwa wazi kabisa’’ *((… Na bila shaka kabla ya hapo walikuwa katika upotofu dhahiri.))* Aali Imran 164. Na zama zao ni zama za *((… zama za Ujahili (Ujinga, ukafiri)… ))* Ahzaabu 33. *((… walipotia nyoyoni mwao mori, mori wa ujinga; …))* Al-Fat-h 26. Kwa hakika katika ada zao walikuwa wanalinda baadhi ya athari za dini ya Ibrahimu na Ismaili Amani ziwe juu yao. Kwa mfano Hija. Lakini athari hizi zilikuwa zinachanganyika na makosa pamoja na ufahamu mbaya kwa kiasi kikubwa mno: *((… Wala sio kufanya wema kuingia*

[1] Watu waliokuwa wanajaribu kumwabudu Mungu kwa mila ya Ibrahimu Amani iwe juu yake.
2 Maeneo ya Makka na Madina nchini Saudi Arabia

*majumba kwa nyuma…))* Al-Baqarah 189. *((Na mwishapo kuzitimiliza ibada zenu (za Hija), basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja wazee wenu; bali mtajeni zaidi Mwenyezi Mungu …))* Al-Baqarah 200.

Kama ilivyokuwa hadhira ya soko la Ukadhi la wakati huo, hawakulumbana kwa ajili ya dini bali walilumbana kwa ajili ufahari wa mambo ya kidunia. Katika mashairi yao maarafu yanayojulikana sana kwa jina la Almuaalaqaatu Dhahabiya hatukuti athari za mambo ya kidini.

Na katikati ya jamii hii kubwa ya watu wenye ujinga wa kufedhehesha. Kulikuwa na watu wachache wanaohesabika kwa vidole, waliojulikana kama Mahunafaa (yaani walioasi mwendo wa jamii – na hili ndilo kundi alilolitegemea Bwana ‘‘Renan’’ katika kuelezea picha ya jamii ya Waarabu katika zama hizo. Wito wa hawa Mahunafaa ulikuwa ni nini hasa?.. Kwa yakini: hakuna kitu! Zaidi ya uasi wao dhidi ya jamii zao na matazamio yao ya kupata dini sahihi. Hivyo walijaribu kuipata dini hiyo nje ya mzunguko wa mipaka ya jamii zao. Na wao hawakuwa na fikra yoyote ya kina inayoweza kubashiri kuhusu wito wa Uislamu walau kwa mbaali.. Na kila kile kinachowezekana kukipata kutokana na uwepo wa Mahunafaa ni kile kilichoelezwa na ‘‘Renan’’ mwenyewe kwa haki kabisa. Nayo ni kuwepo kwa ‘‘aina fulani ya wasiwasi na kungoja kitu kisichojulikana na chenye utata’’ (Uk 1090). Na kwa ujumla, vyovyote vile watu walivyokariri ibara hizi: Allah, dini, manabii, vitabu na pepo katika kipindi hicho. Maneno haya hayakujulisha fikra yoyote ya wazi katika nafsi zao.

Na kilicho bora kwa watu hawa, wawazungumzie Wasabai waliotajwa katika Quran: *((… na Wakristo na Wasabai; yoyote (miongoni mwao) atakayemwamini Mwenyezi Mungu (sasa kama anavyosema Nabii Muhammad) na akaamini siku ya mwisho…))* Al-Baqarah 62. Na Al-Maidah 69, na Al-Hajj 17.

Na Wasabai ni kundi la wapagani wanaoabudu masanamu lenye sifa za kipekee. (Wasabai wa Harani ni wale ambao wanajinasibisha na Sabai bi Sithi aliyekuwa anadai kuwa anasambaza mafundisho ya dini ya baba yake. Na kwamba yeye alikuwa na kitabu cha dini hiyo kwa lugha ya Kisuriyani). Au wao ni kundi la Wayahudi Wakristo liitwalo ((Wasabai)) miongoni mwa (Wakristo wa Yohana Mbatizaji). Au lenyewe ni kundi la kwanza lililokuwa linajiita jina hili. Maswala haya ni maswala yenye tofauti. Fikra kuu na kauli mbiu za Wasabai zilikuwa maarufu na zimekosolewa vikali na Quran na

Hadithi. Na baadhi ya desturi za kundi hili zilikuwa zimeenea sana kwa Maqurayshi kwa kiwango ambacho, inakuwa ni vigumu kuzitenganisha na ibada za kipagani zilizotawala kipindi hicho. Kwa mfano kuwapa uungu malaika na nyota, pamoja na kudai kuwa nyota zinaathiri matukio ya ardhini. Na kumsimika simba ambaye alikuwa akitolewa sadaka kwa ajili ya miungu iliyo daraja la chini badala ya kuielekeza kwa Mungu wa Haki. Pia walikuwa na ibara za mapambio katika hija zilizokuwa na shiriki kwa Mwenyezi Mungu… Pia wana matendo mengine ya kiibada na ada zilizotofauti kabisa na ada za kipagani na za Kiislamu. Hija yao ilikuwa ikifanyika huko Haraani nchini Iraq. Na sadaka zao za kuchinja zilikuwa zikiteketezwa kwa moto kikamilifu. Walikuwa wanaharamisha ndoa za wake wengi. Hawatahiriwi. Na ibada zao zilikuwa ni matambiko wanayokusudia sayari na zilikukwa zikifanywa mara tatu kwa siku: wakati wa kuchomoza jua, kuinama kwa jua na kuzama kwa jua. Na hivi hivi tunaona kuwa upagani uliokuwa umetawala maeneo ya Hijazi (Makka na Madina nchi Saudi Arabia) hauwezi kutupatia maelezo sahihi juu ya chanzo cha Quran.

Huenda mazingira ya Kiyahudi na Kikristo ya wakati huo yakatupatia baadhi ya mwangaza katika mada hii. Hatutotegemea sana juu ya kisa cha mchungaji Bahiira. Kisa ambacho kinataja kuwa Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, alikutana naye akiwa na umri wa miaka kumi na miwili. Pale yeye na baba yake mdogo Bwana Abuu Twalibi walipoenda katika safari yake ya kwenda Sham (Syria). Tukio hilo, ima ni la ngano za kutunga au ni la hakika. Tuchukulie matukio yote hayo yaliyotokea katika hesabu zetu. Huo mkutano ulikuwa mbele ya watu wote waliokuwepo safarini. Na Muhammad, rehema na Amani ziwe juu yake, alikuwa anashika nafasi ya kuwa ‘‘muulizwa’’ na sio msikilizaji.

Na punde tu baada ya mchungaji kumuhoji Mtume Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake, aligundua kuwa utume anaoutarajia, unatarajiwa kupewa kijana huyu na kuwa mtume wa baadaye. Jambo sahihi linatuzuia sisi kuuzingatia mkutano huu wa mpito tu kuwa ndio chanzo cha mafundisho ya Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake.

Na inasemekana kuwa baadhi ya wasafiri wa baharini wa Kirumi au wa Kiafrika weusi wa Ethiopia ‘‘wauza mvinyo au wapambanaji/wamachinga’’ walikuwa wakiishi katika viunga vya Makka vilivyojitenga kando. Pia inasemekana kuwa: ‘‘Hakika Injili ilikuwa ikifundishwa katika baa za Akili Khaam’’. Je, Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake, alikutana na fikra za

kidini katika maeneo haya? Na licha ya hayo, hakika wao bado wanatuacha katika utata na sintofahamu. Wala hawatupatii uthibitisho hata mmoja unaotuthibitishia uhusiano halisi wa aina hii. Huku ikijulikana kuwa shughuli za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kabla ya kupewa kwake utume zilikuwa maarufu na zinajulikana vizuri: zilikuwa huko maeneo ya wazi akichunga wanyama.. Akisafiri katika biashara.. Au katika jamii akiwa pamoja na viongozi wa makabila.

Zaidi ya hayo, kwa hakika hawa walioingizwa walikuwa hawaijui dini yao. Na lugha yao ya kigeni ilikuwa kizuizi kwao cha kimaumbile. Kama kweli hawa ndio walikuwa chanzo kizuri cha kuchukua dini kutoka kwao. Je, haikuwa busara kwa wapinzani wake kukimbilia kwa watu hawa na kuyaangamiza matamanio ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake?

Lililobora tuzungumzie mazingira yenye wigo mpana zaidi na yenye uelewa na utamaduni tajiri zaidi. Katika jambo linalojulikana ni kuwa jamii ya Ghasaasina ya huko Shamu na ya Banii Al-Haarithi ya huko Najrani nchini Yemeni zilikuwa zimejiunga na dini ya Kikristo.. Na hakika Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, katika ujana wake alikuwa mara kwa mara akisafiri kibiashara kwenda Shamu na Yemeni. Sasa kwa nini msafiri huyu wa Kiarabu – kwa kile kilichojulikana kuhusiana na yeye kuwa ana mtazamo mzuri na maumbile yake ya kutilia umuhimu maswala ya kitabia njema – kwa nini hakuathirika na tabia na fikra za jamii hizi? Hii ndio ilikuwa rai ya ‘‘Goldziher’’ na wengineo.. Wameitakidi kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, hapa alipata fungu la kwanza la mfumo wake wa kuirekebisha jamii.. Je, ni kweli kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, aliingia katika ardhi za Kikristo wa kweli? Baadhi ya waandishi wanatiliashaka wazo hili. Kwa kuwa katika Quran hakuna ishara yoyote inayoonesha matukio ya nje nje ya Kikristo. Wakati ambapo Quran inazama katika fikra za kina za roho ya Ukristo wa kimashariki kwa kile ambacho kinatofautiana na mapito ya washairi wa Kiarabu waliowahi kutembelea miji ya Wakristo. Na wakati huo huo kuna waandishi wengine wanakaribia sana na ukweli, nao wanathibitisha kuwa ile misafara ya kibiashara ambayo aliyoenda nayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake, haikufika mbali ya zaidi ya soko la ‘‘Hubaasha’’ katika eneo la Tuhama na ‘‘Gharaashi’’ huko Yemeni.

Na hata kama amewasiliana na Wakristo hivi angepata nini kutoka kwao? Anasema ‘‘G.Sale’’: Ulimwengu wa Kikristo ulikuwa umeshatokezewa na kufutika kwa umbo lake tangu karne ya tatu. Kwa sababu ya tamaa za viongozi

wake, na mipasuko ya wao kwa wao, na migogoro kwa maswala ya kipuuzi kabisa... Wakristo walikuwa wakihimiza mambo kwa ajili ya kuyaridhisha matamanio ya nafsi zao. Na kutumia kila aina ya uchafu, chuki na roho mbaya.. na ukaishia katika kuufukuza na kuutoa huo Ukristo katika uwepo. Na katika zama hizi ndipo zilipodhihiri na kuthibiti aina nyingi za mambo ya hovyo hovyo na ufisadi. Na kanisa lenyewe likajikuta limepasuka pasuka baada ya mkutano wa Nicaea kwa sababu za tofauti zao.

Ama kwa mnasaba wa kanisa la Kimagharibi. Mgogoro wa kugombea kiti cha Uaskofu huko Roma baina ya ‘‘Doumaz’’ na ‘‘Arzisyaan’’ ulifikia upeo wa kukimbilia katika matumizi ya nguvu na mauaji. Ufisadi ukatawala katika tabia na itikadi baina ya viongozi wa nchi na viongozi wa dini. Na hilo likafuatwa na kuharibika kwa raia, hadi ikafikia kuwa shughuli ya watu inayowashughulisha mno ni kukusanya mali kwa njia yoyote ile. Na baada ya hapo ni kuitumia katika anasa na machafu.

Taylor ameandika katika kitabu chake ‘‘Ukristo wa Kale’’ (Mjeledi 1 uk 266): ‘‘Kwa hakika kile alichokutana nacho Muhammad na Wafuasi wake katika kila upande.. Hakikuwa kingine zaidi ya mambo ya hovyo hovyo yanayochukiza. Na upagani uliopea (uliopevuka) na kutia aibu. Na madhehebu ya kanisa yaliyodanganyika. Na ibada za kidini zilizoharibika na ni za kitoto. Kiasi ambacho Waarabu wenye akili yenye mwanga wakahisi kuwa wao ni Mitume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, waliopewa jukumu la kurekebisha kile kilichoizunguka dunia miongoni mwa ufisadi…’’. Na pale ‘‘Mosheim’’ alipotaka kuzielezea zama hizi, alionesha kupingana baina ya Wakristo wa mwanzo na wa mwishoni. Na akatoka na matokeo kuwa dini ya kweli katika karne ya saba ilikuwa imezikwa chini ya lundo la mambo ya hovyo hovyo na ufahamu mbaya na mambo ya kipuuzi. Hadi ikafikia kuwa mambo yalivyo Ukristo hauwezi kuinua kichwa chake. Kana kwamba kurasa hizi zimeandikwa ili kuielezea aya hii: *‘‘Na kwa wale waliosema: ‘‘Sisi ni Wakristo,’’ tulichukua ahadi kwao, lakini wakaacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa, kwa hiyo tukaweka baina yao (wenyewe kwa wenyewe) uadui na bughudha mpaka siku ya Kiama…’’* Al-Maidah 14.

Je, njia za Waarabu walioingia Ukristo zilikuwa na hali nzuri kuliko wenzao? Hapana.. kwa sababu wao waliendelea kudumisha ada zao na tamaduni zao za kipagani za kale. Ali bin Abuu Twalib amesema kwa hakika kile walichokichukua kabila la Taghaalibah kutoka katika Ukristo hakikuwa kingine zaidi ya kunywa pombe. Na ‘‘Huart’’ anasema: ‘‘Vyovyote

itakavyokuwa ushawishi wa fikra ya kuathirika kwa Muhammad kwa yale aliyoyashuhudia miongoni mwa utekelezaji wa Ukristo huko Syria. Kwa hakika unapaswa kuiweka mbali fikra hiyo. Kwa sababu ya udhaifu wa nyaraka za ushahidi na kwa mujibu wa misingi ya kihistoria iliyosahihi''.

Mtume Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake, hapana shaka kuwa mambo aliyokutana nayo kwa bahati mpaka sasa yamejikusanya katika jengo linalopaswa kuvunjwa. Na hakukuwa katika alichokutana nacho kinachofaa kulisimamishia jengo hilo jipya..

Na tupanue wigo wa utafiti huu kidogo, mpaka tufikie ulimwengu wa unaosikika, na mazingira ya vitabu na kujisomea. Kwa hakika yataingia haraka katika ubongo kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, amepata masomo yake kutokana na kupitia kwake moja kwa moja katika vitabu vitakatifu. Ni sawa sawa vya Kikristo au vya Kiyahudi au vinginevyo.[1]

Lakini, je, Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, alikuwa anajua kusoma na kuandika? Quran inajibu kwa kukanusha na kutoa ushahidi wa kutojua kusoma na kuandika kwa Mtume Mkarimu na juu ya mafunzo yake ya kutoka kwa Mola. Yeye ni mtu asiyejua kusoma na kuandika katika watu wasiojua kusoma na kuandika.[2] Na hajapatapo kusoma kitabu au kuandika chochote kwa mkono wake. *((Na hukuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, (ingekuwa hivyo) wangefanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki).))* Al-Ankabuut 48. Na

[1] Amepita Dr. ''S. Tisdall'' mapito ya kufikia upeo kudai kuwa: eti baadhi ya misingi ya Uislamu inatokana na Uzaradishtiya.

[2] ''Leblois'' alijaribu kuwaiga wenzake miongoni mwa waandishi ili athibitishe kinyume. Kwa kutegemea hadithi yenye kueleza kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akiwa kitandani anakaribia kufa aliomba aletewe kitu cha kuandikia usia wake kuhusu suala la uongozi wa baada yake. Nayo ni hoja isiyo na mashiko kwa kuwa hadithi hii haijasema kuwa Mtume aliandika… Na kwa upande mwingine kitenzi ''anaandika'' kwa mujibu wa viongozi na wakuu wa nchi kwa ujumla – maana yake ''anawatajia waandike au anapiga muhuri wake''. Na kwa ajili hiyo ndipo palisemwa katika suluhu ya Hudaibiya ''Wakati alipokuwa Mtume anaandika yeye na Suhaili ghafla akatokea…'' kiuhalisia aliyekuwa akiandika ni Ali kwa kutamkiwa na Mtume. Pia kuna ufafanuzi mwingine waliojaribu kuutoa kutokana na tukio la uwasilishaji lililotokea wakati wa suluhu. Nalo ni kuwa Mtume pale alipomwamrisha Ali kufuta jina la Mtume ''Muhammad Mtume wa Allah..'' Je, Ali ana ujasiri wa kulifuta? Na wakati huo Mtume alimuuliza Ali sehemu lilipo neno linalotakiwa kulifuta na akaliondosha kwa mkono wake… Mpaka hapa hakuna tofauti, isipokuwa kuna hadithi sahihi zinaongeza kuwa Mtume aliandika sehemu ya neno lililofutwa ''Muhammad Bin Abdillahi'' Na hili. Kwa hivyo linanasibishwa kwa nje nje kuwa mwandishi ni Mtume rehema na Amani ziwe juu yake: kwa hakika jaribio la kuitumia nukta hii finyu ili kuthibitisha kuwa Mtume anajua kuandika ni kusahau uhalisia wenyewe unaosema kuwa: Hakika yake hakujua neno linalopaswa kufutwa ila kwa mwongozo mwandishi wake. Na vile vile huko ni kujisahaulisha na kile kilichowekwa wazi katika sehemu hiyo hiyo, ya kuwa Mtume ''Hawezi kuandika''. Kwa hakika jaribio lolote lile la kuthibitisha kinyume, hilo ni dhaifu mno na haliwezi kuutikisa ukweli huu.. kwa kuwa maisha ya Muhammad rehema na amani ziwe juu yake yanajulikana hadi katika maelezo ya mambo ya kina kabisa. Na watu wake hawakuwa na ujinga kiasi hicho cha kutojua ukweli huu.

hapana shaka kuwa wanaompinga Mtume rehema na Amani ziwe juu yake, walikuwa wanajua vizuri huku kutokujua kwake kusoma na kuandika. Kwa sababu wao walisema kumuhusu yeye: *((Na wakasema: ‘‘ni visa vya (watu) wa zamani alivyoviandikisha (Muhammad, kwani mwenyewe hajui kuandika wala kusoma) anavyosomewa asubuhi na jioni)).* Al-Furqaan 5. Yaani ameandikiwa na wengine. Na hawakusema: ‘‘Ameyaandika’’. Na maana hii iliwachanganya baadhi ya mustashriqina. Na hata kama ikikubalika kuwa Mtume alikuwa anajua kusoma, kwa hakika kulikuwa na kikwazo ambacho ni kigumu kukiondoa. Kwani kwa wakati huo hakukuwa na Torati wala Injili ya lugha ya Kiarabu.[1]

Na uwepo wa nyaraka hizi kwa lugha za kigeni ilikuwa ni ukiritimba wa baadhi ya wasomi wanaozungumza zaidi ya lugha moja.. Ambao wameelezwa na Quran kuwa wao ni mabakhili kwa kile walichonacho miongoni mwa elimu: *((… Sema ni nani aliyekiteremsha kitabu alichokileta Musa? Chenye nuru na uwongofu kwa watu, mlichokifanya juzuu juzuu, (zenye vile mnavyotaka vidhihiri) mkadhihirisha. Na yaliyo mengi mkayaficha…’’* Al-An`am 91.

Na kwa hali yoyote ile historia haijatueleza kuwa kulikuwa na mawasiliano yoyote maalum. Na kwa kuwa maneno yanazunguka katika mambo ya jumla jumla tu, kwa hakika ni vigumu kutoa maamuzi katika hili. Na tunapohitaji kuainishwa, hapo ndipo inapotokea kupingana na kubomoana,

Lakini kama Muhammad rehema na amani ziwe juu yake hakupata fikra zake za kidini mubashara si kutoka kwa maandiko ya Taurati wala ya Injili, wala kutoka kwa wasomi waliobobea. Je, si jambo linalowezekana kuwa amezikusanya fikra zake kutoka kwa baadhi ya washairi wa Kiarabu, Kiyahudi na Kikristo au wale waliofanana nao?

Quran inatuwekea wazi kuwa, kwa ujumla Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuwa akitunga mashairi. Bali Quran imeyazingatia mashairi ni pumbao hayastahiki kuwa kwa Mtume.

Kisha tujiulize kuhusu mafundisho yepi yanayowezekana kupatikana kutoka katika aina hii ya fasihi?

**Kwa hapa tunapata mielekeo miwili ya fasihi ya zama za Kijahili:**

---

[1] Dr. ‘‘Graff’’ anathibitisha kuwa hakukuwa na haja ya kuwa na Injili ya Kiarabu ila katika karne ya tisa na kumi… Na Kasisi ‘‘Chediak’’ anasema kuwa hajaweza kupata rejea ya historia ya tafsiri ya kale ya Agano Jipya kwa lugha ya Kiarabu iliyo ya mbali zaidi ya karne ya kumi na moja.

**Wa kwanza;** hakika baadhi ya washairi mfano Al-aashaa alikuwa anatilia umuhimu suala la kuelezea tamaduni na ibada za kanisa – na hili hatupati athari zake katika Quran. Bali walikuwa wanatilia umuhimu sana pombe – iliyopigwa pigo la ushindi (knock out) na Quran.

Ama aina ya **pili ya** ushairi ni ile iliyokuwa inakaribia kuwa inajihusisha kikamilifu katika fikra za kidini. Na mashairi ya Ummaya bin Asswalib ni mfano mzuri wa aina hii ya ushairi. Na hasa hasa katika kuelezea maisha ya ahera na visa vya dini za kale. Na katika baadhi ya mada akieleza ibara zile zile za Quran.

Isipokuwa uhalisia wa mashairi ya Umayyah si wenye kukubalika na watu wote kuwa ni mashairi sahihi. Na Umayyah hajadai kuwa yeye ndiye mtunzi asilia, wala kupata ufunuo. Na hakika Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake na Umayyah waliishi zama moja. Na wawili hao, takribani walikuwa na umri unaolingana. Na zaidi kwa hakika Umayyah aliishi na kuendelea kuishi katika kutunga mashairi hadi kufikia takribani miaka minane baada ya kushuka aya ya mwisho ya Makka. Kwa hiyo ni katika ubishi tu tukisema: eti mashairi haya yalikuwa yameitangulia Quran kwa upande wa kihistoria. Na hebu tuuchukue katika mazingatio yetu msimamo wa wanaompinga Nabii rehema na amani ziwe juu yake, ambao daima walikuwa macho ili kupata upenyo mdogo tu ili wamwelekezee pigo lao la kummaliza. Kwa hiyo ilikuwa ni wepesi mno kwao, kuweka mkono wao katika mashairi yaliyoibwa kutoka kwa Umayyah ambaye wino wake ulikuwa bado haujakauka badala ya kuelekeza tuhuma zao kwa kila upande hadi ikafikia kumpachika Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa ni mwendawazimu kwa kufasiri kwao tukio la ajabu la Quran.

Na kutokana na hili tunafupisha hivi – hata kama haitakuwa kwa uhakika. Basi kwa uchache kuna uwezekano mkubwa – ya kuwa Quran ndio ilikuwa msingi wa zao la fasihi katika zama za kuteremka kwake. Kama vile ilivyo ni uhakika kuwa yenyewe ndio msingi wa fasihi katika zama zilizofuata. Na uhakiki wa mashairi ya Umayyah kwa namna ya upekee umethibitisha kuwa yenyewe yanarejea katika vyanzo vingi tofauti tofauti. Na haya ndiyo aliyoyaona ‘‘Huwaarat’’. Pale mshairi huyu anapozungumzia kuhusu wasifu wa moto alikuwa anaiga Taurati. Na katika wasifu wa pepo anatumia ibara za Quran. Na katika visa vya kihistoria vya kidini alikuwa anarejea katika ngano za kijamii.

Mbele yetu inabaki hatua ya mwisho katika sekta ya kutafuta chanzo asilia cha nje cha Quran. Zinduka chanzo chenyewe ni fikra za kijamii.

Ni katika jambo lisilokubalika kiakili kudai etu Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akiishi kwa kujitenga kabisa hadi kufikia eti hajui mambo ya umma wake katika nukta hii. Na inadhihirika ndani ya Quran ya kwamba umma huu ulikuwa na baadhi ya ujuzi kuhusu dini zilizotangulia. Jambo lililoufanya umma huu kumtaka Mtume rehema na amani ziwe juu yake alete: *((… Basi atuletee Muujiza kama walivyotumwa (Mitume) wa kwanza)).* Al-Anbiyaa 5. Na jamii yake katika kumpinga Mtume inategemea kwa kile walichokisikia: *((‘‘Sisi hatukusikia haya (ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja hata) hata katika hii mila ya mwisho…))* Sad 7. Na jamii hii inalinganisha mila ya Issa (Yesu) na itikadi ya kipagani… hadi mwisho. Lakini kuna sababu nyingi zinazotuzuia kutanua taswira zetu katika jambo hili.. kwani ni katika jambo linaloonekana kutiliwa umuhimu – hata kwa upande wa wale ambao wamesafiri na wakajifunza – walikuwa wanajihusisha na mambo mengine tu na siyo mambo ya kidini.. zaidi ya hayo historia imenyamaza hadi kufikia kiwango kile kile cha maarifa yaliyoandikwa na ambayo yalikuwa kwa umma huu usiojua kusoma na kuandika tena ulioghafilika.

Kiuhalisia, kuvuta taswira ya kuwa umma huu ulifikia daraja ya kuwa na ujuzi unaouwezesha kushiriki katika elimu ambazo maarifa yake yalihusika na baadhi ya wanazuoni wanaohesabika katika nyakati hizo. Jambo hili linahesabiwa ni fikra ya ajabu ambayo haikubaliani na ukweli uliothibitishwa. Hakujapatapo kutokea katika zama yoyote miongoni mwa zama za kihistoria – na kwa jamii nyingi, kimaendeleo na kielimu – kuwa tumepata mfano wa muunganiko huu wa baina ya ujinga na mjuzi aliyebobea.. Na Quran haikukaa kimya kuhusu umuhimu wa mafundisho yake kwa mnasaba wa Waarabu akiwemo ndani yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Zaidi ya hayo hawakuwa na ujuzi wa mafundisho ya Quran kabla ya kuteremka kwa ufunuo kwa Mtume: *((Hizi ni khabari za ghaibu tunazokufunulia; nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao ndani ya maji (kwa kura, wajue) nani wao atamlea Maryamu, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana.))* Aali Imran 44. *((Hizi ni katika khabari za siri tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii (Qurani kuteremshwa)…))* Hud 49. *((Sisi tunakusimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qurani hii. Na hakika ulikuwa kabla ya haya ni miongoni mwa wasio na khabari (hizi).))* Yusuf 3. *((Hizi ni katika khabari za siri tulizokufunulia. Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao, hali*

*wakifanya vitimbi vibaya.))* Yusuf 102. Na kama jambo lilikuwa kinyume na hivyo, maadui wa Uislamu walikuwa wanangoja nini?

Na kwa kutazama kuwa fikra zilizoenea katika jamii hii hazikuwa na mwelekeo mmoja. Bali kila kundi, wakiwemo wapagani, maswabai, na viongozi wa dini, wafursi, Wayahudi na Wakristo kila moja lilikuwa na mtindo wake maalum katika kuuwasilisha ukweli. Je, Mtume rehema na amani ziwe juu yake angeliamini kundi lipi? Na angetegemea mahubiri yepi katika haya mahubiri yanayopingana? Je, Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake alikuwa anaweza kuamini maoni ya wengi kiwepesi wepesi hali ya kuwa yeye ndiye aliyekuwa akisimama msimamo wa kuupa changamoto msimamo wa wale walio wengi? Na kisha Mtume huyo huyo ndio alifanya hima kutusimulia itikadi batili za kila kundi na kila dhehebu na kila tawi katika makundi hayo ya zama zake. Je, ni mkorogeko wa aina gani ungeukuta katika Quran: *((... Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi.))* An-Nisaa 82.

Na mpaka hapa tunalazimika kuingiza sababu nyingine, nayo ni sababu ya kibinafsi.

Huenda ikadhaniwa kuwa, Mtume rehema na amani ziwe juu yake, naye akiwa anaabudu katika pango Hiraa kabla ya kuteremka kwa ufunuo. Au na yeye akiwa amejitenga peke yake wakati wa kuchunga mbuzi na kondoo – kwa fikra zake za kina alikuwa anaenda kutafuta ukweli katika suala hili au lile. Na baada ya kuutafuta huo ukweli alikuwa anafanya uchaguzi na kuuainisha..

Na hapa ni wajibu kupambanua maeneo mawili miongoni mwa maeneo ya maarifa ya kibinadamu nayo ni: maarifa ya matukio halisi yatukiayo kwa majaribio ya kihisia (empirical) na maarifa ya kidhahania kiakili. Historia ya mwanadamu haitegemei mantiki/akili (logic) yetu; kwa kuwa yenyewe huenda ikajumuisha matukio yanayopingana na yale yanayokubalika na akili. Hivyo Muhammad rehema na amani ziwe juu yake hawezi kwa kujitenga kwake na kuwa na nafsi yake tu kugundua tukio lililotokea katika historia fulani katika zama zilizopita. Na kwa ajili hii, juhudi zote zimeelekezwa katika kulinganisha baina ya visa vya dini katika Quran na vile vya katika vitabu vilivoteremshwa wakati uliopita ili kufikia kujua sababu iliyopelekea kupatikana huku kuafikiana kwa ajabu mno.

Tafakuri za kiakili huenda zikawa zina thamani kubwa katika sekta za kufunua ukweli wa milele.. Ni ipi hiyo mipaka ya akili safi katika mada ya dini?

Bila shaka ni mipaka finyu.. kwa sababu akili inaweza kuthibitisha upotofu wa upagani na mambo ya hovyo hovyo na hombwe lake na kutokuwa na maana. Lakini ni lini jambo hilo limeangaza njia yake, na nini kinajengwa katika nafasi yake? Hakuna mahubiri wala madhehebu au nadharia inayojengeka katika ukweli hasi. Na katika jambo lenye kushinda ni kuwa Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake aliikuta nafsi ikiwa katika hali kama hii tunayochorewa na Quran, hali ya huzuni kana kwamba yeye anaugulia chini ya mzigo mzito: *((Na tukakuondolea mzigo wako (mzito). Uliovunja mgongo wako.))* Alam-Nashrah 2 – 3. *((Na akakukuta hujui kuongoza njia. akakuongoza))*. Adh Dhuhaa 7.

Na kuvuka hatua ya mwanzo ilikuwa ni kwa haraka mno. Hakika maarifa ya kumjua Allah Mtukufu Aliyetukuka sio tu ndio elimu yote ya kidini iliyomo ndani ya Quran. Na njia ya kuifikia elimu ya Quran ni ndefu yenye makorongo kama haitakuwa imezibwa mbele ya akili finyu ya mwanadamu anayetegemea uwezo wake wenye mipaka finyu. Basi kwa ilhamu (aina ya ufunuo) gani, Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake ameweza kufunua sifa nyingi nzuri za Allah, uhusiano wa Allah na ulimwengu unaoonekana na usioonekana, mafikio ya mwanadamu baada ya kufa…? Na bila ya kurejea nyuma hata katika ukweli mmoja aliowahi kuutangaza? Pamoja na kuuhifadhi ukweli huo, kwa wakati huo huo kuna kukubaliana kwa ajabu mno pamoja na ukweli wa vitabu vya mbinguni vilivyotangulia na vilivyohifadhiwa kwa uangalifu mkubwa chini ya uangalizi wa wataalamu? Hapana shaka kwamba akili; kwa vyovyote vile itakavyofikia haiwezi kupiga hata hatua moja katika njia hii yenye mfano kama huu, wa uaminifu huu na uwazi huu kama haikuwa na msaada na kusaidiwa kutoka katika mafundisho chanya yaliyo nje ya mipaka ya kibinadamu. Na Quran inathibitisha hili, na inakazia kuwa Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake hakuwa akijua kabla ya kuteremkiwa na ufunuo: *((… Ulikuwa hujui Kitabu ni nini wala Imani; ...))* Ash-Shuura 52. Haya, na zaidi ni lile jengo la kuweka sheria kwa mionekano yake mbalimbali, miongoni mwayo ni mionekano ya kitabia njema, kijamii na kuabudu. Je, alikuwa ana uwezo wa kumwongoza mtu mwingine hali yeye mwenyewe halijui hilo?

## Sura ya pili:
## Kutafiti chanzo cha Quran katika kipindi cha Madina

Je, kuhama kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kuhamia katika mazingira mapya na kuungana kwake na watu waliopewa kitabu, hilo liliathiri tabia zake na chanzo cha elimu yake?

Baada ya kuzunguka pande za Makka kwa haraka haraka na kufikia matokeo hasi popote tulipotafuta. Tulilazimika kututoa hukumu yetu sasa hivi. Lau kama hakujatokea mabadiliko yoyote yale katika mwenendo wa Utume uliobarikiwa. Mabadiliko haya yaliyotokea kwa kuhama kwa sifa ya kipekee. Kwani Mtume rehema na amani ziwe juu yake alihamia mazingira yanayomkaribisha na kumpenda. Akizungukwa na wafuasi wake wenye nguvu na waaminifu. Akawa anawasiliana na kundi lililokuwa na mfumo kamili wa kidini. Na lenye kitabu chake kitakatifu. Nao ni Wayahudi wa Madina.

Kama tutawasilisha kwa sifa ya kijumla, msimamo wa Quran kuhusu Wayahudi.. Je, tunaikuta Quran inaizingatia jamii hii mpya kuwa ni mfano wa kweli wa fadhila zilizoteremka kutoka kwa Allah na kwa hiyo inastahiki kufuatwa na kuigwa?

Tunaona kuwa msimamo wa Quran kwa Wayahudi unapingana na msimamo wake juu ya jamii ya Kikristo. Pindi ikiuongelea Ukristo kwa sifa ya kipekee tunakuta – kama hajawasifia. *((Hakika walio maadui zaidi kuliko watu (wengine) kwa Waislamu ni Mayahudi na wale mushrikina (wasiokuwa na Kitabu), na utawaona waliokaribu kwa urafiki na Waislamu ni wale waliosema: ‘‘sisi ni Wakristo.’’ (Hayo) ni kwa sababu wako miongoni mwao wanavyuoni na wamchao Mungu, na kwa sababu wao (Wakristo) hawatakabari; (wakiijua haki huifuata)).* Al-Maidah 82. Kwa uchache inawaelekezea wao baadhi ya lawama kwa lahaja nyepesi kwa kiasi fulani. *((Na kwa wale waliosema: ‘‘Sisi ni Wakristo,’’ Tulichukua ahadi kwao, lakini wakaacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa, kwa hiyo Tukaweka baina yao (wenyewe kwa wenyewe) uadui na bughudha mpaka Siku ya Kiama. Na Mwenyezi Mungu atawaambia waliokuwa wakiyafanya.))* Al-Maidah 14.

Ama ikizungumzia Wayahudi katika zama hizo au kwa watu wa kitabu kwa ujumla. Kwa hakika msimamo wa Quran unatofautiana. Kwani wao katika mtazamo wa Quran hawafuati kile kilichoteremshwa kwao. Na kwa hakika wanafuata ufunuo wa shetani. *((Wallah! Sisi Tulituma (Mitume) kwa umma*

*zilizokuwa kabla yako; lakini shetani aliwapambia vitendo vyao (vile vibaya wakaviona vizuri wakaendelea navyo). Kwa hivyo leo yeye (shetani) ni rafiki yao; (Lakini watachukiana naye kweli kweli Akhera), nao watapata adhabu iumizayo.))* An-nahl 63.

Na pale Quran ilipogusia yale waliyoyafanya Mayahudi wa Yemeni kwa Wakristo ya kuwawasha moto katika Mahandaki ilizingatia tukio hilo kuwa ni jinai kubwa ya kula njama kwa makusudi dhidi ya Imani ya haki. *((Kuwa) wameangamizwa watu waliowaadhibu Wakristo katika mahandaki.))* Al-Buruji 4. Na pale Quran ilipohamia Madina iliendelea kushikilia msimamo wake na ikaongeza idadi ya kuwashutumu. Kwani wale walioipokea Torati na kuhifadhi maandiko yake hawazingatii maandiko yake kwa moyo wote. *((Mfano wa wale waliopewa Taurati, kisha hawakuichukua (kwa kuitumia) ni kama punda anayebeba vitabu vikubwa vikubwa (bila kupata nafuu kwavyo). Ni mbaya kabisa mfano wa watu waliozikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu.))* Al-Juma`a 5. Na huku wao wakifanya miamala ya riba na kukumbilia kutumia hila mbalimbali ili wale mali za watu kwa batili. *((Na kwa (sababu ya) kula kwao riba, na hali wamekatazwa wasiile, na (kadhalika) kwa kula kwao mali za watu kwa batili. Tumewaandalia makafiri – nao ndio wao – adhabu iumizayo.))* An-nisaa 161. Na kwa kutegemea baadhi ya fahamu mbaya na matumaini hewa wanajihalalishia rushwa na uongo. *((Basi adhabu kali itawathibitikia wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: ‘‘Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu.’’ (Wanasema uwongo huo), ili wachukue thamani ndogo ya kilimwengu. Basi ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao (wakayasingizia kuwa ya Mungu). Na ole wao kwa yale wanayoyachuma.))* Al-Baqarah 79.

Huku wakiamini kuwa wao hawatahukumiwa kuhusiana na makundi mengine. Wala hawashikamani na kufanya uadilifu katika miamala yao na watu wengine. *((Na katika waliopewa Kitabu kuna ambao ukiwapa amana ya mrundi wa mali watakurudishia. Na katika wao kuna ambao ukiweka kwao amana ya dinari moja (tu hivi) hawakurudishii isipokuwa uendelee kuwasimamia (kuwadai). Haya ni kwa sababu walisema: ‘‘Hapana njia juu yetu (ya kulaumiwa) kwa (ajili) ya hawa wajinga (watu wasiokuwa dini moja na sisi).’’ Na wanasema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu, hali wanajua (kuwa sivyo hivyo.))* Aali Imran 75.

Je, sio jambo la kushangaza kuchukulia kuwa watu ambao Quran imewasimamia msimamo huu ndio wawe kielelezo cha kuigwa na Muhammad

rehema na amani ziwe juu yake, na pia ndio wawe chanzo cha mafundisho yake? Kuchukulia huku, vyovyote vile kutakavyofikia katika viwango vya kupingana na akili, hili halizuii kufanya utafiti na uchunguzi juu ya uwezekano huu. Huenda uhalisia ukaonesha uongo wa maamuzi yote ya kufuata mkumbo ya wakati uliopita – kuna faida gani kuijenga Imani katika mchanga unaotembea?

Baadhi ya Mustashiriqina wamejaribu kuthibitisha kuwa yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake yanaboreshwa na kurekebishwa na kurejeshwa nyuma kulingana na kuungana kwake pamoja na jamii ya kiraia iliyopewa elimu. Na wengi wao wameathirika na mitazamo miwili ya kijumla walioikuta ikipingana na utakatifu wa ujumbe wake. Na hoja zao kubwa zinajikita katika msimamo wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake wa kuupinga Uyahudi. Msimamo aliouchukua huko Madina na ni msimamo ambao wameuzingatia kuwa wenyewe ni mabadiliko ya ghafla kwa mnasaba wa msimamo wake wa kule Makka. Na pale tunapoongeza katika hilo, kuna suala la Mtume kuoa wake wengi mwishoni mwa siku za uhai wake. Hilo kwa mtazamo wao, nalo linakuwa ni kama kuvunja mfumo wa kitabia wa Kiislamu katika hatua zake za mwisho. Na hata Mustashiriqina wale wanaoheshimu Uislamu ukiwa unaanza kwa kukandamizwa na kujazwa majeruhi. Pia wanamheshimu Mtume Mwislamu aliyeoa mwanamke mmoja. Hao mustashiriqina wanapatwa na shida kubwa pale wanapomuona baadaye akiwa ‘‘mikono yake imechafuka damu’’. ‘‘na amezungukwa na msafara wa wake zake’’.

Hawa mustashiriqina katika msimamo wao huu walikuwa wanasukumwa zaidi na misimamo yao, ili wasivunje sehemu za imani zao za mafundisho ya Torati kabla ya kuja kwa Masihi. Kuliko kutegemea kwao ushahidi wa kiakili na utafiti. Na kwa hali yoyote ile tumeshathibitisha katika yale yaliyotangulia msimamo wa kanuni za Qurani katika nukta ya kwanza, maswala yale yanayotutosheleza na kurudia rudia. Ama nukta ya pili, kwa hakika yenyewe, hata kama itakuwa inagusa mada ya utafiti wetu kwa mbali nayo ni Quran na sio mambo binafsi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, isipokuwa sisi tutaona namna gani Mtume rehema na Amani ziwe juu yake yanavyoonekana kupitia Quran.

Utu binafsi wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, katika Quran unadhihiri mara chache mno tena katika sehemu tatu: Hisia, Matakwa na Imani. Yeye kwa tabia yake ni binadamu kama Mitume waliotangulia:

*((Hatukuwatuma, (Hatukuwapa Utume kabla yako ila wanaume (wa kibinadamu, si Malaika); Tuliowafunulia, (Tuliowaletea Wahyi). Basi waulizeni wenye kumbukumbu (ya mambo ya zamani) ikiwa nyinyi hamjui. Wala Hatukuwajaalia (hao Mitume kuwa) miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele (wasife))* Al-Anbiyaa 7 – 8. Yeye anakula chakula na anaenda kuchuma riziki yake. *((Na hatukupeleka kabla yako Mitume ila bila shaka walikuwa wakila chakula na wakenda masokoni; na tumewajaalia baadhi yenu wawe majaribio (mitihani) kwa wengine; Je, mtavumilia? Na Mola wako Ndiye aonaye.))* Al-Furqaan 20. Na yeye ana wake na watoto, hii ni kwa baadhi ya Mitume. *((Na Tuliwapeleka Mitume kabla yako, na Tukawaajaalia kuwa na wake na watoto). Na haiyumkiniki kwa Mtume kuleta miujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila muda unayohukumu aliyoiandika Mwenyezi Mungu, (ukitimia muda huo itafika hukumu hiyo.))* Ar-Raad 38. Na yeye anaheshimu uzuri wa kibinadamu. *((Baada ya hawa (wake ulio nao), si halali kwako (kuoa) wanawake (wengine, ukazidisha kuliko idadi ya hawa ulio nao); wala (si halali) kuwabadilisha kwa wake wengine (ili idadi iwe ile ile sawa sawa), ingawa uzuri wao (wa maumbo yao) utakupendeza; isipokuwa yule uliyemtamalaki kwa mkono wako wa kulia. Na Mwenyezi Mungu ni Mchungaji wa kila kitu.))* Al-Ahzaab 52.

Ama sababu ya matakwa, hapa tunamuona Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasifika kwa uweza wa kujizuia hivyo anaiharamishia nafsi yake mambo ya halali miongoni mwa vyakula. *((Ewe Mtume! Mbona (kwa nini) unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu! Unatafuta radhi za wake zako (ndiyo maana ukafanya hivi)? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.))* At-tahrym 1. Kwa hakika Aisha amesema, kuhusiana na Mtume rehema na amani ziwe juu yake, ya kuwa hajawahi kuwepo mtu mfano wa Mtume katika kuzidhibiti hisia zake.

Kisha inakuja mada ya kuingia kwake moja kwa moja katika mafundisho ya Allah Mtukufu Aliyetukuka. Mafundisho ambayo yapo juu zaidi ya mtazamo wake na mapendeleo yake. Tunataja kanuni ya Quran ambayo inamuainishia Mtume makundi ya wanawake ambao anaweza kuwaoa, miongoni mwao ni:

*((Ewe Nabii! Tumekuhalalishia wake zako uliowapa mahari yao, na (wanawake) uliowatamalaki kwa mkono wako wa kulia katika wale aliokupa Mwenyezi Mungu, na (Tumekuhalalishia mabinti wa ami zako na mabinti wa shangazi yako, na mabinti wa wajomba zako na mabinti wa dada za mama zako walohama pamoja nawe; na (tumekuhalalishia kila) mwanamke Mwislamu*

*akijitoa mwenyewe bure kwa Mtume, kama mwenyewe Mtume akitaka kumuoa. Ni halali kwako tu ……))* Al-Ahzabu 50. Na kanuni nyingine inayomharamishia ndoa mpya nyingine yoyote ile, vyovyote itakavyokuwa nguvu za matamanio yake katika ndoa hiyo, au kubadilisha wake zake. *((Baada ya hawa (wake ulio nao), si halali kwako (kuoa) wanawake (wengine, ukazidisha kuliko idadi ya hawa ulio nao); wala (si halali) kuwabadilisha kwa wake wengine (ili idadi iwe ile ile sawa sawa), ingawa uzuri wao (wa maumbo yao) utakupendeza; isipokuwa yule uliyemtamalaki kwa mkono wako wa kulia. Na Mwenyezi Mungu ni Mchungaji wa kila kitu.))* Al-Ahzabu 52. Kisha kuna kanuni maalum kwa hali ya matalaka wa Zaidu (mtoto wake wa kumuasili). Na hiyo ndio ndoa ya pekee iliyoandikwa katika Quran. *((Na (wakumbushe) ulipomwambia yule ambaye Mwenyezi Mungu amemneemesha (kwakumuafikia Uislamu) na wewe ukamneemesha (kwa kumpa uungwana, Naye ni Bwana Zaid bin Haritha ulipomwambia); ''Shikamana na mkeo na umche Mwenyezi Mungu (usimuache),'' na ukaficha katika nafsi yako aliotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa (nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amekuamrisha umuoe wewe huyo mkewe atakapomuacha ili iondoke ile itikadi iliyokuwa ikiitikadiwa ya kuwa mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa), na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea. Basi alipokwisha Zaid haja yake na mwanamke huyo, Tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa Waislamu kuwaoa wake wa watoto wao wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa.))* Al-Ahzabu 37.

Utamuona Mtume rehema na amani ziwe juu yake, anajaribu kwa juhudi zake zote kuizuia ndoa hii. Lakini kanuni za Quran zinamlazimisha aitekeleze (kwa andiko na utekelezaji kwa vitendo) ili akomeshe mfumo wa kuasili watoto wa kipagani. Na ndoa hii inaweza kuitwa ndoa kwa sababu ya msukumo wa kutekeleza wajibu licha ya kuwa na hisia za kuipinga. Na tukitafiti mazingira ambayo ndoa zake nyingine zilipofungwa, tunakuta ndoa zake nyingi amelazimishwa, kwa mazingatio mema ya kibinadamu. Kwa mfano kuliwaza, kumtukuza mke wa shujaa, au mhamiaji aliyekufa baina ya maswahaba zake akiwa katika kuhama kwake. Au kuimarisha baadhi ya mahusiano na makabila aliyowekeana nayo mikataba. Au kuweka mazingira sahihi ya kuwaachia huru matekwa wa kabila zima… hadi mwisho. Na sio vigumu kuhukumu juu ya muoekano wa tabia njema kwa mtu aliyeishi ujana wake akiwa anajichunga kabisa kabisa. Na baada ya kuoa aliishi na mkewe wa pekee kwa nia njema kwa muda unaokaribia miaka thelathini. Alianza kuoa mke wa pili akiwa na mikaa hamsini na mitano.

Kama tukichukulia katika mazingatio yetu shughuli zake na mazito aliyoyabeba na shida zake za kiujumla na kipekee. Kwa mfano kusimamisha swala tano, kufundisha Quran, kugawa sadaka za jamii, kutatua mizozo, kupokea wageni, kuwaandikia barua wafalme na watawala. Na kuongoza vita vya kijeshi, kuweka sheria na kuanzisha dola…hadi mwisho. Na kwa ufupi alikuwa anachunga kila kitu na kwa watu wote. Kisha baada ya hapo anaswali swala za usiku (hadi miguu yake inavimba. Na anasujudu hadi anadhaniwa amekufa..) yote haya yanatufanya tuamini kuwa sababu ya kweli ya kuoa kwake haikuwa kuridhisha matamanio yake ya kimaumbile.

Baadhi ya Mustashiriqina walitaka kuzama zaidi kisha wakaamini kuwa wao wamepata tofauti ya msingi baina ya mafundisho ya Quran katika kipindi cha Makka na mafundisho yake katika kipindi cha Madina. Wakasema kwa hakika visa vya Kiyahudi na vya Kikristo huko Makka vilikuwa katika hali ya mipango ya mwanzo. Na pale Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, alipoungana na Wayahudi huko Madina aliweza ‘‘kutunga visa vya Ibrahimu na uhusiano wa kinasaba baina ya Ismaili na umma wa Kiarabu’’ kwa hakika ‘‘hapo mwanzo aliishi akiwa ametawaliwa na ufahamu mbaya anaouona ni mzuri nao ni kuwa wito wake – yaani Quran – inakubaliana kikamilifu na vitabu vitakatifu vya Kiyahudi na Kikristo. Lakini upinzani mchungu wa Wayahudi ulimthibitishia kinyume chake’’.

Na mwanzoni swala ilikuwa ni mara mbili mchana na usiku. Ama huko Madina ikaongeza swala ya tatu nayo ni swala ya Laasiri ‘‘akikusudia kuwaiga Wayahudi’’. Na kwa sababu hizo hizo akaweka sheria ya siku ya Ashuraa. Na kibla kikageuzwa kuelekea Bethelehemu. Na hii ni michakato miwili iliyofutwa hapo baadaye kwa sababu za misimamo ya Wayahudi ya kiuadui dhidi ya Uislamu. Na hivyo ndivyo sheria za ibada zinavyoathirika kulingana na mabadiliko ya kisiasa kwa mujibu wa maono yao. Na hata fikra ya Quran kutoka kwa Allah, kwa maoni yao, nayo ilibadilika kutokana na kuathirika kwa misimamo ya kivita katika kipindi cha Madina ‘‘ndipo sifa ya nguvu na ubabe dhidi ya makafiri wapingaji ikaungana na sifa ya upole’’. Hebu turudi polepole ili tuone upeo wa usahihi wa mitazamo yao hii.

Kwa upande wa kile kinachohusika na visa vya Kikristo na Kiyahudi kwa ujumla inatusikitisha kuwa hatukuti kile kinachounga mkono madai haya kwa ukaribu au hata kwa mbaali. Na kwa kurejea katika andiko la Quran linathibitisha kinyume na hayo kikamilifu. Kwani sura za Makka ndizo zinazowasilisha hatua za visa hivyo kwa maelezo ya kina. Na sura za Madina

hazikuachiwa kitu zaidi ya kutoa mafunzo yatokanayo na visa hivyo. Na mara nyingi ni katika uwekaji sawa wa mambo kwa ufupi.

Na ama maudhui ya Ibrahimu yameshatangulia kuashiriwa katika sura za Makka. *((''Mola wetu! Hakika mimi nimewaweka (nimewakalisha baadhi ya kizazi chake – mwanangu Ismaili na mama yake, Hajara) katika bonde (hili la Makka) lisilokuwa na mimea yoyote; katika nyumba yako takatifu (ya Al kaaba utakayotwambia tuijenge). Mola wetu! Wajaalie wasimamishe swala. Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao (wapende kuja kukaa hapa ili pawe mji) na uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru.'')).* Ibrahin 37. Pia Quran imemlingania Mtume afuate mila ya Ibrahimu ambaye ni mtiifu kamili. *((Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahimu (aliyekuwa) mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.))* An-Nahl 123.

Kama ilivyo, sisi hatuujui umma wowote wenye hamu kubwa ya kujua elimu ya nasaba kama umma wa Kiarabu. Umma wa Kiarabu umehifadhi nasaba za kizazi hadi cha ishirini. Na wanakumbushwa na Alkaaba ambayo ina sehemu zinazobeba jina la Ibrahimu na Ismaili. Ama msimamo wa Uislamu kuhusu dini zilizotangulia haukutokezewa na mabadiliko ya aina yoyote ile. Kwani sura za Makka zinawataka watu wa kitabu watoe ushuhuda wao juu ya vitabu vitakatifu. *((Na wanasema waliokufuru: ''Wewe si Mtume.'' Sema: ''Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na baina yenu (kuwa mimi ni Mtume) na (pia) yule mwenye ilimu ya Kitabu. (Kila aliyeisoma Taurati iliyosahihi na Injili iliyo sahihi ameziona khabari za Nabii Muhammad humo).''))* Ar Raad 43.

Na kwa wakati huo huo tunaona, waandishi waliomfuata shetani na kuungana naye. *((Wallahi! Sisi tulituma (Mtume) kwa uma zilizokuwa kabla yako; lakini shetani aliwapambia vitendo vyao (vile vibaya wakaviona vizuri wakaendelea navyo). Kwa hivyo leo yeye (shetani) ni rafiki yao: (Lakini watachukiana naye kweli kweli Akhera), nao watapata adhabu iumizayo.))* An-Nahl 63.

Na Quran ikadumisha msimamo wake huko Madina kwa wanazuoni inaowatolea ushahidi, huku yenyewe ikikazia kuwa idadi kubwa miongoni mwao hawataki kutoa ushahidi wao. *((Wale tuliowapa Kitabu wanakijua (kitendo hiki cha kuelekea Al-Kaaba kuwa ni haki) kama wanavyowajua watoto wao; na baadhi katika wao wanaificha (kila) haki, na hali wanajua.))* Al-baqarah 146.

Na hivi hivi Quran inatofautisha baina ya vitabu vitakatifu vyenyewe, wanazuoni ambao wanavifuata vitabu hivyo kwa moyo wote na baina ya wale wengine wanaojiita Wayahudi au Wakristo. Na hali ya kuwa wanafuata matamanio yao.

Ama idadi ya swala za Waislamu tunathibitisha kuwa hakuna katika vitabu na rejea zote za Kiislamu tulizozipitia, hata ishara moja inayoashiria mfano wa mabadiliko kama haya waliyoyadai. Na katika jambo la kusikitisha hasa, ni kuwa wahakiki wa kimagharibi hawatuoneshi uthibitisho ni wapi wamechukua fikra hii ya ajabu.

Katika Quran hakujakuja kutajwa siku ya Ashura. Lakini wanazuoni wa hadithi wanathibitisha kuwa Maqurayshi kabla ya Uislamu walikuwa wanapupia sana kufunga siku hii. Na hakika Mtume mwenyewe alikuwa akiifunga kabla ya kuhama kwake. Na hadithi zinausia hilo. Ama kauli eti Mtume amechukua maamuzi haya hapo mwanzoni ili kuwaiga Wayahudi na kuwa yeye akarejea nyuma baadaye kwa sababu mabadiliko ya kimsimamo wa kisiasa. Kwa hakika hiyo ni kauli isiyoafikiana na uhalisia uliothibitika.

Ama kuhusu Qibla, madai ya kuwa mabadiliko ya kibla kutoka Bethelehemu (Yorusalemu) kuelekea Al-kaaba (jambo linalotetewa katika Quran) eti yanatokana na uadui wa Wayahudi dhidi ya Uislamu. Madai haya yanaingiliana katika historia. Uadui wa Wayahudi ulidhihiri mwaka 625 A.D wakati ambapo mabadiliko ya Kibla yalikuwa mwaka 623 A.D.

Unabaki mtazamo wa mwisho unaofungamana na fikra za Quran kuhusu Allah. Kwa hakika kile kinachostahiki kusisitizwa hasa ni kinyume cha maono ya wahakiki. Kwani uhalisia unaonesha kuwa maono yao ni uongo. Kwani ‘‘Mungu wa vita’’ anaonekana sana katika sura za Makka kiasi sehemu ambayo ina visa vya kale vya kihistoria vya shari na vya heri. Na adhabu chungu iliyoteremka kwa nyumati mbalimbali. Na ndani yake kuna vitisho – lakini vyenyewe ni vya kudumu – kwa miji ambayo itapita njia kama hizo. Bali kwa hakika vita vilivyoamrishwa huko Madina dhidi ya maadui havikuwa vingine zaidi ya kutekeleza maonyo ya kijumla na ya wazi wazi na yalijirudia rudia kutajwa kabla ya hapo huko Makka. *((Basi wanangoja jingine ila (kuwajia) mfano wa siku za (adhabu zilizowafika) watu waliopita kabla yao? Sema: ‘‘basingojeni, mimi (pia) ni pamoja nanyi katika wanaongojea.))* Yunus 102. Na *((Na waambie wale wasioamini: ‘‘Fanyeni (muyatakayo) kwa tamkini yenu , nasi pia tunafanya (tutakavyo) kwa tamkini yetu. Hakuna anayelazimishwa*

*kufuata Uislamu kwa nguvu.)). Na ngojeni, na sisi tunangojea.''))* Hud 121 – 122. Na *((Na hakutakuwa mji wowote ila sisi tutauhilikisha kabla ya siku ya Kiama au tutauadhibu adhabu kali (kama unastahiki hayo). Haya yameandikwa katika Kitabu (kilichoandika kila kitu)).* Bani Israil 58.

Kimsingi kuna upingaji wa mwisho, na katika vyanzo vingi visivyokuwa hivyo. Kosa hili linahusiana na fikra iliyoenea kutokana na istilahi ''Annasikhi = kufuta''[1] au ''kubatilisha'' katika Uislamu. Watafiti wasiokuwa wa Kiislamu wanalifahamu neno hili, ima kwa maana ya kurejea katika jambo lilitolewa. Au kugundua ukweli uliokuwa haujulikani katika wakati uliopita. Na hizi maana zote mbili zinatofautiana na maana sahihi. Na kama tulitumia neno annaskhi kwa maana ya ''kupata elimu mpya'' katika elimu ya Allah Mtukufu – yaani katika sekta ya maarifa ya kinadharia – hilo litakuwa ndio ukafiri wenyewe na haliingii akilini.

Na kinyume chake katika sekta ya kiutendaji, kwa hakika Annaskhi imepatikana kiuhalisia kabisa katika mafundisho ya dini moja. Na katika mafundisho ya dini moja hadi nyingine. ''Hakika walikwambieni hivi na mimi nakwambieni kitu kingine''. Je, kanuni za Mwenyezi Mungu zinafutwa eti kwa kuwa uzoefu umethibitisha kuwa kanuni hizo zinakataana na uadilifu au zilikuwa na makosa? Hakuna mjadala kuwa jambo hilo halikubaliki moja kwa moja katika jambo la uwekwaji wa sheria za Mwenyezi Mungu zilizoteremshwa. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu harejei nafsi yake wala harejei katika maamuzi yake. Na kanuni iliyopita na kanuni iliyopo zote mbili zina utakatifu. Na kila moja katika hizo imewekwa katika zama zake. Na ilikuwa ikiwakilisha hekima ya pekee. Kwa hiyo, mabadiliko yanajificha katika matukio ya kihistoria na ufumbuzi wa aina mbali mbali unaolazimika kwa wakati huo. *((Na vivyo hivyo tumekufanyeni umma bora (kama qibla chenu tulivyokifanya bora) ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi*

---

[1] Nayo inajumuisha mkanganyiko tangu zamani, na maana yake ni kufanya ufutaji wa maandishi kama linavyomaanisha kubatilisha. Na hutumika katika kanuni au sheria kwa maana ya ''kusimamisha utekelezaji wa kanuni kwa muda fulani''. Lakini pamoja na kuipanua maana yake baadhi ya wafasiri wa Quran wanalitumia neno hili kwa maana ya kila ufafanuzi au kuweka mipaka ya kile kinachojulishwa na ibara yoyote. Na kwa hakika Ibnu Hazim alilitumia sana neno hili kwa maana hii ya mwisho. Naye akazingatia ibara ''Ila'' ''na lakini'' ni kufuta maana ya jumla au iliyoashiriwa. Mfano wa matumizi haya ya ajabu: mwanzoni mwa sura ya Muzzamil, Ibnu Hazim anasema: ''Isipokuwa kidogo'' imefuta neno ''usiku'' na neno ''nusu yake'' limefuta ''Isipokuwa kidogo'' na limefuta' ''nusu yake''. Anahesabu sehemu tatu za kufutwa katika aya hii. Je, utashangaa pale anaposema katika Quran kuna ufutaji 224. Kwa hakika Mustashiriquna wameiokota idadi hii bila ya kuichukua njia ya Ibni Hazim katika hesabu zao, na wakaongeza mengi katika hili.. Wakasema kuwa hii ndio idadi ya kupingana kwenye Quran inayokubaliwa na Waislamu wenyewe. Kwa kuizingatia kuwa kupingana huko kumetokana na mabadiliko ya kisiasa (Kitabu kilichotangulia Renan uk 1079) (Na S. Tisdall katika ''vyanzo vya Quran'' kwa Kingereza uk 278).

*juu yenu. Na hatukukifanya qibla ulichokuwa nacho (mara ya kwanza kuwa ndio qibla chako sasa na mpaka mwisho wa ulimwengu) ila tupate kumjulisha (atambulikane) yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma. Na kwa yakini lilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale aliowaongoza Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuipoteza Imani yenu...))* Al-Baqarah 143.

Na wakati mwingine maelezo ya kwanza yanajieleza kuwa yenyewe ni ya muda tu. *((… Basi (nyinyi Waislamu) sameheni na puuzeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake…))* Al-Baqarah 109. Na *((… basi wazuieni majumbani mpaka mauti yawafishe au Mwenyezi Mungu awafanyie njia nyingine…))* An-Nisaa 15. Na mara nyingi hilo linakuwa limestiriwa. Kwani mtunga sheria mwenye kufanikiwa huwa anabadilisha mfumo wa watu kwa mujibu wa maendeleo ya uwezo wao wa kutenda, na uwezo wao wa kufahamu na kutambua. Ili kutengeneza nafsi zenye nuru na tabia madhubuti na umma wenye nidhamu.

Mambo waliyoyaonesha Mustashriqina hapa na sisi kuyavunja kwa hoja – yalitokana na uhakiki ndani ya mafunzo ya Quran – yalikuwa yanalenga kutafuta uwepo kwa baadhi ya vithibitisho vya kidini huko Madini, vinavyothibitisha kuwa kulikuwapo na uhusiano baina ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake na baina ya watu wa Kitabu. Kwa hiyo, kwa njia hiyo Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipokea elimu kutoka kwao. Sasa kwa nini tangu mwanzo jambo lao hili hawajatuletea huyo mtu au hao watu ambao Muhammad rehema na amani ziwe juu yake alipokea elimu kutoka kwao? Hakuthubutu hata mwanahistoria mmoja anayehishimu kubeba jukumu la kielimu kufanya jambo hilo.

Lakini iweje kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake asiwe na mawasiliano na wasomi wa Kiyahudi na hali ya kuwa yeye anaishi katikati yao? Walikuwa na msimamo gani kwake? Quran inatuongoza katika jambo hili, na inawagawa hao wasomi sehemu mbili: asilimia kubwa walikuwa wanaupinga Uislamu hata kabla ya kuhama kwake. Na walikuwa wanaficha elimu zao kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Na walijaribu kumuhadaa na kuweka vikwazo katika njia yake. Na wakati mwingine kwa kupitia njia ya ndugu zao walikuwa wakimuuliza maswali ya kumshindishwa kuhusu roho. *((Wanakuuliza habari ya roho. Sema: ‘‘Roho ni jambo lililohusika na Mola wangu (Mwenyezi Mungu)…)) Bani Israil 85. Na kuhusu baadhi ya mitego na vitendawili vya kihistoria. ((Je! Unafikiri ya kwamba (wale) watu wa Pangoni na (wenye*

*habari) zile zilizoandikwa (vitabuni) walikuwa ajabu katika ajabu Zetu?))* Al-Kahf 9. Pia walimtaka ateremshe kitabu kutoka mbinguni. *((Watu waliopewa Kitabu (Mayahudi) wanakutaka uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni. Na kwa hakika walimtaka Musa makubwa kuliko haya; wakasema: ''Tuoneshe Mungu wazi wazi''... ))* An-Nisaa 153.

Na wakati mwingine wanapinga maandiko yaliyothibitishwa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa yapo katika vitabu vyao na walikuwa hawakubali hadi pale atakapowapa changamoto na kuwashinda na kuthibitisha udanganyifu wao. *((Kila chakula kilikuwa halali kwa kizazi cha Israili (Mayahudi) isipokuwa kile alichojiharamishia Israili mwenyewe – kabla haijateremshwa Taurati. Sema: ''Leteni hiyo Taurat muisome ikiwa mnasema kweli.'' Na wowote watakaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya haya, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao)...))* Aali Imran 93 – 95. Na *((Na watakuwaje wewe kuwa hakimu wao, nao wanayo Tauratu yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanakengeuka (unapowahukumu). Na hao si wenye kuamini (lolote; basi tu wanafanya khadaa))*. Al-Maidah 43.

Na hivi hivi tunaona kuwa wasomi hawa wa Kiyahudi walikuwa wapo mbali mno na msimamo wa kumfundisha au wa kumkaribisha. Na katika kinyume chake, kulikuwa na kundi lingine dogo la wanazuoni wa Kiyahudi ambao walishindwa kuvumilia madai ya kibaguzi ya wenzao, wakahudhuria ili wamsikilize na kuupima uso wake. Na pale walipomjua, – kutokana na baadhi ya alama zake zilizopo katika vitabu vyao – pale pale walimshuhudia kuwa utume wake ni wa kweli. *((Wale (katika Ahli Kitabu) tuliowapa Kitabu (Tautari, Injili, Zaburi...) wakazisoma kama ipasavyo kukisoma (bila ya kupotoa tafsiri yake wala kutoa hili na kutia lile). Hao huiamini hii (Qurani wakasilimu)...))* Al-Baqarah 121.

Na aliyekuwa mashuhuri zaidi miongoni mwao ni Abdullah bin Salaam. Ambaye Wayahudi walikuwa wanamchukulia kuwa ndiye mwenye elimu zaidi miongoni mwao na ndiye mwenye tabia nzuri zaidi, na hayo yalikuwa kabla ya kutangaza kusilimu kwake mubashara. Na punde tu alipotangaza kusilimu, walimpinga na kumkanushia yote hayo katika kikao hicho hicho. Na baina ya haya makundi mawili, historia haikuwaachia nafasi ''marafiki walimu''.

Ama yale madai eti Mtume rehema na amani ziwe juu yake ameipata elimu yake kutoka kwa Abdullah bin Salaam mwenyewe. Kwa hakika hilo

linaingia katika kipengele cha kupotosha ukweli wa kihistoria.[1] Kwa kuchanganya baina ya mfuasi na anayefuatwa. Na unaingia katika moyo wa mpangilio wa matukio ya kihistoria yanayojulikana. Kwa sababu kiini cha ukweli wote wa Taurati ulikuwa umetangazwa katika kipindi cha Makka. Na aya chache tu ziliteremka Madina. Na zenyewe zilikuwa zinahusiana na ukweli wa dini ya Kikristo ambao unapingwa na Wayahudi. Na kwa vyovyote vile wapinzani watakavyotoa juhudi za kujaribu kukusanya nukta za kufanana baina ya ukweli wa Quran na ukweli wa Wayahudi na Wakristo[2].. Hilo halitakuwa kingine zaidi ya kuwa ni kutengeneza silaha zinazoupa faida ukweli wa Quran ambayo inasisitiza kuwepo kwa mfanano huo katika vitabu vilivyoteremshwa na vilivyopita. *((Na haya (yaliyomo katika Qurani) yamo katika Vitabu vya kale (walivyoteremshiwa Mitume wa zamani).* Ash-Shuaraa 196. *((Hakika haya (mnayoambiwa humu katika Qurani) yamo katika Vitabu vilivyotangulia. Vitabu vya Ibrahimu na Musa (na wengineo))*. Al-Alaa 18 – 19. Na kwa hakika ushuhuda wa wasomi wa Kiyahudi ni ushahidi tosha juu ya ukweli wake. *((Je, haikuwa alama kwao kwamba wanayajua haya wanavyuoni wa wana wa Israili (hata wamesilimu)?))* Ash-Shuaraa 197.

Lakini kuafikiana ni kitu kimoja na kunukuu ni kitu kingine. Na baina ya viwili hivyo kuna ombwe kubwa halijabahatika kupata mtu wa kuliziba mpaka wakati wetu huu japo kwa uchache.

---

[1] Pia kuna uchanganyaji wa kihistoria unaofanana na huo, licha ya utofauti mkubwa wa muda kuhusu mchango wao wanaoudai kwa Salmani Al-Faarisiyu na Mariamu Al-qibtwiya. Kiuhalisia Salmani alisilimu baada ya kuhama Makka kwa muda mchache na hakuambatana na Mtume rehema na amani ziwe juu yake ila katika mwaka wa tano katika vita vya Khandaqi. Ama Mariamu Al-qibtwiya alifika mwaka wa saba wa kuhama.

[2] Na jambo hili ndilo lililofanyiwa kazi sana na Doctor (S. Tisdall) akijaribu kuthibitisha kuwa Quran inafungamana na ngano za kihistoria (uk 61 – 62) na kwa makusudi kabisa akajisahaulisha kutaja aina yoyote ya kufanana baina Quran na baina ya Agano la Kale na Agano Jipya. Na badala yake akazama katika kufunua uhusiano wa baadhi ya maelezo ya kina katika Quran kwa yale yaliyokuja katika Talmudi na Athari za Kiyahudi na Kikristo iliyo mbali na Taurati na Injili.

## Hitimisho
## wa Mlango wa sura ya tatu

Tumeshatafiti uwezekano wa kuwepo kwa chanzo cha kibinadamu cha mafundisho ya Quran. Tukamfuatilia Mtume rehema na amani ziwe juu yake, katika maisha yake ya kawaida na maisha yake ya Utume, huko Makka na huko Madina. Katika misafara yake na mawasiliano yake. Pia tulipitia uwezo wake wa kusoma. Na upeo wa kuwepo kwa vithibitisho mikononi mwake. Njia zote za utafiti zimethibitisha udhaifu wa kuwepo kwa chanzo cha kibinadamu na kukosa uwezo wa kuleta uwezekano wowote wa njia za kawaida kuwa ndio chanzo cha Quran. Hii Quran ni jengo refu lenye elimu nyingi iliyohuru katika uga wa dini, historia, tabia njema, kanuni na ulimwengu.. hadi mwisho.

Je, Mtume alijaribu kuyauliza maumbile au kujiuliza mwenyewe? Hilo linawezekana. Lakini jibu ambalo angeweza kulipata lisingekuwa linauvuka ule ukweli wenye utata ulio chini ya yale ambayo mazoea yanaviita vitu kama hivyo ‘‘Dini za kimaumbile’’ na ambazo zinatofautiana na elimu sahihi na ukweli uliochambuliwa katika kila sekta.

Kwa hiyo, ufunuo huu unatoka wapi? Je, sio kutoka ndani kabisa ya nafsi yake? Hakika matukio halisi yanatuthibitishia kinyume na hivyo. Kwani tabia ya fikra zinazomfikia kwa njia ya ufunuo; ima ni kwa njia ya majaribio au ni zaidi ya kiwango cha akili ya mwanadamu. Yaani, yenyewe ipo mbali na sekta ya akili safi. Na hivyo hivyo ipo mbali na hisia zilizofungika katika vyanzo vyake vya kawaida, mfano wa ilhamu wapatazo washairi na wanafalsafa. Kwani jambo linaloonekana ni kwamba ufunuo si fikra zinazofuatana ndani ya nafsi yake. Na hakika si vinginevyo huko ni kusikia sauti safi yaani kwa hakika mawazo hayataenda pamoja na maongezi wala hayatayatangulia.

Mtume mwenyewe rehema na amani ziwe juu yake alikerwa na tukio hili la kusikia hapo mwanzoni mwa hili jambo.. na pale alipotaka kuchukua aya za ufunuo alijikuta amelazimika kulikariri andiko yeye mwenyewe, neno kwa neno wakati wa kupokea ufunuo. Na hakuacha kufanya hivyo ila pale alipopata amri ya wazi pamoja na kuhakikishiwa kuwa Allah atamfundisha yeye na kumfafanulia. *((Wakati tunakusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha. (kukubainishia)).* Al-Qiyama 18 – 19. Neno hili linastahiki

kupewa mazingatio na linatuweka mbele ya ufunuo wa maandiko bila kizuizi wala sharti.

Kwa hakika ufunuo ni uzoefu aliouishi Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Na wale waliokuwa zama moja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake mara nyingi wanapohudhuria tendo la kushuka ufunuo wakiwa ni mashahidi mubashara. Walishuhudia wao wenyewe matokeo ya nje ya tukio la ufunuo. Tukio ambalo kwa upande wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, lilikuwa uzoefu aliouishi na wala hajautengeneza. Hakika hilo ni tukio analolipokea kwa kila hali yake ya ugumu. Na hakuwa na uwezo wa kulikimbia wakati linapomjia. Wala hakuwa na uwezo wa kujiandaa kulipokea anapohitaji hilo.[1] Na zaidi ni kuwa kila somo katika ufunuo lilikuwa ni sura mpya inayoongezwa katika hazina zake ya kielimu. Na mbali ya mwanga huu wa kielimu ya Mwenyezi Mungu. Mtume rehema na amani ziwe juu yake anarudi katika mipaka ya uwezo wake wa kibinadamu. Kwa hiyo mbele ya yaliyopita na yajayo, na mbele ya yale ambayo ni magumu kwa werevu wa kibinadamu uliosalama kupenya pazia yake. Alikuwa hawezi ila kuweka alama za kuuliza kama walivyo watu wengine kwa uaminifu wote na kwa unyenyekevu wote.

Na jambo linalojulikana kuwa msimamo wa Mtume uliojaa hofu na utakatifu mbele ya Quran iliyoteremshwa kwake, imani yake ya kuwa hayo ni maneno ya Allah mwenyewe. Na wakati wa kuyatafsiri, msimamo wake ulikuwa kama msimamo wa mfasiri mwingine mbele ya andiko ambalo sio lake. ((At-tauba 80) ((Al-Munaafiquuna 6)). Alikuwa ana hofu sana juu ya fikra ya kuinasibisha kauli yoyote kwa Allah ambayo Allah hajaisema hata iwe ndogo kiasi gani kauli hiyo. ((Al-Haaqah 44 – 47)). Kama alivyokuwa akihisi kuwa na ulinzi mkubwa kutoka mbinguni na wasimamizi wakimzunguka. ((Al-Jinni 27 – 28)).

Sio sahihi kuwa Quran inaakisi utu wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Mara nyingi Quran haitaji chochote juu yake na wala hutapata mwitikio hata mdogo wa huzuni zake. Na pindi inapotaja kitu basi ni kwa ajili ya kumhukumu au kudhibiti tabia zake muda wa kuwa jambo lenyewe linahusiana na mwenendo wa tabia njema. Na hapa tunapata kupingana kwa waziwazi baina ya mamlaka ya kutunga sheria na nafsi nyenyekevu iliyojisalimisha.. na sio

---

[1] Katika tukio la uzushi ufunuo ulichelewa kwa mwezi kamili na hakukuwa katika uwezo wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kuharakisha au atamke kitu au kuhakikisha au kukanusha uvumi. Na kama jambo lingekuwa mikononi mwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kama lingekuwa linasimama kwake. Je, hakuwa na uwezo wa kueleza maudhui hiyo kwa ufundi wake wa maneno kisha ainasibishe kauli yake hiyo katika ufunuo?

jambo la nadra Quran kuwa na somo la lawama kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake hata kwa kosa dogo litokalo kwake kwa kuwa yeye ni mfano wa kuigwa.[1] Na muda wa kuwa yeye hakuwa na mafundisho ya wazi kutoka katika ufunuo yanayohusu jambo fulani. Yeye ana tabia ya kustahi na kuhisi aibu na haya. *((…Wala msiweke mazungumzo, maana jambo hili linamuudhi Mtume, naye anakuoneeni haya; lakini Mwenyezi Mungu haoni haya kusema haki…))* Al-Ahzab: 53.

Ana hisia kali kwa kile atakachosemwa: *((… na ukaficha katika nafsi yako aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa, na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye mwenye haki zaidi ya kumchelea. Basi alipokwisha Zaidi haja yake na mwanamke huyo. Tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa Waislamu kuwaoa wale wa watoto wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao…)).* Al-Ahzab: 37.

Hatoi maamuzi ya mwisho bila ya kusikiliza rai za maswahaba zake. *((Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao (Ewe Muhammad). Na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangalikukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo…)) Aali Imran 159. Anakiri kuwa hajui hatima yake wala hatima ya wengine itakuwaje. ((Sema: ‘‘Mimi si kiroja (mpya), katika Mitume. Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala mtakavyofanywa nyinyi. Sifuati ila yaliyofunuliwa kwangu;…))* Al-Ahqaf: 9.

Lakini punde tu anapopokea elimu yake kwa Ufunuo tunamuona anafikisha ujumbe wake kwa kujiamini na kwa nguvu zote. Na anasimama msimamo wa mwalimu na mlezi wa watu wote; *((Na kama (makafiri) wakikuhoji, basi sema: ‘‘Nimeuelekeza uso wangu kwa Mwenyezi Mungu. Na walionifuata (wamefanya vivyo hivyo).’’ Na waambie wale waliopewa Kitabu na wale wasio na ilimu (makafiri wa Kiarabu na wengineo): ‘‘Je, mmejisalimisha (kwa Mungu)?’’ Kama wakijisalimisha wameongoka; na kama wakikengeuka, basi juu yako ni kufikisha tu…))* Aali Imran 20.

---

[1] Tukichunguza matukio yaliyopingwa na Quran na ambayo yanamhusu Mtume rehema na amani ziwe juu yake, tutashangaa tukiyakuta kuwa yenyewe yanasifika kuwa yana sifa za uchaguzi. Uchaguzi huo ni kuwa mimi nipo mbele ya hali mbili kila moja katika hizo ni halali (Na mara nyingi kunakuwepo na andiko la wazi) ‘Muhammad: 4’ ‘Annur: 62’ ‘Attauba: 80’ ‘Al-Ahzaabu: 4’ ‘Al-Ahzaabu: 48’. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake alichagua jibu lile ambalo aliloliona kuwa ndio linafaa kwa maslahi ya jamii. Na jibu lililokuwa mwafaka zaidi katika hali mbili hizo lipo katika udhalili wake mbele ya akili yoyote ya mwanadamu. (Attauba: 47). Ama katika mtazamo wa hekima ya MwenyeziMungu. Hakika uchaguzi wake ulikuwa na maana ndogo katika daraja za mwanzo kidogo. (katika hali mbili za mwanzo) akimsamehe kidogo (katika hali ya tatu) na ukali kidogo katika (hali ya nne). Au ikilenga lengo lisiloweza kulitekeleza katika (hali ya tano).

Tangu kabla ya kuhama anatangaza kuwa kiini cha ujumbe wake ni kuwaongoa wana wa Israili. Na kwa sifa ya kiujumla ni kuziongoa nyumati zote zilizopokea dini za mbinguni. Na kuwawekea wazi mambo ya hakika katika mizozo na tofauti zao. *((Na hatukukuteremshia Kitabu (hiki) isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitilafiana, na (pia kiwe) uwongozi na rehema kwa watu wanaoamini.))* An-Nahl: 64. *((Na Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa watu wawili (wengine). Mmoja wao ni bubu, hawezi chochote, naye ni mzigo juu ya bwana wake, popote amwelekezapo haleti kheri. Je! Huyu anaweza kuwa sawa na yule anayeamrisha uadilifu, naye yuko juu ya njia iliyonyooka?)).* An-Nahl 76.

Na pale anapotoa hukumu hampendelei yeyote. *((… na useme: ''Naamini vitabu alivyoteremsha Mwenyezi Mungu; na nimeamrishwa nifanye uadilifu baina yenu…))* Ash-Shuura 15.

Nyuma ya msukumo huu imara kuna nguvu kuu; na sio nguvu ya mwanadamu huyu. Na kwa sababu hii tunamuona ana moyo usio tikisika, na imani isiyoyumba akiwa pamoja na Allah na kupata msaada wake. *((Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa mmoja (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake, (peke yao); walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake: ''Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi.'' Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu…))* Attawba 40. Na anaiweka nafsi yake na watu wake katika hatari ya kulaaniana. *((Watakaokuhoji (sasa) katika haya baada ya kukufikilia ilimu (hii na kuwafikilia wao), waambie: ''Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu; na wanawake wa kwetu na wanawake wa kwenu, na sisi na nyinyi; kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.))* Aali Imran 61. Yeye alikubali lakini wale wenye shaka na watiao watu shaka walikataa.

Ama kwa ushahidi huu mwingi usio na shaka, waandishi wengi wa Kikristo[1] – ambao wanatafuta ukweli bila kupendelea - wameafiki kuwa Nabii wa Kiarabu rehema na amani ziwe juu yake, anasifika kwa moyo safi na ukweli wa nafsi, vitu hivi vinamfanya awe mwenye nguvu kubwa mno katika kuwaathiri watu na kuwatosheleza.

[1] Na miongoni mwao ni (Andrae), (J. St- Hilaire), (Carlyle), Goldziher), (Massignon) na Noeldeke) mpaka mwisho.

Hata hivyo, kukubali huko hakukuwapelekea wakiri kuwa huo moyo wake safi unazingatiwa kuwa chanzo cha ufunuo wake ni wa Mwenyezi Mungu. Kwani huenda mtu akawa ni muhanga wa ufahamu wake mbaya bila kujijua. Kwa hiyo ghafla katika ubongo wake kunadhihiri fikra na maelezo ambayo yeye anayadhania kuwa yenyewe ni mapya kabisa. Wakati ambapo kuhalisia mtu huyo anacheua maarifa ya zamani yaliyozikwa katika kina cha nafsi yake. Bali, ni katika jambo linalowezekana kwa mtu kuamini kuwa elimu mpya aliyoipata imemjia kwa njia ya ufunuo na ilhamu. Muda wa kuwa yeye mwenyewe katika nafsi yake anaamini na kuhakikisha imani yake kwa ilhamu yake binafsi. Na hali ya kuwa yeye hajui chochote kuhusu chanzo chake cha kweli.

Isipokuwa huku ni kufahamu vibaya. Na huu ni udhaifu wa kumbukumbu, yote hayo ni matokeo ya hali ya ubongo isio sawa. Na hali hii haina uhusiano wowote na hali ya Mtume tunayoitazama, si kwa upande wa maudhui wala kwa upande wa utu wake. Na kwa upande wa maudhui tunaona kuwa, ima kuna kukosekana kwa vyanzo jamii, na ima kuwepo kwa uvumi wenye utata na wenye kupingana. Haviwezi kusimama na kuelezea kwa nini mstari ulioufuatwa na Quran umenyooka. Pia kueleza hatua zake zilizothabiti zenye maelezo ya kina. Na kwa upande wa utu wake, huku hakuna hata alama ndogo inayoashiria kwa umbali au kwa ukaribu kuwa eti alikuwa na dosari za kiakili. Bali kinyume chake ndio sahihi. Na ushahidi wa (Renan) ni dalili bora juu ya hili, pale aliposema: ‘‘Katu haijapatapo kuumbwa akili mfano wa akili safi ya Muhammad, na katu hajawahi kuwepo kwa mwanadamu anayezidhibiti akili zake kuliko yeye.’’ (rejea iliyopita uk 1080). Na kufanana na ukweli unaotokana na hali mbili hizi. Hilo linaweza kutuongoza katika kutoa maamuzi yetu juu ya upeo wa uchanya wake kwa mujibu wa kiwango cha kuafikiana au kutofautiana kwake.

Na mara tu baada ya kupita kwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, katika mambo mawili haya, anaongea kwa ubongo ulio macho juu ya mawasiliano yake na ulimwengu unaoonekana na ulimwengu usioonekana, kwa maada na kwa roho. Kwa hakika huo ni uzoefu aliouishi, kuurudia rudia na kujihakikishia kutokana na uzoefu huo mara elfu kwa maelfu. Kwa hakika kabisa, na kwa wazi wazi, alimsikiliza mjumbe aliyemsemesha kwa jina la Allah. Na kwa wazi wazi kikamilifu alimuona kwa macho yake akiwa katika umbo lake kubwa mno. *((Kwa hakika hii (Quran) ni kauli (aliyokuja nayo)*

*Mjumbe mtukufu (Jibrili). Mwenye nguvu, mwenye cheo cha hishima kwa Mwenyezi Mungu.))* At-Takwyr 19 – 20.

Na alimuona mara nyingi. *((Moyo haukusema uongo uliyoyaona. (Moyo wake ulisadikisha haya yaliyotokea). Je! Mnabishana naye juu ya yale anayoyaona (daima)? Na (Mtume) akamuona (Jibrili) mara nyingine (kwa sura ile yake ya Kimalaika katika usiku wa Miiraji). Penye Mkunazi wa kumalizikia (Mambo yote). Karibu yake ndiyo kuna hiyo Bustani, (Pepo) itayokaliwa (maisha na hao watu wema). Kilipofunika Mkunazi huo kilichofunika (katika mambo ya kiajabu ya kimbinguni). Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka (uliowekwa))*. An-Najm 11 – 17. Je, inafaa tumpinge mtu mwenye mwili na akili safi iliyosalama, kwa kile alichokiona? *((Je! Mnabishana naye juu ya yale anayoyaona?))* An-Najm 12.

Isipokuwa sisi – sisi wasikilizaji – hatuwezi kupitia uzoefu huo huo. Wala kuuishi kama alivyouishi yeye. Hili ni sahihi, lakini tuna njia za kurejelea zinazotusaidia kuhakikisha kama haya ya Mtume ni maruerue au ni tukio linaloridhiwa na akili. ‘‘linalowatokea wale wenye uwezo wa kupitiliza peke yao’’ au sauti ya Mwenyezi Mungu mwenyewe wa haki ndio iliyomfunulia. Kwa hiyo yatupasa kurejea yaliyomo katika mafundisho yake na madhumuni yake. Na si kukazia na kutosheka nayo tu. Chukua sampuli tatu zifuatazo:

**1 – Hakika za kidini, kitabia njema na kihistoria.**

Tumeona kutokana na mifano ya misingi ya kitabia njema, kuwa hamasa ya aina yoyote au maarifa tata juu ya vitabu vitakatifu haviwezi kutoa hakikisho kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Kuafikiana na kupatana huku kwa kupendeza mno na kwa kushangaza baina yake na baina ya mafundisho yake. Na huenda likawa ni katika jambo lenye faida tukifanya mlinganisho baina ya Taurati na Quran kuhusu sifa za Mwenyezi Mungu, Malaika, Manabii na yale yaliyo nje ya maumbile... Lakini hayo yatakuwa ni kutoka nje ya mada ‘‘mlango huu’’ na itutoshe tu kusema kuwa pale vitabu viwili hivi vinaposhirikiana kuzungumzia maudhui ya aina moja. Kwa hakika kiini cha maana huwa kinafanana baina ya vitabu viwili hivi, kwa kiwango kinachovutia macho. Tena kwa kiasi ambacho, tofauti zao zinakaribia kufungika katika tofauti ndogo ndogo tena za upili. Ni kana kwamba, daima Taurati ilikuwa chini ya jicho la Mtume. Hiyo ni pamoja na kujipambanua kwa Quran kwa kuwa huru katika lahaja na mizani yake. Na kuwa na njia yake katika kuwasilisha masomo. Na mwelekeo wake upande wa kung`amua mafunzo kutoka katika uwasilishaji.

Kwa hakika ‘‘Jules David’’ ameandika katika Makala yenye anuani ‘‘Kuafikiana na Kutofautiana Baina ya Visa vya Kidini Katika Taurati na Quran’’. Anasema kuwa kwa hakika kiini ni kimoja na tofauti si nyingine isipokuwa ni katika maumbo tu, na katika maelezo machache mno.’’

Ijulikane kuwa ‘‘Tofauti’’ zinakuwa katika ‘‘kupingana na kukinzana’’ na jambo hilo ni la nadra sana baina ya hivi vitabu viwili, na tena tofauti hizo zinakubali kutolewa maelezo ya kupatanishwa. Ama kuhusu kuondosha na kuzidisha hayo hayaitwi kutofautiana. Na wale watiao shaka wanategemea tofauti za kipuuzi ili waukatae Uislamu kwa ujumla wake. Wakati ambapo mantiki/akili safi inawataka wawe na msimamo kinyume na huo. Na pale wapokezi wa kuaminika wanapotofautiana, basi tusimame mbele ya nukta zenye tofauti peke yake. Ili tusubirishe kutoa maamuzi yetu au tujaribu kutafiti aina fulani ya kiunganishi kinachoturuhusu kusahihisha baadhi ya mapokeo kwa kutumia mapokeo mengine. Na njia ile ile inayofuatwa katika kuleta kuafikiana na kuziweka pamoja baina ya Injili nne, inapaswa ifuatwe katika kuyatafiti mawaidha na wosia wa kidini waliotuachia Manabii wote wa Mwenyezi Mungu. Kwani wao wote ni wenye kutukuzwa na ni watakatifu. Na kwa hakika wamepitia uzoefu wa kuwasiliana na ulimwengu uliofichikana. Na kwa hakika kuafikiana kwa kauli zao katika kiini cha mafundisho yao kunapaswa kufungua macho ya walioghafilika kuhusu ukweli wao na usahihi wa misingi yao iliyoshughulikia ukweli wa hali ya juu kwa pembe mbali mbali.

**2 – Hakika za kisayansi (Kielimu).**

Na Quran katika wito wake wa kuielekea imani na wema inatumia hakika za kimaumbile za daima, na kuziita akili zetu zitafakari kanuni zilizothabiti – si kwa lengo la kuzisoma na kuzifahamu tu – kwa hakika zenyewe zinakumbusha kuhusu Muumba Mwenye hekima Mwenye uwezo. Na tunaona kuwa hakika zinazotolewa na Quran zinaafikiana kikamilifu na zile za mwisho kabisa zilizofikiwa na sayansi ya kisasa. Kwa mfano chanzo cha jamii ya mwanadamu. *((Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na kifua (mbavu).))* Tariq 6 – 7.

Na hatua za ukuaji wa mwanadamu katika tumbo la mama yake. *((.. kwa hakika tulikuumbeni kwa udongo. (Mzee wenu Nabii Adamu), kisha (tukawa tunakuumbeni nyinyi) kwa manii, (mbegu ya uhai), kisha (yanageuka) kuwa kipande cha damu, kisha huwa kipande cha nyama kinachoumbika, (kinachofanyika sura) na kisichoumbika; ili tukubainishieni (Kudura yetu). Nasi*

*tunakikalisha matumboni tunachokitaka mpaka muda uliowekwa, kisha tunakutoeni kwa hali ya utoto; kisha (tunakuleeni) ili mfikie baleghe yenu…))* Hajj 5.

Na idadi ya maeneo ya giza yanayotumika ndani yake kumuubia mtu. *((Amekuumbeni kwa nafsi moja, kisha akamfanya mwenziwe (mkewe) katika jinsi ile ile, na akakuteremshieni (akakuumbieni) wanyama wanane (hawa wenye nafuu kubwa kwenu) madume na majike. (Ngamia, ng`ombe, kondoo na mbuzi). Hukuumbeni matumboni mwa mama zenu – umbo baada ya umbo – katika viza vitatu. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu; Ufalme ni wake; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?))* Zumar 6. Na chanzo cha viumbe hai ni maji. *((… Na tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai. Basi jee hawaamini?))* Al-Anbiyaa 30. Na kutengenezwa kwa mvua. *((Mwenyezi Mungu ndiye anayezileta pepo ziharakisha mawingu, kisha akayatandaza (hayo mawingu) mbinguni kama apendavyo, na akayafanya mapande mapande, kisha unaona mvua ikinyesha ndani yake…))* Ar-Rum 48. Na umbo la dunia kuwa la kimviringo. *((… hufunika usiku juu ya mchana, na hufunika mchana juu ya usiku. Na amelitiisha jua na mwezi; …))* Az-Zumar 5. Na mviringo wa ardhi usiokuwa wa duara kamilifu katika ncha za dunia. *((… Je, hawaoni ya kwamba tunaiendea ardhi yao tukiipunguza mipaka yake?...)).* Al-Anbiyaa 44. Na jua kutembea hadi katika nukta maalum. *(( Na jua (pia ni alama kwao); linakwenda (maisha) mpaka kituoni pake. Hayo ni matengenezo ya (Mwenyezi Mungu) Mwenye nguvu (na) Mwenye kujua.))* Ya-sin 38.

Na kuishi kwa wanyama katika makundi yafananayo na makundi ya jamii za wanadamu. *((Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake mbili. Ila ni umati kama nyinyi…))* Al An-Am 38. Na ameyaeleza maisha ya nyuki. *((Na Mola wako akamfahamisha nyuki ya kwamba ‘‘Jitengenezee majumba (yako) katika milima na katika miti na katika yale (majumba wanayoyajenga (watu).’’ Kisha ‘‘Kula katika kila matunda, na upite katika njia za Mola wako zilizofanywa nyepesi (kuzipata).’’ Kinatoka katika matumbo yao kinywaji (asali) chenye rangi mbalimbali; ndani yake kuna ponyo (poza) kwa wanadamu…))* An Nahl 68 – 69. Na jozi za mimea na viumbe vingine. *((Ametukuka Mwenyezi Mungu aliyeumba dume na jike katika (vitu) vyote; katika vile ivioteshayo ardhi, na katika nafsi zao (wanadamu), na katika vile wasivyovijua.))* Ya-sin 36. Na kuchavusha kwa njia ya upepo. *((Na tunazileta pepo za kuchavusha…))* Al-Hijr 22.

Lakini ubora na upekee wa Quran hausimamii katika yale inayoyaeleza tu, bali muujiza wake unarefuka hadi kufikia katika yale inayojizuia kuyataja au yale inayoyaacha kwa makusudi.. (kwa mfano suala la roho..).

Mifano iliyopita inajumuisha kuafikiana kwa kustaajabisha mno baina ya ufafanuzi wa Quran yenyewe na baina ya ufafanuzi wa kisayansi uliothibiti baada ya tafiti ndefu katika zama na vizazi vilivyopita. Tafiti zilizoishia na matokeo yaliyothibitishwa kuwa Quran yenyewe ni sahihi. Kwa hisani ya michango ya wasomi waliobobea, kila mmoja katika somo lake maalum. Je, haya yametokea kwa bahati tu? Je, katika zama za ujinga, inawezekana kuwepo na mtu asiye na vifaa husika na elimu ya upasuaji, wala vifaa vya hali ya hewa, wala vifaa vya mazingira, wala vya kisaikolojia kwa wanyama na wanadamu, na vifaa vya matawi mengine mengi ya kisayansi, awezaye kufanya hivi?. (Na zaidi kitabu chake kiwe kimejumuisha utatuzi wa kero za tabia njema, za kidini na za kijamii). Na pia kinatupatia katika kila mada data za kisayansi za ukwelii za milele zisizotikisika. Tena mtu huyo bila ya kuacha athari yake yoyote hata kama ni ndogo mno, inayoonesha zama zake, au mazingira yake au hata katika taswira zake binafsi katika sekta yoyote ile?

**3 – Utabiri wa yajayo.**

Kwa hakika Quran imeeleza matukio yatakayotokea wakati ujao. Na tumeyaona yametokea kama yalivyoelezwa: kwa mfano misimamo mitatu ya wapinzani wake ambayo ni (Kwenda kinyume, kupendelea mwafaka na kumfanyia uadui). Na mwisho wao ukafuatana kwa mujibu wa kila msimamo (njaa, raha na kushindwa).

*((Basi ingoje siku ambapo mbingu zitakapoleta moshi uliodhahiri. Utakapowafunika watu; (wawe wanasema): ‘‘Hii ni adhabu iumizayo’. ‘‘Mola wetu! Tuondolee adhabu (hii) hakika tunaamini’’. Nini faida ya kukumbuka kwao (sasa)? Na alikwisha wajia Mtume abainishaye. Wakampa kisogo na wakasema: ‘‘Amefunzwa (na watu haya, hakuletewa Wahyi; na ni mwendawazimu.’’ Kwa yakini sisi tutaiondoa adhabu kidogo (lakini) nyinyi mtarudia (makosa yenu). Na (wakumbushe) siku tutakayoshambulia mashambulio makubwa; bila shaka sisi ni wenye kutesa (kweli kweli))).* Ad-Dukhan 10 – 16.

Na kabla ya Mtume kuhamia Madina kwa miaka kadhaa Quran ilitangaza kuwa Maqurayshi watashindwa katika vita vya Badri, (vilivyotokea mwaka wa pili tangu Mtume ahamie Madina) na wakati huo huo Wafursi watashindwa na

Warumi. *((Warumi wameshindwa. Katika nchi iliyokaribu (na nchi ya Bara Arabu. Nayo ni Shamu); nao baada ya kushindwa kwao, watashinda. Katika miaka michache; amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla (yake) na baada yake; na siku hiyo Waislamu watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu (atakayowapa wao. Nayo ni kuwashinda Makureshi siku hiyo). (Mwenyezi Mungu) humnusuru amtakaye; naye ni Mwenye nguvu (na) Mwenye rehema.))* Ar-Rum 2 – 5. Na kueleza pigo la upanga puani alilolipata Al-Waliid Ibnu Al-Mughiira. *((Tutamtia kovu juu ya pua yake, (tutamdhalililsha).))* Al-Qalam 16.

Na kubakia milele kwa mahubiri ya Quran licha ya kupita miaka mingi. *((… Basi lile povu linapita kama takataka tu basi; lakini vile vinavyowafaa watu vinakaa katika ardhi…))* Ar-raad 17.

Na kusimama kwa dola changa ya Kiislamu duniani. *((Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia Amani baada ya hofu yao…))* An-Nur 55.

Na nguvu zote za duniani zimeshindwa kuumaliza wito wa Quran. *((Hakika wale waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuilia (watu wasipate kuamini) njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watazitoa, kisha zitakuwa majuto juu yao, kisha watashimdwa…))* Al-Anfal 36.

Na kuhusu mustakbali wa Ukristo (ni mipasuko na kutofautiana mpaka siku ya Kiama). *((Na kwa wale waliosema: ''Sisi ni Wakristo,'' tulichukua ahadi kwao, lakini wakaacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa, kwa hivyo tukaweka baina yao (wenyewe kwa wenyewe) uadui na bughudha mpaka siku ya Kiama…))* Al Maidah 14.

Na kutawanyika kwa Wana wa Israili katika nchi za dunia na kusongwa kwao, na haja yao ya daima ya kuwa na mshirika. *((Wamepigwa chapa ya dhila mahala popote wanapokuwako; ila (kwa kushika) kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu au kamba ya watu (wawasaidie; lakini wenyewe peke yao hawajitoshelezi). …))* Aali Imran 112.

Na Ukristo kuupita Uyahudi hadi siku ya Kiama. *((… na nitawaweka wale waliokufuata, juu ya wale waliokufuru, mpaka siku ya Kiama…))* Aali Imran 55.

Na hivi hivi yanapatikana kwa wingi matukio yaliyopita, ya sasa na yajayo katika sekta za uhalisia na kuendana pamoja na ulimwengu wa kutafakari na kuunga mkono matukio hayo. Je, kutokana na haya yote tunapata nini?..

Imma kwa hakika Allah anatuhadaa na kuuacha ushahidi wote huu usio na shaka uwe unaelemea upande wa uongo wenye kuhadaa na wala hautuachii hata upenyo wa kupata mwanga wa kutusaidia kuling`amua jambo lake. Au imma kuwe kuna ahadi iliyofungwa ikiwa pamoja na uangalifu wa Mwenyezi Mungu, na kwa muktadha wake umekesha na wito huu ili kuulinda na kila aina ya kuteleza.

Kwa hakika Quran si zao la kienyeji (la eneo moja tu), kwa sababu mambo ya hakika yanayoelezwa na Quran ni katika aina ya mambo yaliyo mepesi kwa akili za aina zote kuyafahamu na kupata faida ya kitabia njema kutokana na mambo hayo. Na kwa hili tunaona kuwa nafasi/cheo cha Quran ni cha juu zaidi ya mazingatio yote ya kijiografia na kiubaguzi.. Na kwa ajili hii, kwa ujumla Quran haitaji majina ya watu wala maeneo inayoyasimulia. Na kwa hakika yenyewe inazingatia zaidi ujumbe na mafunzo yanayopatikana na kutoa faida katika malezi ya mwanadamu.

Kwa hakika mtaala (mpango, mkakati na mbinu) huu uliokamilifu, ndio wa kipekee unaopatikana katika Quran peke yake. Mtaala huu kwa dhati yake nao ni hoja tena hoja ya aina yake. Kwa hakika wito wa Quran umeenea, mwanzoni ukianzia peninsula ya Uarabuni baina ya Waarabu. Lakini lengo lake likiwa ni kuwafikia watu wote.

# REJEA

## A – Rejea za Kiarabu:


| | | | |
|---|---|---|---|
| Ibnu Abii Daaud | Kitaabu Almaswaahifu | Almatwibaatu Arrahmaaniya Bilkaahirah. | 1936 A.D |
| Ibnu Saad | Attwabaqaatu | 8 Ajizaai Twabaa Lubnaana | 1335 H. |
| Ibnu Nnadiim | Alfahrasatu | Twabaa Liibziiji | 1872 A.D. |
| Ibnu Hishaam | Siiratul Arrasuul | Juzuaani Twabaa Swahiih Bilkaahirah | 1929 A.D. |
| Abuu Daaud | Assunani | 4 Ajizaai Twabaa Alkhasshaab Bilkaahirah Alaa Haamishi Azzurqaaniyyi Ala Almuwatwai | 1310 H. |
| Albukhaariyyu | Aljaamiu Asswahiihu | 9 Ajizaai Twabaa Bulaaqi Bilkaahirah | 1289 H. |
| Attirmidhiyyu | Aljaamiu (Au Assunanu) | Juzuaani Twabaa Bulaaqi Bilkaahirah | 1292 H |
| Diraazu | Annabau Al-Adhiimu | Twabau Almuliijiyyi Bilkaahirah | 1352 H. |
| Arraaziyyu | Mafaatihul Ghaibi (Almaarufu Bitafsiiri Alkabiiri) | 6 Ajizaai Twabaa Bulaaqi Bilkaahirah | 1278 H. |
| Rastaduufaaniy | Taarikhu Alqurani Walmaswaahifu | Twubia Bitwarisiiburji | 1323 H. |
| Azzanjaaniyyu | Taarikhu Alqurani | Twabau Lajnati Attaaliifu Wattarjamati Wannashri Bilkaahirah | 1935 AD. |
| Assuyuutwiyyu | Al-Itiqaanu fii uluumi Alqurani | Juz-aani Almatwibaatu Al-Azhariyyati Bilkaahirah (Alaa Haamishi Tafsiiri Aljalaalayni). | 1344 H. |
| Assuyuutwiyyu | Aljaamiu Asswaghiiru (Maa Ziyadaati Allatii Dhwammahaa Ilayhi Annabahaaniyyu | 3 Ajizaai Twabau Alhalabiyyi Bilkaahirah | 1350 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Wajamaahumaa Tahta Ismi Alfat-hi Alkabiiri) | | |
| Assuyuutwiyyu | Addurru Almanthuuru | 6 Ajizaai Twabau Alhalabiyyi Bilkaahirah | 1314 H |
| Twaahiru Aljazaairiyyu | Attibiyaanu libaadhil Mabaahithul Mutaaliqati Bilquran | Twabau Darul Manaari Bilkaahirah | 1934 AD |
| Al-Uqqaadu | Allahu | Twabau Darul Maarifi Bilkaahirah | 1947 AD |
| Maaliku | Almuwatwau | Juzuaani Bisharhi Assuyuutwiyyi – Twabau Alhalabiyyi Bilkaahirah | 1349 H. |
| Muslimu | Asswahiihu (Au Aljaamiu Asswahiihu) | 8 Ajizaau Twabau Istanbuuli | 1334 H. |
| Annabahaaniyyu | Al-Anuwaaru Almuhammadiyyatu | Twabau Bayruuti | 1312 H. |
| Annawawiyyu | Tahdhiibu Al-Asmaai Wallughaati | Twabau Landan (Jam-iiyatu Nashri Annuswuswi Asshar-qiiyati) | 1847 AD. |

## B – Rejea zisizo za Kiarabu:


| | | |
|---|---|---|
| La Bible | trad fr. par Louis Segond | Imprim. Univ. De Cambridge, 1932 |
| L'Encyclopédie de l'Islam | Par les principaux Orientalistes | Leide 1908-1938 |
| Andrae | Mahomet, sa Vie et sa Doctrine | Ed. Paris, Maisonneuve, 1945 |
| Barthélemy-St-Hilaire | Mahomet et le Koran | Paris ‹Didier ‹1865 |
| Caussin de Perceval | Essai sur l'histoire des Arabes avant l'Islamisme, pendant l'époque de Ma-homet et jusqu'à la ré-duction de toutes les tribus sous la loi muslumane | 3 vol. Paris, 1847. |
| Chidiac | Voir Al-Ghazali "Réfutattion Excellente de la divinité de JésusChrist d'après les Evangiles traduit et commenté par Robert Chidiac | Paris ‹Leroux 1933 |
| David | Analogies et Divergences entre les Légendes de la Bible et du Koran | Revue Socio. Et Hist. IVe série. T. Il., Mars 1884. |
| Draz | La Morale du Koran | Le Caire, Al-Ma'aref 1949. |
| Al-Falaki (Mahmoud) | Mémoire sur le Calendrier Arabe avant l`Islamisme et sur la Naissance et l`Age du Prophéte Mohammed | Asiantique, Paris, 1858 |
| Gaudefroy-Demombynes | L'Islam | Paris, Alcan. Extrait de: Histoire et Historiens, depuis cinquante ans (1876 - 1926). |
| Gautier | Moeurs et Coutumes des Muslumans | Paris Payot, 1931 |
| Goldziher | Le Dogme et la Loi de l'Islam. Trad. Fr. Par Félix Arin. | Paris ‹Geuthner, 1920. |
| Huart | Une Nouvelle Source du Koran | Jour. As. Jullet-Août 1904. |
| Jeoffery (Dr). | Materials for the History of the Text of the Qur'an | Leiden 1937. |

| | | |
|---|---|---|
| Jouguet | L'Impérialiasme Macédonien et l'Héllénisation de l'Orient | Paris, Renaissance du Livre, 1926. |
| Kazem (dit Mirza Alexandre). | Observation sur le Chapitre Inconnu du Koran | Jour. As. Mai 1843. |
| Lammens (Père) | Age de Mohammad | Jour. As. Mars-Avril 1911 |
| Lammmens (Père) | Berceau de l'Islam à la Veille de l'Hégire | Rome, 1914. |
| Lammmens (Père) | L'Islam, Croyance et Institutions | Beyrouth, éd Catholique, 1926 |
| Leblois | Le Koran et la Bible Hébraique | Paris, Fishbacher, 1887. |
| Massé | L'Islam | Paris ‹Colin, 1937. |
| Massignon | La mubâhala | Paris, Imp Admini-strative, 1944 |
| Noeldeke | Geschichte des Quràns | Leipzig, 2e éd. 19091938 Leipzig, 2e éd. 19091938 |
| Padwik | Al-Ghazali and the Arabic Gospels | Rev. The Moslem World.1939. |
| Porter | Discours Préliminaire sur la Religion des Mahométants (trad. Fr., mise à la tête de l'Al-Coran de Du Ryer) | Amsterdam, 1775 |
| Renan | Mahomet et les Origines de L'Islamisme. | Revue des Deux Mondes Décembre 1851. |
| Sinclair Tisdall | The Original Sources of the Qur‘an | London, Society for Promoting Christian Knowledge, 1905. |
| Salâma (Dr). | Enseignment Islamique en Egypte | Le Caire, Imp. Nationale, 1939. |
| Sale (Georges). | Observation Historiques et Critiques sur le Maho-métisme (trad. Fr, mise à la tête de l'Al-Coran de Du Ryer). | Amsterdam, 1775 |
| Schwally | See Noeldeke, Geschichte des Qur'ans. | Leipzig, 2e éd, 19091938. |

# YALIYOMO

UTANGULIZI WA MUHTASARI ........ 5

**Ufupisho wa dibaju ya mwandishi** ........ 7

MLANGO WA KWANZA........ 9

UKWELI WA KWANZA ........ 9

WA KIHISTORIA ........ 9

**Utangulizi** ........ 11

**Sura ya kwanza:** ........ 13

**Maisha ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake,** ........ 13

**kabla ya kupewa Utume.** ........ 13

**Sura ya pili** ........ 25

**Namna lilivyokusanywa andiko la Uteremsho wa Hekima** ........ 25

**Sura ya Tatu** ........ 33

**Namna msingi mkuu wa Quran ulivyofikishwa ulimwenguni** ........ 33

MLANGO WA PILI........ 46

QURAN KUPITIA MIONEKANO YAKE MITATU:........ 46

KIDINI, KITABIA NA KIFASIHI ........ 46

**Sura ya kwanza**........ 50

**Haki au ni agenda ya kidini**........ 50

**Sura ya pili**........ 56

**Heri au dondoo ya tabia njema katika Uislamu** ........ 56

**Sura ya tatu**........ 76

**Uzuri na upande wa fasihi**........ 76

MLANGO WA TATU ........ 84

CHANZO CHA KWELI CHA QURAN........ 84

**Sura ya Kwanza**........ 88

**Utafiti juu ya chanzo cha Quran katika sura za Makka** ........ 88

**Sura ya pili:**........ 100

**Kutafiti chanzo cha Quran katika kipindi cha Madina**........ 100

**Mwisho**........ **Error! Bookmark not defined.**

**wa Mlango wa sura ya tatu** ........ 113

REJEA ........ 124

**A – Rejea za Kiarabu:** ........ 124

**B – Rejea zisizo za Kiarabu:**........ 126